

# **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

## **BUNGE LA TANZANIA**

### **MAJADILIANO YA BUNGE**

#### **MKUTANO WA KUMI NAMBILI**

**Kikao cha Ishirini na Saba - Tarehe 18 Julai, 2003**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

#### **D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

#### **HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

##### **NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Shirika la Nyumba la Taifa kwa Mwaka 2000/2001 *(The Annual Report and Accounts of the National Housing Corporation for the year 2000/2001)*

Hotuba ya Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2003/2004.

##### **MHE. KIDAWA HAMID SALEH (k.n.y. MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI):**

Taarifa ya Kamati ya Kilimo na Ardhi kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi katika Mwaka uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2003/2004.

#### **MASWALI NA MAJIBU**

Na. 259

##### **Ubinafsishaji**

**MHE. MARIA D. WATONDOHA** aliuliza: -

Kwa kuwa baadhi ya malengo ya ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma ni kuongeza ajira, soko la wakulima wa Tanzania na kuongeza Pato la Taifa: -

(a) Je, tangu ubinafsishaji huo uanze kutekelezwa, ajira ya Watanzania imeongezeka kwa kiasi gani?

(b) Je, ni mazao gani ya wakulima wa Tanzania yameweza kununuliwa kwa wingi na kuwaongezea kipato kutokana na ubinafsishaji huo?

(c) Je, ni kiasi gani cha fedha kimepatikana kutoka kwa kila Shirika tangu mwaka 1998 - 2002?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maria Watondoha, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifautavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, tangu ubinafsishaji uanze kutekelezwa, ajira ya Watanzania kuongezeka ni wazi na imeongezeka kwa kiasi kikubwa. Mashirika mengi yaliyobinafsishwa sasa yamefufuliwa na yameanza kufanya kazi vizuri na kwa ufanisi na hivyo kuongeza ajira hususan nje ya Mashirika yenyewe.

Mheshimiwa Spika, bidhaa nyingi zinazalishwa na kusambazwa kwa walaji wa hapa nchini na hata nje ya nchi kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji mali na utoaji wa huduma mbalimbali katika Mashirika yaliyobinafsishwa, yote hii ikimaanisha ongezeko la ajira nje ya Mashirika yenyewe.

Mheshimiwa Spika, aidha, ongezeko la ajira ya Watanzania kwa Mashirika yaliyobinafsishwa kama vile Kiwanda cha Bia, Kampuni ya Sigara, Viwanda vya Sementi linajionyesha kupitia kazi zinazofanywa na Sekta Binafsi mfano uwakala, ujenzi, matengenezo, usambazaji na kadhalika. Kiwanda cha Sukari cha Kagera kimeajiri wafanyakazi 1,050 hivi sasa wakati kilikuwa na wafanyakazi 120. Kiwanda cha Sukari cha Mtibwa kimeajiri wafanyakazi 1,800 na ukichanganya wale wa muda wanafikia wafanyakazi 3,000.

Mheshimiwa Spika, Mashirika yapatayo 70 yalikuwa yamefungwa hata kabla ya ubinafsishaji kuanza na hivyo wafanyakazi wote walipoteza ajira zao. Mengi ya Mashirika hayo sasa yamefufuliwa baada ya kupata wawekezaji wapya na hivyo yamejiajiri upya wafanyakazi. Hapa mfano ni Kiwanda cha Mablankeji, Kiwanda cha Kukausha Tumbaku (Morogoro), Kiwanda cha Viatu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inalifanyia tathmini ya kina zoezi zima la ubinafsishaji ili kujua matatizo yaliyojitokeza na mafanikio yaliyopatikana. Tathmini hiyo pia itaangalia suala la ajira mpya zilizopatikana katika uchumi kutokana na mafanikio yaliyopatikana utekelezaji wa zoezi la ubinafsishaji.

(b) Mheshimiwa Spika, baadhi ya mazao ya wakulima Watanzania yaliyoweza kununuliwa kwa wingi kutokana na ubinafsishaji ni Chai (Rungwe na Lushoto baada ya viwanda husika kufufuliwa), Tumbaku (baada ya Kiwanda cha Kukausha Tumbaku cha Morogoro kukarabatiwa na kuanza uzalishaji upya), Pareto (baada ya Kiwanda cha Mafinga kupata mwekezaji), Miwa ya wakulima wadogo wadogo (baada ya Viwanda vya Sukari vya Kilombero na Mtibwa kukarabatiwa na kuongeza uzalishaji).

(c) Mheshimiwa Spika, thamani ya Mikataba ya ubinafsishaji kati ya mwaka 1998 hadi 2002 ni takriban shilingi bilioni 68.7 na takriban Dola za Kimarekani milioni 204.0. Kati ya fedha hizo, jumla ya shilingi bilioni 43.02 na Dola za Kimarekani 64.6 zimekwishalipwa.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, je, atakubaliana nami kwamba ubinafsishaji haujaleta mafanikio makubwa sana hasa kwa ajira, kwa mfano, tukiona mgogoro uliopo sasa *NBC* na wengine wengi ambao wameachishwa katika Mashirika mbalimbali? (*Makofi*)

(b) Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amesema kuna mazao ambayo yameweza kununuliwa kwa wingi kama vile chai na tumbaku. Mikoja ya Lindi na Mtwara ni wazalishaji wakubwa wa korosho; je, Viwanda vya Korosho vya Mtwara na Lindi vingebinafsishwa si kwamba zao la korosho nalo lingepata soko kubwa na Wananchi wa kule kuajiriwa? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, ni dhahiri kabisa zoezi la ubinafsishaji limeongeza ajira, kwa sababu kabla ya zoezi lenyewe kufanyika zaidi ya viwanda 70 vilikuwa vimeshafungwa au vimefilisika na hivyo kupoteza ajira ya wafanyakazi hao. Baada ya viwanda hivi kufufuliwa ajira zilianza upya na kama nilivyotoa mifano katika maeneo mengi, watu wengi wameweza kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la migogoro kama hiyo inayotokea *NBC*, ni lazima tuangalie mahusiano kati ya Menejimenti na Utawala kwa sababu hata katika maeneo ambayo viwanda vimeendelea, migomo kama hii inatokea kutokana na migogoro kadhaa ambayo inajitokeza kati ya menejimenti na wafanyakazi.

(b) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Maria Watondoha, kwamba ikiwa Viwanda vya Korosho vitabinafsishwa au tutapata wawekezaji vitasaidia sana kuongeza kwanza si tu thamani ya zao la korosho, lakini vile vile, upatikanaji wa ajira katika maeneo hayo. Sasa hivi Serikali kwa kushirikiana na Bodi ya Korosho tunafanya jitihada ya kupata wawekezaji wa kuweza kuwekeza katika viwanda vile vya korosho.

Mheshimiwa Spika, tatizo tunalolipata ni kwamba, viwanda vingi teknolojia yake ni ya zamani. Kwa hiyo, wakati wa uwekezaji huo ni lazima kufikiria taratibu ambazo zitafanya wale wawekezaji waweze kumiliki viwanda hivyo na kupata teknolojia mpya ya kisasa ili kuweza kufanya kazi kwa tija na ufanisi. (*Makofi*)

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa baadhi ya viwanda vya korosho vilivyokodishwa kwa watu binafsi vilisababisha kero kubwa. Kwa mfano, katika Kiwanda cha Korosho cha Kibaha, wafanyakazi wake mpaka sasa hivi hawajalipwa pesa na matokeo yake wahusika wamekimbia.

Je, Mheshimiwa Waziri anasema nini kwa wafanyakazi hao? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, wawekezaji waliowekeza na waliokodisha Kiwanda cha Korosho cha Kibaha, kwanza ni wawekezaji wa Tanzania. Taarifa nilizonazo ni kwamba, wawekezaji hawa wamekuwa wakifanya jitihada mbalimbali za kuweza kupata fedha ili kulipa mishahara ya wafanyakazi husika. Sasa hivi kinachojitokeza ni kiwanda hiki kupeleka order ya korosho wapate fedha ili waweze kuwalipa wafanyakazi hao.

Mheshimiwa Spika, ninachosema ni kwamba, siyo kwamba inaleta kero, lakini ukosekanaji wa mitaji na mbinu ya kutafuta mitaji hiyo ndiyo inayofanya ucheleweshaji utokee katika baadhi ya maeneo kama Kiwanda cha Korosho cha Kibaha, lakini kitaendelea vizuri.

Na. 260

### **Kuhusu Utafiti wa Mkondo wa Biashara ya Korosho**

**MHE. ABDULA S. LUTAVI** aliuliza: -

Kwa kuwa inasemekana kwamba Tume ya Kurekebisha Mashirika ya Umma imekamilisha utafiti juu ya mkondo wa biashara ya Korosho kwa nia ya kubaini manufaa ya kiuchumi ya kuuza korosho ghafi na zile zilizobanguliwa:

(a) Je, utafiti huo umechukua muda gani na matokeo yake ni nini?

(b) Baada ya matokeo ya utafiti huo; je, sera ya nchi yetu kuhusu uwekezaji kwenye Viwanda vya Kubangua Korosho itachukua mwelekeo gani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdula Lutavi, Mbunge wa Tandahimba, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, utafiti juu ya mkondo wa biashara ya korosho ulichukua kiezi sita na matokeo yake yamebainisha yafuatavyo:-

(i) Tani 4.5 za korosho ghafi hutoa tani 1 ya korosho zilizobanguliwa. Bei ya mauzo ya tani 4.5 za korosho ghafi ni Dola za Kimarekani 3,375, ambapo tani ya korosho iliyobanguliwa ni Dola za Kimarekani 5,000. Kwa kuza korosho iliyobanguliwa nchi inapata mapato zaidi.

(ii) Kuwepo viwanda vya ubanguaji kunawezesha kupatikana *by products* kama vile *Cashew Nuts Shell Liquid (CNSL)* na maganda ya korosho ambayo hutumika katika kutengeneza chakula cha mifugo *by products* hizi pia huingiza mapato.

(iii) Kuwepo viwanda vya ubanguaji kunaongeza ajira kwa Wananchi na pia soko la chakula kwa wakulima wa zao la korosho. Utafiti umebainisha kuwa viwanda vyenye uwezo wa kuzalisha tani 10,000 vinaweza kuajiri kati ya wafanyakazi 700 hadi 1,000.

(iv) Ajira zaidi zitapatikana kwenye Kampuni zinazohusiana na Viwanda vya Korosho kama vile karakana za kukarabati na kutengeneza vipuri vya Viwanda vya Korosho.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe pia, hivi sasa soko la korosho zetu ni soko tegemezi ikiwa korosho ghafi zinazuzwa India ambapo baada ya muda si mrefu India itakuwa imejitosheleza katika uzalishaji wa korosho ghafi na hivyo kutoagiza korosho toka nje. Hivyo, utafiti huo ni changamoto kwa Taifa katika kuwezesha kuinua zao la korosho nchini kabla hali haijawa mbaya.

(b) Mheshimiwa Spika, baada ya matokeo ya utafiti huu Serikali imeweka kipaumbele kuhamasisha wawekezaji kukodisha au kununua Viwanda vya Korosho ili kuzalisha na kuendeleza biashara ya korosho zilizobanguliwa. Kwa kuweka msukumo zaidi Bodi ya Korosho, ikishirikiana na Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma inafanya juhudi za kutafuta wawekezaji ndani na nje ya nchi katika kuwekeza katika Sekta ya Korosho. Hii pia ni changamoto kwa Waheshimiwa Wabunge na hasa wanaotoka maeneo yanayozaisha zao la korosho wasaidie katika juhudi hizi za kutafuta wawekezaji katika Viwanda vya Korosho nchini.

**MHE. ABDULA S. LUTAVI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Baada ya majibu aliyotoa Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Pamoja na orodha ndefu ya faida ambazo zinatokana na uamuzi wa kubangua korosho hapa hapa nchini, kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri na kwa kuwa sasa hivi ni viwanda viwili tu katika vile 11 ambavyo vilikuwepo katika miaka ya 1970 ndivyo vimekarabatiwa na vinaweza kufanya kazi, je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba, ipo busara kubwa ya kuangalia utaratibu mzima wa ubinafsishaji wa viwanda hivyo ili iwezekane kwa Serikali kufanya mbinu zote zinazowezekeka kuhakikisha kwamba viwanda hivi vinafanya kazi kwanza kabla hatujamtafuta mtu wa kuwekeza? Maana utaratibu huu wa kuwapa watu viwanda ambavyo vimekufa miaka mingi haujatuletea matunda mpaka sasa hivi.

(b) Kwa kuwa huko tulikotokea viwanda hivi vilikuwa mali ya iliyokuwa Mamlaka ya Korosho Tanzania. Nini nafasi ya Mamlaka ya Korosho kwa maana ya umiliki wa hivi viwanda, hivi leo na huko tunakokwenda kwa kutuletea sera hii ya ubinafsishaji na kazi inayofanywa na *PSRC?* (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, ni vema sasa Serikali tukatafuta utaratibu mzuri wa kubinafsisha hivi Viwanda vya Korosho ili viweze kufanya kazi badala ya vile vyote 12 vilivyowekezwa kufanya kazi. Tatizo linalojitokeza hapa ni kwamba, wawekezaji wengi wamekuwa hawapendelei viwanda hivi kwanza kama nilivyosema, kwa sababu ya teknolojia duni.

Kwa hiyo, inawezekana kabisa mwekezaji akawa ananunua kiwanda na mashine, lakini kumbe ananunua *godown!* Sasa, katika hali hii, Serikali itaangalia utaratibu wa kuona ni jinsi gani wawekezaji hawa wanapewa motisha ya kuwekeza.

Aidha, katika suala zima la kungalia bei za viwanda vyenyewe au teknolojia ya viwanda vyenyewe au menejimenti ya viwanda vyenyewe ili viweze kufanya kazi, jinsi tunavyozidi kuendelea katika suala zima la ubinafsishaji tunaolewa wazi kwamba katika uzalishaji, Bodi ya Korosho inaweza ikawa na jukumu kubwa sana la uzalishaji lakini katika usindikaji (*processing*) hili litaachiwa wawekezaji binafsi kuendelea na ubanguaji wa kuendeleza viwanda hivyo vya korosho.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Waziri mwenyewe amesema hapa kwamba, kuwepo kwa viwanda vingi ndiyo kutakakoisaidia nchi hii kuwa na mapato makubwa zaidi kutokana na zao la korosho:

Je, kwa kuwa yeye ni Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji, analiambia nini Bunge hili na Wananchi kwa jumla, kwamba atakuja na mipango gani ya kuhakikisha kuwa kuna viwanda vidogo vidogo nchini vya kubangua korosho ili Watanzania waweze kupata manufaa zaidi kwa zao hili la korosho? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, kama Waziri wa Mipango ya nchi nzima, ninayeangalia mwenendo wa uchumi wetu, kwa sasa sifurahii wala sisherehekei na Serikali pia haifurahii wala haisherehekei baadhi ya viwanda hivi kutokufanya kazi, kwa sababu tunajua viwanda hivi visipofanya kazi *opportunity cost* yake ni kubwa kwa uchumi kuliko kama vingefanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho naweza kuliambia Bunge hili ni kwamba, bado tutaendelea na mikakati yetu ya uwekezaji katika viwanda hivi, lakini hapo hapo tukiangalia ni zipi kero kubwa zinazofanya wawekezaji wasivutiwe, tuziondoe hizo. Wawekezaji wavutiwe ili viwanda hivi viweze kufanya kazi, tuweze kutoa korosho zilizobanguliwa kwa kiwango kikubwa kuliko sasa.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIAHARA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji, naomba kutoa nyongeza ifuatayo: -

Mheshimiwa Spika, Wizara yetu imepitisha Sera ya Viwanda vidogo vidogo na kama mlivyosikia kwenye Bajeti ya Waziri wa Fedha, tumetenga shilingi milioni 500 ambazo ziko *under Credit Guarantee Scheme* ya kusaidia viwanda vidogo vidogo. Kwa hiyo, napenda niwafahamishe Waheshimiwa Wabunge wanaokaa katika Majimbo yanayotoa korosho wawasiliane nasi ili tutazame uwezekano wa kuwapatia fedha hizo za kununua mashine ndogo ndogo za kubangua korosho. (*Makofi*)

Na. 261

### **Uchunguzi wa Vifo mbalimbali**

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE** aliuliza:-

Kwa kuwa ni wajibu wa Polisi kufanya uchunguzi wa vifo mbalimbali pamoja na vile vya kujinyonga na kutumbukia majini na kwa kuwa katika sehemu nyingi za Vijijini huduma za Polisi ziko mbali hivyo husababisha usumbufu mkubwa kwa Wananchi ukiwemo ule wa kuacha shughuli zao na kulinda maiti hizo kwa siku kati ya tatu au tano:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kurekebisha kasoro hizo na utaratibu mzima ili kuwapunguzia kero Wananchi hasa wale wa Vijijini?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Kipole, Mbunge wa Msalala, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa ni wajibu wa Polisi kisheria kufanya uchunguzi wa vifo mbalimbali pamoja na makosa mengine ya jinai yanayotokea sehemu yoyote ile ndani ya nchi yetu na ni kweli pia kuwa sehemu nyingi za Vijijini zipo mbali na Vituo vya Polisi na hivyo kukosa huduma za haraka na kusababisha usumbufu kwa Wananchi. Nia ya Serikali ni kuwa na huduma ya Polisi karibu na maeneo yote wanamoishi Wananchi.

Hata hivyo, pamoja na nia hii nzuri bado safari ni ndefu, yapo maeneo mengi nchini ambayo hayana huduma ya Polisi na hasa maeneo ya Vijijini. Mara nyingi Polisi wanachelewa kufika kwenye matukio Vijijini kwa kukosa vitendea kazi hasa magari. Katika hali hii mkakati wa Serikali ni kuongeza Bajeti ya Jeshi la Polisi kwa ajili ya kuajiri Askari wa kutosha, pamoja na kuongeza vitendea kazi kama vile magari na vifaa vya mawasiliano ili kuwawezesha kupata taarifa za matukio haraka na pia kuwawezesha kufika kwenye matukio haraka. Mkakati huo ulianza mwaka 2002/2003 na kuendelea mwaka 2003/2004.

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba tatizo hili ni kubwa na linaleta usumbufu mkubwa kwa Wananchi; je, Serikali inaweza ikakubali angalau kutoa utaratibu wa muda ambao unaweza ukatumika kwa kipindi fulani wakati inajaribu kutatua kero hii?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, Serikali iko tayari kutoa mpango huo wa muda anaofikiria, lakini itabidi tuzungumze na Mheshimiwa Emmanuel Kipole, atushauri kwa mujibu wa mazingira ya kwao ni mpango gani huo ambao tutauzingatia na kutekeleza. *(Makofi)*

Na. 262

#### **Nyumba za Askari Polisi Kijiji cha Mfikiwa - Wawi na Finya - Wete**

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR** aliuliza: -

Kwa kuwa katika hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ya mwaka 2002/2003 Serikali ilieleza kwamba fedha zimetengwa kwa ajili ya kumaliza ujenzi wa nyumba za Askari Polisi zilizoko kwenye Kijiji cha Mfikiwa - Wawi na Finya - Wete na kwa kuwa nyumba hizo zimeachwa bila kushughulikiwa kwa muda mrefu na kusababisha Askari wetu kukosa makazi ya uhakika pamoja na familia zao: -

(a) Je, ni lini (mwezi gani) ujenzi huo utanza tena?

(b) Je, kwa nyumba za Finya - Wete, Serikali inategemea kuongeza nyumba ngapi kwa kuwa zile zilizopo ni chache sana?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Wawi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ya mwaka 2002/2003 Serikali ilieleza kuwa fedha zimetengwa kwa ajili ya kumaliza ujenzi wa nyumba za Askari Polisi zilizopo katika Kijiji cha Mfikiwa.

Tamko hilo la Serikali lilikuwa sahihi na la kweli, kwani katika mwaka wa fedha 2002/2003 Serikali ilitenga jumla ya shilingi 500,000,000/= kwa ajili ya miradi ya ujenzi ya Jeshi la Polisi ikiwa ni pamoja na mradi wa ujenzi wa nyumba za Askari za Mfikiwa/Chake Chake. Hivi sasa kama Mheshimiwa Faida anavyojua, ujenzi wa nyumba 53 za Mfikiwa umekwishakamilika na kilichobaki ni kufikisha umeme tu.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa nyumba za kuishi Askari huko Finya ni chache. Katika kukabiliana na upungufu huo wa nyumba, Wizara imetenga shilingi 35,000,000/= katika Bajeti yake ya 2003/2004 kwa ajili ya ujenzi wa maghorofa matatu ya kuishi Askari huko Finya. Wizara yangu inapenda kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa ushirikiano na ufuatiliaji wa karibu katika utekelezaji wa miradi hii muhimu kwa ustawi wa Askari Polisi.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Mheshimiwa Spika, tunashukuru sana kwa ujenzi wa nyumba za Askari zilizojengwa katika Kijiji cha Mfikiwa - Wawi. Lakini kama tunavyojua, nyumba haiwezi kukaa tu bila mambo muhimu kama hivyo alivyozungumza Mheshimiwa Waziri, umeme, hospitali, viwanja vya starehe pamoja na mambo mengine kama tunavyojua Askari wanayapendelea. Je, shughuli hizo zitafanywa lini?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kuingiza kifungu cha ujenzi wa nyumba za Askari kila mwaka katika Bajeti yake? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, suala la kufikisha umeme tunalifanyia kazi na tunatarajia katika kipindi cha mwaka wa fedha 2003/2004 litakamilika. Hizo huduma nyingine siwezi kumuahidi kwa sababu zinahusiana na Wizara nyingine.

Namuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa nyumba mbalimbali za Jeshi la Polisi kama ambavyo tumekuwa tukifanya huko nyuma. *(Makofi)*

Na. 263

### **Mfuko wa Pembejeo**

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA** aliuliza: -

Kwa kuwa Serikali inaeleza wazi kuwa inajiondoa kabisa katika uendeshaji wa Mashirika ya Umma na hiyo ndiyo sababu ya kubinafsisha Mashirika karibu yote hapa nchini: -

(a) Je, Serikali haioni kwamba kuweka fedha zake za Mfuko wa Pembejeo katika Benki binafsi na kutozwa riba ya asilimia 12 inafanya biashara ya fedha zake kwa mlango wa nyuma?

(b) Je, ni wakulima wangapi wadogo nchini wanafaidika na mkopo huo wa Mfuko wa Pembejeo kama si wafanyabiashara na viongozi tu?

(c) Je, si busara Serikali kutafuta mbinu nyingine ya ukopeshaji ili kuondoa riba hiyo ya asilimia 12 au kuishusha ili wakulima wadogo na Wananchi wa kawaida waweze kutumia huduma hiyo pia kuangalia uwezekano wa kuongeza muda wa kulipa walau ufikie miaka miwili badala ya mwaka mmoja ambao wengi wa wakopaji watashindwa kulipa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mbunge wa Kalambo, naomba kutoa ufafanuzi mfupi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, siyo kweli kwamba Serikali imejiondoa kabisa katika uendeshaji wa Mashirika ya Umma. Bado yapo Mashirika ya Umma ambayo yataendelea kusimamiwa na Serikali, kwa mfano, Vyuu Vikuu vya Dar es Salaam, Sokoine na Mzumbe, Benki Kuu, Shirika la Kuhudumia Viwanda

Vidogo Vidogo (*SIDO*), *NDC*, Bodi za Mazao na kadhalika. Sera ya Serikali ni kujiondoa katika shughuli za moja kwa moja za uzalishaji au za kibiashara na kuiachia Sekta ya watu binafsi kuzifanya shughuli hizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo haya mafupi, saa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, kama ifuatavyo: -

(a) Uamuzi wa kupitisha fedha za Mfuko wa Pembejeo katika Mabenki ulitokana na ukweli kwamba watu wengi waliokopa fedha kutoka kwenye Mfuko kati ya mwaka 1995/1996 na mwaka wa 1998/1999 hawakuzirejesha. Kutokana na tatizo hilo, Serikali iliamua kutumia Mabenki kusimamia fedha za Mfuko huo kwa kuwa wana ujuzi na uwezo wa kufanya hivyo. Riba ya asilimia 12 ni nusu ya riba inayotozwa na Mabenki ya Biashara. Hata hivyo, Wizara imeunda Kamati ya kuangalia uwezekano wa kupunguza gharama na kuongeza ufanisi wa kutoa mikopo kwa lengo la kupunguza riba inayotozwa na msambazaji wa pembejeo.

(b) Hadi tarehe 30 Mei, 2003 Mfuko kupitia Benki ulikuwa umewapatia wasambazaji wa pembejeo (*stockiest*) 64 mikopo ya thamani ya shilingi bilioni 2.074 kwa ajili ya kununua na kusambaza aina mbalimbali za pembejeo nchini. Wakulima wadogo wa korosho, mkonge na kahawa na wafugaji katika Mikoa 17 walifaidika kwa kupata pembejeo zilizounuliwa na kusambazwa na wafanyabiashara waliochukua mikopo kutoka kwenye Mfuko. Ni vigumu kwa Wizara kuwa na orodha ya wakulima wadogo waliopata mbolea. Hata hivyo, tunayo orodha ya wafanyabiashara au wasambazaji waliopata mikopo kutoka Mfuko wa Pembejeo.

(c) Ili kurahisisha upatikanaji wa mikopo kwa wasambazaji wa pembejeo, majadiliano yamefanyika kati ya Benki ya Ushirika ya Wakulima Kagera, Benki ya Wananchi ya Mufindi na Shirikisho la Vyama vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa Tanzania (*SCULT (1992) Ltd*). Aidha, kuanzishwa kwa *SACCOS* na Mfuko wa Pembejeo wa Tunduru ni kati ya hatua zilizochukuliwa na Serikali kufikisha huduma ya mikopo karibu na Wananchi na kuwapunguzia riba. Mikopo ya pembejeo hutolewa katika kipindi cha mwaka mmoja ambapo wasambazaji wanawakopesha wakulima pembejeo wakati wa msimu wa kilimo na mikopo hiyo kurejeshwa baada ya mavuno, ili fedha zinazorejeshwa zikopeshwe kwa wateja wengine. Hivyo, kuongeza muda hadi miaka miwili ni kupunguza uwezo wa Mfuko wa kutoa mikopo kwa msimu unaofuata.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a) Mheshimiwa Spika, kwa sababu Serikali ilipoamua kuipatia Benki ya *Exim* ambayo haina matawi yaliyotandaa nchi nzima, je, Serikali haikubaliani kwamba ugawaji wa pembejeo katika msimu uliopita ulikuwa ni wa makosa kwa sababu wananchi vijijini hasa katika Wilaya mbali mbali hawakuweza kupata mbolea (*evenly*) kwa uwiano unakwenda pamoja?

(b) Kwa sababu Mkoa wa Rukwa ni Mkoa unaolima mahindi na wakulima wake wanahitaji sana mbolea lakini katika Jimbo la Kalambo ni Kata moja tu ndiyo iliyopata mbolea vizuri. Je, Waziri ni vipi atahakikisha katika msimu ujao kata nyingine kama za Mambwe, Msanzi, Mwaje, Matai, Kasanga wanapata mbolea kwa mtindo wa kutumia mfuko huu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tulianza na Benki ya *Exim* kwa sababu kama alivyosema Waziri wa Kilimo na Chakula siku mbili zilipita ni kuwa tulipotangaza kuzitaka taasisi za fedha kujihusisha mpango huu ni Benki ya *Exim* na Benki ya Ushirika ya Kilimanjaro zilizojitokeza na hatukuweza kuwalazimisha mfano *Micro Finance Bank*, *NBC* kwa sababu hawakuwa tayari ndiyo tulianza na hizi. Ukikumbuka katika jibu letu wakati wa Bajeti ilielezwa kuwa sasa tunataka kuwashirikisha taasisi mbali mbali mfano *SACCOS* au sasa tunavyosema *SCULT* inahusika, *Community Bank*, kama Mufindi, mifuko ya pembejeo ya Wilaya yote hii inahusika.



Kwa hiyo, ushauri wangu ni kuwa Mheshimiwa Mbunge arudi nyumbani akahamasishe wananchi aidha, waunde Vyama vya Ushirika vya kuweka na kukopa au tuunde mifuko ya pembejeo ya Wilaya au Halmashauri ya Sumbawanga ihusike na hivyo watanufaika na masuala haya. *(Makofi)*

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Waziri anavyoeleza kuwa tuunde au tuandae hivyo Vyama vya Ushirika au Mashirika yaweze kupeleka mbolea huko, hajui maeneo haya ya kilimo hasa cha uzalishaji wa mahindi na kahawa ilitakiwa mbolea hizi ziwe zimefike sasa na kusambazwa kwa watu? Haoni atachelewa katika kukamilisha haja hii? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Edson Halinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hatujachelewa bado, Vyama vya Ushirika si suala geni vinajulika, kuna *SACCAS* na *SACCOS*, Mifuko ya Pembejo ya Wilaya, Halmashauri zipo. Tulijaribu kwa miaka miwili, mitatu huko nyuma kuelezea kuwa Halmashauri za Wilaya, zijihusishe na matatizo ya wananchi. Huu mfuko siyo wa *donation* ni mfuko wa *BX* uendeshwe kibiashara. Bado narudia kumwomba Mheshimiwa Mbunge, ashirikiane na sisi kuhamasisha wananchi kupitia Halmashauri za Wilaya kusudi taratibu hizi zifuatwe na tutafanikiwa. *(Makofi)*

Na. 264

#### **Mfereji wa Kwesasu**

**MHE. MUSA A. LUPATU** aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula alipotembelea Wilaya ya Korogwe tarehe 18 Agosti, 2001 Wananchi wa Kijiji cha Mkumbara waliomba Serikali kupitia kwake kwamba iendelee na kazi ya kukamilisha kufungua mfereji wa umwagiliaji maji ya Kwesasu ambao ulianza kujengwa kwa intake zaidi ya miaka 20 iliyopita na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri waliwaagiza watumishi wa Kilimo wafanye utafiti na kutoa mapendekezo ya utafiti huo Serikali.

(a) Je, nini matokeo ya utafiti huo?

(b) Je, Serikali imeweka mikakati gani kutokana na matokeo ya utafiti huo kwa makusudi ya umwagiliaji Bonde la Mkomazi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Musa Lupatu Mbunge wa Korogwe Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Tarehe 11 Agosti, 2002 timu ya Watalaamu wa Wizara ya Kilimo na Chakula ilitembelea maeneo ya Bwiko - Kwesasu na kufanya uchunguzi ambao ulibaini kuwa sehemu unapopita mfereji uliochimbwa na wakulima ilikuwa ina mwamba mgumu ambao uliwafanya wasiweze kuchimba mfereji wenye kina kinachohitajika ili kuwa na mporomoko mzuri wa maji. Uchunguzi pia ulibaini kuwepo kwa korongo kubwa ambalo halifai kutumika kama mfereji wa kupitishia maji hadi Ziwa la Manka kwa kuwa lina chumvi.

Aidha, Ziwa Manka lina chumvi na kwa hiyo, maji yake hayafai kwa kumwagiliwa mashambani. Katika eneo hilo, kuna mfereji mdogo wenye haki miliki ya maji kutoka Bodi ya Maji ya Bonde la Mto Pangani. Haki miliki hiyo ni ya lita 112 kwa sekunde kiasi ambacho kinatosheleza umwagiliaji maji kwenye shamba la mpunga la hekta 45 tu au hekta 100 za shamba la mazao mengine kwa mfano mahindi, mikunde nakadhalika.

(b) Katika Bajeti ya mwaka wa 2003/2004 Serikali imetenga shilingi milioni 100 kwa ajili ya kujenga bwana kwenye eneo la Chamamba katika Bonde la Mkomazi kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji katika Vijiji vya Manga Mtindiro, Goha, Mazinde, Mkumbara, Kwenangu, Kasiga na Mabogo. (*Makofi*)

Wakati Bwawa la Chamamba likijengwa, wananchi wa Kwesasu watapewa mafunzo juu ya kilimo bora cha umwagiliaji na mfumo wa umwagiliaji uliopo utaboresha.

**MHE. MUSA A. LUPATU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja.

Kwanza, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na kupeleka shukrani hizi kwa wananchi wa maeneo aliyoyataja. (*Makofi*)

Pamoja na majibu hayo naomba kujua katika mwaka huu wa fedha ambao fedha hizi shilingi milioni 100 zimetengwa matarajio ya kuanza kazi ni mwezi upi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Musa Lupatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tarajio letu ni kuwa tukishatoka hapa, fedha zikaanza kutoka hazina tutaanza kazi hiyo mara moja.

Na. 265

#### **Miradi ya Maji Iliyofanyiwa Mchoro Kitaalam**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imefanya kazi nzuri sana ya kuandaa michoro ya miradi ya Maji ya Kwakidole, *Bumbuli Mission* na Kaya, Funta na Mgwashi:-

- (a) Je, miradi hiyo minne kila mmoja utagharimu kiasi gani?
- (b) Je, Serikali itasaidiaje nguvu za wananchi katika miradi hiyo?
- (c) Je, utekelezaji wa miradi hiyo utanza lini?

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka 1998 hadi mwaka 2003 Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto kwa ushirikiano wa wadau wengine katika sekta ya Maji, wamefanikiwa kukamilisha upimaji na uchunguzi wa miradi mipya ya maji 12. Katika miradi hiyo, miradi 11 imefanyiwa usanifu. Katika Jimbo la Bumbuli pekee, jumla ya miradi iliyopimwa ni 5 na kati ya hiyo minne imefanyiwa usanifu. Miradi hiyo ni pamoja na Kweminyasa (Vijiji vya Mkinga, Shangarawe na *Mponde factory*), Kwakidole (Vijiji vya Kwalei, Kwekitui na Kwadoe, Manga Funta Vijiji vya Manga na Funta, Bumbuli Kaya Vijiji vya Mbokoi, Bumbuli Kaya, *Bumbuli Mission*, Kwanguruwe, Dule na Wema, mradi umepimwa tayari bado unafanyiwa usanifu. Usanifu wa mradi huo unategemewa kukamilika mwezi Julai, 2003 na Mgwashi Vijiji vya Kihitu, Tuliani, Mgwashi na Nkongo.

Katika hatua hizi za awali za kutekeleza miradi ya maji, wanavijiji kwenye vijiji husika walihamasishwa namna ya kulinda na kutunza vyanzo vya maji, kushiriki katika kugharamia upimaji na kutoa maeneo katika mashamba yao. Serikali ilitoa ruzuku kusaidia gharama za usafiri, vifaa na posho za wapimaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa William Shellukindo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Gharama za miradi kwa bei za mwaka 2003 ni kama ifuatavyo:-

Manga Funta - shilingi 246,397,000, Kwakidole - shilingi 372,118,780, Mgwashi - shilingi 82,000,000/=, Bumbuli Kaya gharama zitajulikana baada ya usanifu na makisio kufanyika.

(b) Ili kuunga mkono juhudi za wananchi ambao wameshiriki katika upimaji wa miradi hiyo kwa kutumia nguvu zao, kuunda kamati za maji na kuchangia mifuko ya maji, Serikali itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga miradi hiyo. Aidha, kwa kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto, Serikali imepanga kutumia kiasi cha shilingi 82,000,000/= kukamilisha mradi wa Mgwashi kwa awamu kuanzia mwaka ujao wa fedha.

(c) Utekelezaji wa miradi hiyo utanza mara fedha zitakapopatikana. Aidha, vigezo vya kiasi cha michango na utayari wa wananchi kutekeleza miradi yao vitangaaliwa ili fedha zitakapopatikana zitumike kwa miradi ambayo ni endelevu.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri yenye matumaini na busara nyingi ya Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo naomba kuuliza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa ni ukweli usiofichaka kwamba jungu kuu halikosi ukoko. Je, Waziri atakubaliana na mimi kumsaidia Mhandisi wa Maji wa Wilaya ya Lushoto kiasi kidogo ili aandae michoro ya Kijiji cha Kwangwenda cha wananchi ambao jumata tu hii walinitumia salaam kwamba wanashida ya maji kupitia Kituo cha Ubungo?

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la William Shellukindo, kama ifuatavyo:-

Katika mwaka huu wa fedha tumewasaidia Lushoto shilingi milioni 10. Jungu kuu unalosema sina, analo Mheshimiwa Waziri wa Fedha. (*Makofi/Kicheko*)

Na. 266

#### **Jimbo la Kilwa Kusini**

**MHE. OMAR M. MWENDA** aliuliza:-

Kwa kuwa vijiji vyote kwenye Jimbo la Kilwa Kusini vimetekeleza agizo la Serikali la kutaka kila kijiji kifungue *account* ya maji na kuunda Kamati za Maji na kwa kuwa utafiti umeshafanyika katika vijiji vyote.

Je, Serikali itakubaliana nami kuwa sasa ni muda muafaka wa kuvipatia maji vijiji hivyo?

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Omar Mwenda, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Mbunge na Viongozi wa Wilaya kwa kusaidia kuhamasisha wananchi wakaweza kuanzisha Kamati za Maji, Mifuko ya Maji na kufungua akauti kwa kila kijiji kwa ajili ya kuboresha na kuendesha na utunzaji wa miradi ya maji vijijini.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo naomba kumshauri Mheshimiwa Mbunge ahimise uchangiaji zaidi wa fedha kwa lengo la kutunisha akaunti hizo kila wakati ili ziwe na fedha za kutosha kwa kuweza kuendesha miradi ya maji pamoja na kuitengeneza pale itakapoharibika.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa ni muda muafaka wa kuvipatia maji vijiji hivyo na tayari hatua zimeanza kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu kwa kushirikiana na Serikali ya Japan kupitia shirika lake la *JICA* ilifanya uchunguzi katika vijiji vyote katika Jimbo la Kilwa Kusini wakati wa kusanifu mradi kabambe wa maji ujulikanao kama *Lindi Mtwara Water Master Plan*. Kwa sasa mazungumzo kati ya Serikali yetu na Serikali ya Japan yanaendelea ili kuona ni jinsi gani mradi huo ambao unajumuisha Vijiji vya Kilwa Kusini utakavyotekelezwa.

**MHE. OMAR M. MWENDA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza maswali yafuatayo:-

(a) Kwa kuwa mazungumzo yanaendelea na wananchi bado wana tatizo la maji je, hakuna mbinu zingine za kuweza kupatiwa maji? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa wananchi hawa wametekeleza Agizo la Serikali kutowapatia maji huwaoni kwamba unawavunja moyo? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Omar Mwenda, kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Kwanza si nia yetu kuwavunja moyo wanavijiji. Tunataka sana wanavijiji wawe na moyo na wajitolee kufanyakazi hizi za kusaikia kuwapatia maji. Lakini kama tulivyosema katika Bunge hili, uwezo wa Serikali yetu ni mdogo. Kwa hiyo, tunagawana sungura mdogo. Sungura huyo mdogo ndiyo mwingine anapata makanyagio na kadhalika, hali halisi kwamba sungura ni mdogo. Kwa suala la Kilwa nimemwahidi Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali ya Japan tumeshasema mazungumzo yanaendelea kwa madhumni ya kuanza utekelezaji mwanzoni mwa mwezi Oktoba. (*Makofi*)

Na. 267

### **Mapato Yatokanayo na Uingizaji wa Kanda za *Video* Nchini**

**MHE. MONICA N. MBEGA** aliuliza:-

Kwa kuwa nchi yetu imekuwa ikilaumiwa na nchi nyingine za *SADC* kwa kuingiza nchini kanda za *video* isivyo halali na kwa kuwa takwimu zinaonyesha kuwa Tanzania ndiyo nchi yenye *video players* nyingi kuliko nchi yoyote katika Afrika:-

(a) Je, kwa mwaka 2000 - 2001 Serikali imeingiza kiasi gani cha mapato kutokana na uingizaji wa kanda za radio, *video cassette* na *CDs*?

(b) Je, Serikali imekusanya kiasi gani cha kodi ya forodha kutokana na kazi za wasanii wa nje ambao hurekodi miziki ya Tanzania huko nje ili kupata ubora na kisha kuzirudisha nchini?

**WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Monica Mbega, Mbunge wa Iringa Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mapato yaliyokusanywa na Serikali kutokana na uingizaji nchini wa kanda za radio, *video cassette* na *CDs* katika mwaka 2000/2001 na 2001/2002 ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 2000/2001, ushuru wa forodha (*Import Duty*), Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) kwa jumla vimeingiza shilingi 383,043,991/= . Mwaka 2001/2002, ushuru wa forodha (*Import Duty*) na Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) jumla shilingi 435,659,494/= .

(b) Makusanyo ya ushuru wa forodha unaotokana na kuingiza nchini kanda za redio, *video cassette* na *CDs*, yanahusisha kazi za wasanii zilizorekodiwa nje ya nchi kutoka sehemu mbalimbali za dunia na Tanzania. Takwimu tulizo nazo kuhusu makusanyo hayo hazitenganishi kazi za wasanii kufuatana na nchi waliko. Kwa hali hiyo basi, mapato yanatokana na kazi za wasanii wa nje ambao hurekodi miziki ya Tanzania huko nje ili kuzipa ubora na kisha kuzirudisha nchini yamejumlishwa katika takwimu za miziki iliyorekodiwa huko nje na kuingizwa nchini.

**MHE. MONICA N. MBEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa sababu swali hili ni la siku nyingi sana ni la mwaka 2002 na lengo lilikuwa kuishauri Serikali ili iweze kupata chanzo kingine cha mapato kwa maana *CDs* na *Cassettes* ni chanzo kizuri kwa kuweza kupata mapato mengi na kutoa kodi ambazo ni kero kwa wananchi.

Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba kuanzia Bajeti zijazo itaunda kamati ambayo itashughulikia kwa usahihi kabisa kuhakikisha kwamba chanzo hiki kinaleta mapato ya kutosha kwa sababu kama alivyosema katika taarifa yake fedha zilizozingia kama kodi ni kidogo sana? (*Makofi*)

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Monica Mbega, kuwa nakubaliana naye. (*Makofi/Kicheko*)

Na.268

#### **Malipo ya Fidia kwa Abiria Wanaopata Ajali ya Basi**

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA (k.n.y. MHE. SIMON M. MBILINYI)** aliuliza:-

Kwa kuwa utaratibu wa kukata Bima kwa vyombo vya usafiri hususan mabasi na magari madogo ya abiria ni nzuri sana, karibu au ni mabasi yote huwa yana bima na kwa kuwa tatizo ni kuwa abiria wengi hawajui haki zao hali nusura ikitokea ajali wanaojua kidogo wanaenda bima kudai na Kampuni ya Bima inampeleka kwa mwenye mabasi kudai:-

Kwa kuwa matokeo ni kuwa watu wengi wenye haki za kulipwa bima hawalipwi. Je, ni mapatano kati ya Kampuni ya Bima na wenye mabasi kuwadhulumu abiria wao?

**WAZIRI WA FEDHA** atajibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Simon Mbilinyi, Mbunge wa Peramiho, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, zipo aina tatu za Bima zinazotoa kinga kwa abiria na hivyo kuweza kumnufaisha abiria ambazo kwanza ni kinga ya Kisheria (*Ordinance Cover*) ambayo ipo kwa mujibu wa sheria ya *Motor Vehicle Insurance Ordinance Chapter 169*. Chini ya sheria hii, mmiliki yeyote na gari au chombo cha moto hupaswa kuwa na bima hii ili kumwezesha mtembea kwa miguu (*pedestrian*) kulipwa kifuta machozi endapo atagongwa na kujeruhiwa au kufariki na ya pili ni *Third Party Insurance Cover* kinga hii huchukuliwa na mmiliki wa gari ili kuwezesha kulipwa fidia abiria waliolipa nauli na waenda kwa miguu wakipata ajali kwa kugongwa na gari au chombo cha moto cha mmiliki huyo. Aidha, kinga hii hulipa fidia kwa uharibifu wa mali ya mtu mwingine.

Mheshimiwa Spika, aina ya tatu ni Bima ya Mseto (*Comprehensive Insurance Cover*) kinga hii huchukuliwa na mmiliki wa gari au chombo chochote cha moto kuwezesha kulipwa fidia abiria waliolipa

nauli na waenda kwa miguu endapo kutatokea ajali na wakajeruhiwa au kufariki. Kinga hii pia hulipa fidia kwa uharibifu wa gari ya mmiliki mwenyewe na mali ya mtu mwingine.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kuwa ni kweli kuwa ni matakwa ya sheria kwa mabasi na magari madogo ya abiria kuwa na Bima ikiwa ni kinga kwa mali na waathirika mara ajali inapotokea.

Hata hivyo katika kukata bima hakuna mapambano yoyote yanayofanywa kati ya kampuni ya Bima na wenye basi kuwahudumia abiria wao ajali inapotokea. Zipo taratibu ambazo kampuni za bima zinasisitiza zifuatwe ili kuwezesha abiria kulipwa fidia. Taratibu hizo ni pamoja na wenye mabasi kuthibisha kama mdai alikuwa ni abiria wa basi lililopata ajali ambapo uthibitisho wake ni orodha ya abiria wa safari husika *passenger manifesto*.

Mheshimiwa Spika, endapo uthibitisho huu utakosekana, hapo ndipo kampuni ya bima humtaka mdai kum dai fidia mwenye basi na matokeo yake abiria mdai hujikuta akihangaika. Taratibu ambazo kampuni za bima zimeweka katika kushughulikia madai ya abiria zina lengo la kuhakikisha kuwa wale wanaolipwa fidia ni stahili yao na hakuna udanganyifu wa aina yoyote ule. Hivyo ni vizuri kampuni za mabasi zikawa na utaratibu wa kutunza kumbukumbu za abiria wanaosafiri ili ziwe uthibitisho pale ajali inapotokea.

Aidha, ni muhimu wananchi wakaelimishwa juu ya haki zao za kisheria ili wapatao ajali waweze kufidiwa ipasavyo.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa abiria wengi nchini wanapata hasara kubwa ya kupoteza maisha hata mali yao, lakini hawapati fidia ni kutokana kwamba wananchi hawana elimu ya haki zao. Je, Serikali inafanya utaratibu gani wa kuwaelimisha wananchi ili haki zao zisipotee kama zinavyopotea huko nyuma? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi Serikali haina utaratibu unaoeleweka wa kuwaelimisha wananchi. Hata hivyo, wazo lake ni zuri nitalichukua nikalifanyie kazi. (*Makofi*)

**MHE. DR. MASUMBUKO LAMWAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii.

Kwa kuwa suala la *passenger manifesto* ni wajibu wa mwenye basi na abiria hana uwezo wowote wa kuhakikisha kwamba hiyo *manifesto* inawekwa na kwa kuwa katika usafiri wa mabadi abiria anapewa tiketi. Je, Mheshimiwa Waziri hawezi kuona kwamba huu utaratibu wa kudai *manifesto* ni ujanja wa kuweza kudhulumu abiria ambaye hana *control* na *passenger manifesto* na kwamba ni muhimu *proof* ya safari iwe tiketi na siyo kitu kingine? (*Makofi*)

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, siyo tu kwamba baadhi ya wenye mabasi hawaweki hiyo orodha, lakini kweli vile vile kwamba hata baadhi ya mwenye mabasi hawatoi tiketi zenyewe. Kwa hiyo, eneo hili liko gizani. Kwa sababu Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, ni Mwanasheria nitatumia fursa hii kushauriana naye zaidi ili tuchukue hatua za kuboresha sheria ili Serikali iweze kuchukua hatua za kisheria za kuhakikisha kwamba abiria hawezi kupoteza haki zake kwa sheria siyo kamilifu. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. SALOME J. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali.

Kwa kuwa bima ni moja ya vyombo vya fedha kama ilivyo mabenki ikiwemo Benki ya *NBC* na kwa kuwa Wabunge mara kwa mara wamekuwa wakiitaka Serikali ifanye *intervention* katika masuala kadhaa na Serikali inapata kigugumizi kuwaa-*pre tax* kwamba tuko katika soko huria. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kuna umuhimu wa kufanya *intervention* katika suala la *NBC* linaloendelea kwa sababu *NBC* imetapakaa nchi nzima na hivyo inaweza ikaathiri uchumi? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu anataka kutoa majibu ya swali hilo. (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salome Mbatia, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Suala la *NBC*, Serikali hajjaliachia. Serikali inalishughulikia kikamilifu na ndiyo maana hata Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Mheshimiwa Juma Kapuya, hayupo hapa yuko Dar es Salaam anashughulikia jambo hilo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha kwa hiyo tunaendelea na shughuli nyingine. Vikao vya leo ni kama ifuatavyo:-

Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mwenyekiti wake Mheshimiwa John Malecela, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane mara baada ya Waziri anayewasilisha hoja yake leo kumaliza kuwasilisha hoja yake katika chumba namba 58 Vyumba vya Kamati.

Kamati ya pili ni Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dr. William Shija, anaomba Kamati ikutane baada ya Waziri anayewasilisha hoja yake leo kumaliza kuwasilisha hoja yake, kamati ya Nchi za Nje inakutana chumba namba 56 katika Vyumba vya Kamati.

Kamati ya tatu inayokutana leo ni Kamati ya Fedha na Uchumi, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Lephy Gembe, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane muda huo huo baada ya kumsikiliza Waziri akiwasilisha hoja yake leo.

Mwisho wa matangazo ya Vikao vya Kamati. Kesho kuna semina napenda kuwakumbusha Wabunge seminar ya kesho inahusu Ushirikishwaji Katika Kupunguza Umaskini inadhaniwa na Ofisi ya Makamu wa Rais kwa masharti yale yale ya kawaida. (*Makofi/Kicheko*)

Vikao vya Jumuiya za Vyama vya Hiari vya Wabunge, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Umoja Wabunge Vijana, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, anaomba Wabunge vijana wakutane saa 9.00 alasiri chumba namba 155 ghorofa ya nne. (*Makofi*)

Mwisho Katibu Mkuu wa Chama cha Wabunge cha Kupambana na Ukimwi (*TAPAC*) anaomba Wajumbe wake wakutane leo baada ya kuahirisha Bunge saa saba. Anadhani ni wengi kwa hiyo anaomba wakutane katika ukumbi huu huu.

Saa 7.00 mchana kutakuwa na Kikao cha pamoja cha Tume ya Huduma za Bunge na Kamati ya Wenyevitani mbalimbali Kamati ya Uongozi kutakuwa na Kikao cha pamoja saa 7.00 mchana kwa muda mfupi kwa jambo muhimu. Kwa hiyo, wale wajumbe wa Kamati hizi mbili wale Wajumbe wa *TAPAC* tafadhali wanasemehewa na Katibu Mkuu wasihudhuri *TAPAC* waende kwenye kikao changu. (*Makofi/Kicheko*)

Kuna mabadiliko ya *Order Paper*. Waheshimiwa Wabunge, mtaona kwamba kuna *item* ya uchaguzi mdogo wa kujaza nafasi zilizoachwa wazi. Nimegundua kutokana na vikaratasi vinavyoniuliza kuhusu utaratibu kwamba kwa kweli hatujaweka utaratibu kwa uchaguzi wa aina hii na kwa hiyo wengi hawajui itakuwaje. Kwa ajili hiyo, nimeamua kuahirisha *item* hiyo ya *Order Paper*, tutaifanya wakati mwingine wiki ijayo. Kwa hiyo, *Order Paper* inarekebishwa kwa maana hiyo kwamba *item* Namba 3 inafutwa. Tunaendelea.

## HOJA ZA SERIKALI

### **Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2003/2004 Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi**

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kutokana na Taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi naomba kutoa Hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa Fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutumia fursa hii kutoa pole na salamu za rambirambi kwa Watanzania wote kwa misiba yote iliyotokea katika mwaka wa Fedha 2002/2003. Tumeondokewa na kupungukiwa na nguvu kazi ya kulijenga Taifa letu. Mwenyezi Mungu aendelee kuziweka mahali pema Peponi Roho za Marehemu wote. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa kujiunga na Bunge hili Tukufu mwezi Mei, mwaka huu 2003. Pongezi maalum ziwaendee Wabunge wa CCM kwa kuongeza idadi ya kikosi chetu cha wapiganaji ndani ya Umma wa Tanzania na ndani ya Bunge letu Tukufu. Vilevile napenda kumpongeza Mheshimiwa Ali Said Salim, Mbunge wa Ziwayi kwa kuteuliwa kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Natumaini tutakuwa na ushirikiano mzuri kwa manufaa ya Taifa letu.

Naomba pia nitumie nafasi hii kumpongeza Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Spika, kuwa Wajumbe wa Kamati hiyo muhimu. Wizara yangu imetiwa moyo na imani kubwa kwa jinsi Kamati ilivyoanza kufanya kazi yake kwa makini na uhakika. Kamati hiyo, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mbunge wa Mbozi Magharibi, imetembelea Wizara yangu na imepitia Bajeti ya Wizara yangu na kufanya uchambuzi wa kina. Tunashukuru kwa hoja mbalimbali, ushauri wa busara na maelekezo yaliyotolewa. Wizara yangu inayathamini na itayazingatia katika mkakati wa utekelezaji Bajeti yetu ya mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu limekwishaelezwa na kuzingatia misingi ya jumla ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2003/2004 kama ilivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafishaji. Nawapongeza na kuwashukuru wote kwa hotuba zao nzuri.

Baada ya kuzingatia misingi hiyo ya jumla, hoja yangu itajielekeza katika kuainisha kwa undani zaidi malengo na mikakati ya utekelezaji katika Sekta ya Ardhi na Makazi.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ambayo ni kusimamia Sera ya Ardhi inayohusu utoaji, uhifadhi na utumiaji endelevu wa ardhi nchini, kusimamia Sera ya Uendelezaji Makazi ya Wananchi Mijini na Vijijini na kusimamia Upimaji wa Ardhi na Utayarishaji wa Ramani kwa Matumizi Mbalimbali. Majukumu mengine ni pamoja na kupima na kuhifadhi alama za mipaka kati ya nchi yetu na nchi tunazopakana nazo; kutafsiri mipaka ya maeneo mbalimbali ya kiutawala kama vile Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji ndani ya nchi yetu; kusimamia taaluma za Wizara na kuwaendeleza kitaaluma na kiutumishi Wafanyakazi wote wa Sekta ya Ardhi na Makazi.

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa mapato, katika mwaka wa fedha 2002/2003 Wizara ilikuwa na lengo la kukusanya jumla ya shilingi 4,902,523,000/= kutokana na ada mbalimbali za ardhi. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Mei, 2003 Wizara ilikuwa imekusanya shilingi 4,764,933,220.90 ambayo ni sawa na asilimia 97.19 na nina hakika kufikia mwisho wa mwaka wa fedha tutafikia lengo ambalo lilikuwa limewekwa. Kati ya makusanyo hayo shilingi 4,361,016,811.00 ni ada itokanayo na viwanja na mashamba ambayo ni asilimia 88.95 ya makusanyo hayo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003 Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 4,818,378,800/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 10,036,413,700/= kwa ajili ya miradi ya



maendeleo. Katika tengeo la fedha za kawaida shilingi 1,003,311,100.00 zilitengwa kwa ajili ya mishahara na shilingi 3,815,067,700.00 zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Juni, 2003 Wizara ilikuwa imepokea shilingi 4,396,339,240.36 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 10,036,413,700/= kwa ajili ya miradi ya maendeleo kutoka Hazina. Kazi zilizotekelezwa ni zile ambazo ambazo ziliaishwa katika hotuba ya mwaka jana ambazo ni upimaji wa viwanja 20,000 katika Jiji la Dar es salaam, uimarishaji, utunzaji na upatikanaji wa kumbukumbu za ardhi, kusimamia makusanyo ya ada za ardhi katika vituo 115 nchini, kusambaza na kutoa elimu ya Sheria ya Ardhi Na. 4 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na.5 za mwaka 1999, kuandaa Kanuni za Sheria ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi na Nyumba (*Land Disputes Courts Act of 2002*), kutoa huduma mbalimbali zinazohusu ardhi, kama ugawaji, uthamini, uandaaji wa hati miliki, uhakiki na usajili wa Hati, utatuzi wa migogoro ya ardhi na nyumba, upimaji na uwekaji wa alama za mipaka ya Vijiji, kuimarisha na kupima mipaka ya Kimataifa na kutayarisha ramani za msingi.

Pia kuratibu upembuzi yakinifu katika mpango wa kudhibiti Mto Songwe, kufanya na kusambaza utafiti wa vifaa vya ujenzi na utaalum wa nyumba bora na za gharama nafuu, kuweka mipango ya kuendeleza maeneo ya kati ya Manispaa za Mbeya, Tabora na Miji ya Sumbawanga na Kigoma, kuandaa na kutekeleza mipango ya kimkakati ya Miji (*Strategic Urban Development Plans*) kwa Miji ya Kibaha, Vwawa, Tunduma na Lushoto, kutoa mafunzo ya cheti na stashahada katika vyuo vya Ardhi Tabora na Morogoro, kutoa mafunzo kwa watumishi, marekebisho ya Sheria ya Mipangomiji sura Na. 378 (*Cap 378*), kuratibu shughuli za Shirika la Nyumba la Taifa, ujenzi wa jengo la kukusanyia ada za ardhi na Ofisi za Kitengo cha *Management Information System (MIS)*, kutoa elimu ya kupambana na Ukimwi kwa watumishi wa Wizara, kutayarisha mipango ya matumizi bora ya ardhi, kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha utawala bora ikiwa ni pamoja na kupambana na rushwa na kuanza kwa zoezi la kuweka kumbukumbu za ardhi katika kompyuta kwa Ofisi za Msajili wa Hati Moshi na Mwanza.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ambayo Wizara imeyapata katika mwaka wa fedha 2002/2003 ni pamoja na upimaji wa viwanja zaidi ya 20,000 katika Jiji la Dar es salaam, kuweka kumbukumbu za viwanja katika kompyuta, zoezi ambalo limesaidia Wizara kubaini wamiliki na walipa kodi za viwanja, baadhi ya Halmashauri zimeelewa umuhimu wa kutenga fedha kwa ajili ya kutayarisha Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi, ongezeko la ujenzi wa nyumba za kuuza na kupangisha unaofanywa na Shirika la Nyumba la Taifa, ongezeko la Usambazaji wa utaalum na matokeo ya utafiti wa vifaa vya ujenzi wa nyumba bora na za gharama nafuu na ongezeko la elimu ya Sheria za Ardhi kwa wananchi ngazi ya Wilaya na Vijiji.

Mheshimiwa Spika, matatizo yaliyoikabili Wizara katika kipindi hiki ni pamoja na ubovu wa majengo yenye mitambo ya kutengeneza ramani, ambayo yalijengwa tangu enzi ya mkoloni, unatishia mazingira na usalama wa watumishi na mitambo ndani ya majengo hayo, ukosefu wa fedha za kutosha kulipia fidia kwa mujibu wa sheria mpya za ardhi, upungufu wa ramani za msingi (*base maps*) katika baadhi ya maeneo nchini ili kuwezesha uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi na upimaji wa viwanja na mashamba, ukosefu wa utaratibu/mfumo wa kuwawezesha wananchi kupata mikopo ya kujenga nyumba za kuishi, baadhi ya Wapangaji kushindwa kununua nyumba walizokubaliwa kuuziwa na Shirika la Nyumba la Taifa, baadhi ya wapangaji wa Shirika kukaidi kulipa kodi ya pango ya nyumba na baadhi ya wamiliki wenye mashamba makubwa kukaidi kulipa kodi ya pango ya ardhi licha ya viwango vya ada kushushwa kutoka Sh. 600 kwa ekari hadi shilingi 200/=.

Mheshimiwa Spika, pia Mipaka kati ya nchi yetu na nchi jirani kutoeleweka kwa urahisi kutokana na alama kuharibika, kung'olewa au kuwa mbalimbali sana pamoja na juhudi za kutoa elimu juu ya Sheria mpya za Ardhi, wananchi wengi bado wana uelewa mdogo juu ya sheria hizi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2002/2003 Wizara iliweka mikakati itakayosaidia kutatua baadhi ya matatizo yaliyobainishwa hapo juu, mikakati hiyo ni pamoja na kuendeleza mazungumzo na Wizara ya Fedha kuona uwezekano wa Serikali kugharimia ujenzi wa jengo jipya la ramani katika mwaka wa fedha 2004/2005, kutafuta Wahisani mbalimbali ili kugharamia utayarishaji ramani za msingi kwa nchi nzima. Hii ni kwa sababu utayarishaji wa ramani za msingi unahitaji fedha nyingi, ambapo Serikali pekee haiwezi kutekeleza kazi hiyo, kuendeleza mazungumzo na Wizara ya Fedha

ili kuona uwezekano wa kutunisha Mfuko wa *Plot Development Revolving Fund* utakaowezesha Wizara na Halmashauri kutwaa ardhi na kupima viwanja kwa lengo la kupunguza uhaba wa viwanja Mijini, kuanzisha mfumo utakaowezesha wananchi kukopa fedha kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa nyumba na kurekebisha Sheria ya Shirika la Nyumba ili kuwabana wapangaji wakorofi wasiolipa kodi za pango.

Pia kutoa elimu kwa umma juu ya Sera na Sheria za Ardhi kwa kuzingatia mkakati uliokubaliwa na Wadau Morogoro Mei, 2003 ili kuwafikia wananchi wengi zaidi, kujenga mfumo wa Wizara ili kuunganisha mifumo iliyopo ya kila Idara kwa lengo la kurahisisha mawasiliano (*Ministry of Lands Information System – MOLIS*) na kujenga uwezo wa kutumia teknolojia ya *satelite* katika kutengeneza ramani.

Mheshimiwa Spika, mwelekeo wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2003/2004 unatoa kipaumbele kwa maeneo makuu matatu ambayo yanaweza kuwa kichocheo kikuu cha kuwaletea Watanzania maendeleo endelevu. Maeneo hayo ni Kwanza, kutekeleza mkakati wa kuwaondolea wananchi umasikini; pili, kuongeza ukusanyaji wa mapato ya Serikali na tatu, ni kudumisha amani kwa kushughulikia migogoro ya ardhi na nyumba nchini kwa wakati na kwa mujibu wa sheria. Katika kutekeleza vipaumbele hivi Wizara itaendeleza mikakati iliyojiwekea mwaka wa fedha 2002/2003.

Mheshimiwa Spika, Wizara imejiwekea lengo la kukusanya jumla ya shilingi 5,430,401,000/= kutokana na kodi na ada mbali mbali za ardhi. Aidha, nakusudia kuliomba Bunge lako Tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 600,000,000/= kwa ajili ya miradi ya maendeleo na jumla ya shilingi 5,413,928,900/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Maelezo ya kina kwa utekelezaji wa kazi mbalimbali umefafanuliwa kwa kila Idara na Taasisi chini ya Wizara kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003 Wizara iliendelea kutoa huduma za maendeleo ya ardhi kwa wananchi kwa mujibu wa sera na sheria zilizopo ili kuwawezesha kuondokana na umasikini. Huduma hizo ni pamoja na utwaji na ugawaji wa ardhi, usajili wa hati miliki pamoja na nyaraka mbalimbali, kutoa vibali vya uwekaji rehani hati za kumiliki ardhi na uhamisho wa miliki, uthamini wa mali, utatuzi wa migogoro ya ardhi na kutoa elimu kwa umma kuhusu Sera na Sheria mpya za ardhi. Aidha, Wizara iliendelea kuchapisha na kusambaza fomu za aina mbalimbali kwa ajili ya umilikishaji ardhi kwenye Halmashauri za Jiji, Manispaa, Miji na Wilaya. Wizara itaendelea kutoa huduma hizo katika mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2002/2003, Wizara ilikamilisha utwaji wa ardhi na ubatilisho wa miliki kwa mashamba 24 na viwanja 197 na kutoa vibali vya uhamisho na uwekaji rehani hati 538 za kumiliki ardhi. Utwaji wa ardhi huo ulihusisha maeneo ya Boko Dovya, Bunju, Buyuni, Kisota, Mbweni, Mivumoni, Mwanagati, Mtoni Kijichi, Tuangoma na Vijibweni ambayo yalitwaliwa kwa ajili ya upimaji viwanja 20,000 Jijini Dar es Salaam.

Aidha, katika kutekeleza Sheria mpya za Ardhi madaraka ya kugawa ardhi yamepelekwa kwenye Halmashauri. Ili kuziwezesha Halmashauri kutekeleza kazi hiyo, katika mwaka uliopita Wizara yangu imekamilisha uteuzi wa Kamati za Kugawa Ardhi kwa Halmashauri 102. Kamati hizo zimeanza kufanya kazi.

Kwa utaratibu huo, Wizara imebaki na jukumu la kushughulikia maombi ya viwanja kwa ajili ya Balozi mbalimbali, maeneo ya ufukweni, visiwa vidogo vidogo, maeneo ya ujenzi wa nyumba nyingi kwa pamoja (*Estates*) yanayozidi hekta tano, maeneo ya uwekezaji chini ya Kituo cha Uwekezaji (*TIC*) na maeneo ambayo matumizi yake ni ya manufaa kwa Taifa kama viwanja vya ndege na migodi. Natoa wito kwa Halmashauri ambazo hazijapendekeza majina ya Wajumbe wa Kamati hizo wafanye hivyo mara moja ili waweze kutekeleza jukumu la kugawa ardhi kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Halmashauri kupewa madaraka ya kugawa ardhi bado Wizara yangu ina jukumu la kusaini hati miliki na kuzisajili. Katika mwaka uliopita Wizara yangu ilisajili hati 3,505 pamoja na nyaraka zinazohusiana na hati miliki 8,191. Nyaraka nyingine zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Nyaraka ni 2,363 na rehani za mali zinazohamishika 567. Wizara pia ilishughulikia

uandaaji wa nyaraka za kisheria 29 kwa ajili ya kufanya mabadiliko kwenye daftari la msajili (*deed of rectification*) na kuhudhuria vikao 245 vya Mahakama mbalimbali hapa nchini.

Aidha, katika hotuba ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2001/2002 nilizungumzia uanzishaji wa huduma ya Usajili wa Hati za Kimila ngazi ya Wilaya na Kijiji. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa ujenzi wa masjala ya mfano unaendelea katika Kijiji cha Igamba Wilaya ya Mbozi. Pia maandalizi ya kujenga masjala ya mfano katika ngazi ya Wilaya huko Mbozi unaendelea. Aidha, kwa kushirikiana na Halmashauri zote nchini Wizara yangu itaendelea kutoa ushauri wa ujenzi wa masjala katika Wilaya nyingine.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2002/2003 Wizara yangu imekamilisha utojaji vibali vya uhamisho 544 na uwekaji rehani kwa hati 210 za kumiliki ardhi. Kutokana na madai ya Chama cha wenye Mabenki (*Bankers Association*) kwamba Sheria za Ardhi ni kikwazo katika kutoa mikopo kwa kuweka rehani za miliki za Ardhi, Wizara imekuwa na vikao vya majadiliano na Wawakilishi wa Chama hicho na wawekezaji binafsi ili kupata mapendekezo ya kuzifanyia marekebisho sheria hizo.

Aidha, mtaalamu mwelekezi aliyeteuliwa na Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba kushughulikia suala hilo amekwishatoa taarifa yake. Mapendekezo ya taarifa zote mbili yatazingatiwa wakati wa kupendekeza marekebisho ya Sheria hizo ambayo yanatarajiwa kuwasilishwa katika kikao cha Bunge cha Oktoba - Novemba, 2003.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Juni 2003, Wizara imethamini nyumba 364 ambazo zilitozwa ada ya uthamini kiasi cha shilingi 9,554,497.50. Aidha, Wizara ilipokea na kupitisha jumla ya taarifa za uthamini 1,781 kutoka Makampuni binafsi na kutoza ada ya uhakiki (*Approval fee*) kiasi cha shilingi 45,099,796.70. Pia ukadiriaji wa ada ya ardhi kwa matoleo mapya ya viwanja na mashamba 731 yenye thamani ya ada ya shilingi 33,680,338.00 ulishughulikiwa. Vile vile Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa imethamini nyumba ambazo zinatarajiwa kununuliwa na Balozi zetu huko Pretoria, Afrika ya Kusini, Kampala, Uganda na Khartoum, Sudan.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya mwaka wa fedha 2002/2003 niliahidi kwamba Wizara ingeanza kutatua migogoro ya ardhi na nyumba kwa kufuata mfumo mpya chini ya Sheria ya *The Land Disputes Courts Act* Na. 2 ya mwaka 2002. Kazi hiyo, imeendelea kufanyika chini ya mfumo uliokuwepo kwa sababu kanuni za sheria iliyotajwa zilikuwa hazijaandaliwa na matatizo mengine ambayo yalikuwa nje ya uwezo wa Wizara. Matatizo hayo ni ugumu wa upatikanaji wa ofisi katika Mikoa na Wilaya ambapo Wizara inalenga kuunda Mabaraza ya Ardhi na Nyumba na suala la ajira ya watumishi katika Mabaraza hayo.

Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba Kanuni za sheria Namba 2 ya mwaka 2002 zimekamilika na Sheria mpya itaanza kutumika mwezi Oktoba 2003. Napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru viongozi wote wa Mikoa na Wilaya ambao wametambua umuhimu wa kuundwa kwa chombo hiki kwa kuhakikisha kwamba ofisi na majengo zinapatikana. Kwa kuwa Ofisi na majengo yaliyopatikana yanahitaji kufanyiwa ukarabati, Wizara katika mwaka wa fedha 2002/2003 ilifanya maandalizi ya kukarabati majengo katika Mikoa ya Mbeya, Dodoma na Morogoro. Kazi hiyo itaendelea kwa Mikoa mingine katika mwaka wa fedha 2003/2004. Kuhusu suala la ajira Wizara inaendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais, Idara Kuu ya Utumishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mabaraza ya Ardhi na Mabaraza ya Nyumba yaliyopo yameendelea kuwahudumia wananchi. Jumla ya migogoro ya ardhi 316 na 689 ya nyumba imeamuliwa. Vilevile rufaa 47 za migogoro ya ardhi na 52 za nyumba zimesikilizwa na kutolewa uamuzi katika mwaka wa fedha 2002/2003.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Kituo cha Uwekezaji (*TIC*) imeazimia kuanzisha Hazina ya Ardhi yaani *Land Bank* ili kuhamasisha uwekezaji nchini. Utafiti umefanywa nchi nzima ili kuainisha maeneo yanayofaa kwa uwekezaji. Mpaka sasa zaidi ya ekari milioni nne zimeainishwa. Vikosi vya wataalamu wa Wizara wakishirikiana na Wizara za Maliasili na Utalii, Kilimo na

Chakula, Maji na Mifugo, TAMISEMI, Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafishaji vinafanya uhakiki ili kubaini hali halisi ya maeneo hayo tayari kupimwa na kukabidhiwa TIC ili yaingizwe kwenye Hazina ya Ardhi (*Land Bank*).

Mheshimiwa Spika, Wizara katika mwaka wa fedha 2002/2003 iliendelea na programu ya kutoa elimu kwa umma juu ya Sheria za Ardhi za mwaka 1999 na kanuni zake kwa njia ya redio, *television* na makala katika magazeti mbalimbali pamoja na semina. Kwa kushirikiana na TAMISEMI na Mashirika yasiyo ya Kiserikali, elimu hii ilitolewa kwa Maofisa Watendaji Kata na Wenyeviti wa Serikali za Vijiji katika Mikoa ya Mwanza, Kagera, Tanga, Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Mara, Mtwara, Morogoro, Mbeya, Shinyanga, Iringa na Dodoma. Sambamba na zoezi hilo vitabu vya Sheria ya Ardhi ya Vijiji nakala 3,464 na kanuni zake nakala 2,681 pamoja na Kitabu cha Mwongozo wa kutoa elimu ya Sheria ya Ardhi ya Vijiji nakala 7,876 vilisambazwa. Kazi hiyo itaendelea katika mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, Sheria Mpya za Ardhi zinamgusa kila mwananchi, hivyo si rahisi kwa Wizara peke yake kuwaelimisha wananchi kuhusu sheria hizo. Kwa sababu hiyo, mwezi Mei, 2003 Wizara iliandaa warsha ya Wadau kujadili Mkakati wa Kitaifa wa kutoa Elimu ya Sheria za Ardhi kwa Umma ili kuhakikisha kuwa Watendaji katika ngazi zote na Wadau wanazielewa vizuri sheria hizo. Baada ya kukaa na wadau hao hususan NGOs, Vyombo vya Habari, vikundi vya kijamii, Taasisi za Dini na Wizara nyingine, ulitayarishwa mkakati unaoelezea ni namna gani kila mmoja wao anaweza kushiriki katika kazi hii. Mkakati huo utaanza kutekelezwa rasmi katika mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia imeshiriki katika Maonyesho ya Sabasaba. Wizara imetumia fursa ya maonyesho hayo kuwaeleza wananchi juu ya taratibu mbalimbali zinazotakiwa kufuatwa katika kutoa huduma mbalimbali za Sekta ya Ardhi kwa kutumia vipeperushi, mabango na picha za video. Kwa kuendeleza elimu hiyo, Waheshimiwa Wabunge wamepata kabrasha lenye vipeperushi ambavyo nina imani vitawasaidia pamoja na wapiga kura wao wanapohitaji huduma zinazotolewa na Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, uimarishaji na upatikanaji wa kumbukumbu kwa wakati ni moja ya azma ambayo Wizara imeamua kutekeleza. Wizara inaendelea na kazi ya kuimarisha mfumo wa utunzaji wa kumbukumbu za ardhi kwa kutumia kompyuta.

Mheshimiwa Spika, zoezi la kutambua wamiliki wa viwanja na upanuzi wa wigo wa zoezi hilo hadi Ofisi za Msajili wa Hati Moshi na Mwanza lilifanyika katika mwaka wa fedha 2002/2003. Hadi kufikia mwezi Juni, 2003 jumla ya wamiliki wa viwanja 45,000 kwa Mkoa wa Dar es Salaam, 16,900 Ofisi ya Msajili wa Hati Mwanza na 15,200 katika Ofisi ya Msajili wa Hati Moshi walitambuliwa.

Sambamba na utambuzi huo, jumla ya hati 36,500 za viwanja vilivyopimwa katika Mkoa wa Dar es Salaam zilitambuliwa na nyaraka za majalada 152,000 zilipigwa picha na kuhifadhiwa kwenye kompyuta. Aidha, ujenzi wa jengo la Idara inayoshughulikia uwekaji wa kumbukumbu umeanza na hadi mwezi Juni, 2003 lilikuwa limekamilika kwa asilimia 25.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha mbinu za ukusanyaji mapato yatokanayo na kodi ya pango la ardhi, Wizara imejenga mfumo (*Land Rent Management Programme*) ambao utawezesha kuweka kumbukumbu za walipa kodi ya ardhi, kufuatilia mwenendo wa ulipaji kodi na wa kutoa ilani kwa walipa kodi. Makadirio ya mahesabu ya ada yatarahisishwa na kutolewa kwa wakati. Mfumo huu unatumika Wizarani kwa majaribio na baadae utatumika kwenye vituo vingine vya makusanyo.

Mpaka mwezi Juni 2003 jumla ya walipa kodi wa viwanja na mashamba 15,600 katika Mkoa wa Dar es Salaam wameingizwa kwenye kompyuta. Katika mwaka wa fedha 2003/2004 Wizara itaendelea kuimarisha mfumo ya kila Idara na kuiunganisha kwa lengo la kuwa na mfumo wa Wizara nzima (*Ministry of Lands Information System-MOLIS*) ambao utarahisisha utendaji kazi na maamuzi.

Mheshimiwa Spika, tangu teknolojia ya kisasa ianze kutumika katika Wizara, tumeweza kuzalisha ramani na kutoa huduma kwa wananchi kwa kiwango kikubwa. Kiwango cha utendaji kazi ni cha juu ukilinganisha na miaka ya nyuma ambapo upimaji ardhi ulikuwa unafanyika kwa kutumia nyenzo duni. Matumizi ya teknolojia mpya yamewezesha kupima kwa ufanisi, viwanja 20,000 katika Jiji la Dar es

Salaam, upimaji wa mipaka ya Vijiji, upimaji wa mipaka ya Kimataifa na upimaji wa mashamba Wilayani Mbozi.

Aidha, Wizara itaendelea na utekelezaji wa mpango wa Kitaifa wa kutayarisha ramani za msingi za Miji. Pamoja na kazi zilizoainishwa hapo juu upimaji wa viwanja, mashamba na Vijiji uliendelea kutekelezwa katika maeneo mbalimballi nchini.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili napenda nisisitize jambo moja, nalo ni kuhusu mradi wa kupima viwanja 20,000 katika Jiji la Dar es Salaam. Miji yetu mingi ina matatizo ya upatikanaji viwanja na ina makazi mengi ambayo hayapangwi vizuri. Mradi wa viwanja 20,000 katika Jiji la Dar es Salaam kama ilivyoelezwa kwa undani zaidi katika aya za 20 hadi 31 katika hotuba yangu ni jitihada za kujaribu kutatua tatizo hilo katika Manispaa zote tatu za Jiji la Dar es Salaam.

Wizara yangu inashirikiana kwa karibu sana na Mkoa, Jiji na Manispaa zote tatu. Matatizo yote yanayojitokeza tunayapatia ufumbuzi ndani ya Vikao vyetu vya mashauriano. Tukifanikiwa Dar es Salaam tutaendelea zoezi hili katika Miji mingine nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yamekuwepo malalamiko mengi kuhusu upatikanaji wa viwanja vilivyopimwa hasa katika maeneo ya miji. Hali hii imekuwa kero kubwa kwa wananchi. Ili kupunguza kero hii, Wizara ilibuni mradi wa kupima viwanja vingi. Kazi hii itafanyika kwa awamu na kwa kuanzia, viwanja zaidi ya 20,000 vimepimwa katika jiji la Dar es Salaam. Viwanja hivyo vimepimwa katika maeneo ya Tuangoma, Kisota na Mtoni Kijichi katika Manispaa ya Temeke, Buyuni Manispaa ya Ilala na Mbweni Mpiji, Mbweni JKT na Bunju, Manispaa ya Kinondoni. Ulipaji fidia na upimaji unaendelea katika maeneo ya Vijibweni, Mivumoni na Mwanagati.

Aidha, uchongaji wa barabara katika maeneo ya mradi yaliyopimwa unaendelea. Katika utekelezaji wa mradi huu, Wizara ilibuni michoro 45 ya mipango miji. Uthamini wa mali katika maeneo yote umebaini kuwa zinahitajika shilingi 10,868,175,700.00 kulipa fidia shilingi 6,286,757,600.00 zimelipwa na bakaa italipwa mwaka wa fedha 2003/2004.

Hadi sasa jumla ya viwanja 21,883 vimepimwa, viwanja vilivyogawiwa 16,747 vilivyolipiwa 3,674, viwanja vilivyotengenezewa hati 2825 na kiasi cha fedha kilichopatikana ni shilingi 4,283,000,000.00. Kasi ya ulipaji wa viwanja ilikuwa ndogo katika siku za mwanzo kutokana na wananchi kusubiri kukamilika kwa upimaji wa maeneo wanayoyapenda kwenye mradi. Ugawaji wa viwanja umefanywa na Manispaa na umilikishwaji unasimamiwa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa viwanja 20,000 utaleta mafanikio yafuatayo:-

Kuzuia kupanuka kwa ujenzi holela katika maeneo yasiyopimwa na hivyo kuwa na mpangilio bora wa makazi na itaongeza idadi ya nyumba na huduma za jamii Dar es Salaam, kuongeza mapato ya Serikali, kuondoa kero ya wananchi/Taasisi wanaotafuta viwanja, kupunguza msongamano wa watu na huduma mbalimbali katika maeneo ya katikati ya Jiji la Dar es Salaam, kuondoa mwanya wa rushwa katika uthamini na ugawaji wa viwanja, wananchi/Taasisi waliopatiwa viwanja wamepatiwa hati ambazo wanaweza kuzitumia kupata mikopo kuendesha shughuli za kiuchumi na hivyo kujikwamua na umaskini, kutoa mafunzo kwa vitendo kuhusu sheria mpya ya ardhi kwa wathamini, wapima ardhi, maafisa wa mipango miji na maafisa ardhi, kununua vifaa vya kisasa vya utendaji kazi, kubuni na kutumia mfumo wa kutoa barua za toleo na hati katika muda mfupi kwa kompyuta, kubuni mfumo wa kuweka takwimu *(data)* za uthamini unaodhibiti udanganyifu katika taarifa za uthamini, kutoa kazi kwa wakandarasi wadogowadogo katika ujenzi wa barabara, uthamini mali na upimaji ardhi na kutoa ajira kwa vijana waliofanya vibarua na mamalisha waliotoa huduma za chakula.

Mheshimiwa Spika, pia utekelezaji wa mradi wa viwanja utaleta mafanikio ya soko la vifaa vya ujenzi litapanuka kufuatia uendelezaji wa viwanja, mradi utaongeza ajira na mapato katika Sekta ya Ujenzi na mradi umetoa nafasi ya kuimarisha mshikamano kati ya viongozi na wataalamu wa Wizara, Mikoa na Halmashauri hivyo kupunguza udanganyifu na urasimu katika masuala ya viwanja.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna viwanja vingi katika Manispaa zote za Jiji la Dar es Salaam na ugawaji wa viwanja hivyo unafanyika kwa uwazi na uhakika. Kwa ujumla mradi huu umeimarisha utawala bora na umeongeza imani ya wananchi kwa Serikali yao. Hivyo natoa wito kwa wananchi kuendelea kutoa ushirikiano wao na kuacha tabia ya kutaka huduma za ardhi nje ya taratibu zilizowekwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2002/03 kazi ya upimaji wa mipaka ya vijiji iliendelea katika mikoa ya Singida, Ruvuma na Mbeya. Katika Mkoa wa Singida jumla ya vijiji 347 vilipimwa katika Wilaya ya Iramba 120, Wilaya ya Manyoni 143 na Singida vijijini 84.

Katika Mkoa wa Ruvuma jumla ya vijiji 366 vilipimwa katika Wilaya ya Tunduru 85, Wilaya ya Songea vijijini 72, Wilaya ya Namtumbo 54 na Wilaya ya Mbinga 155.

Aidha, katika Mkoa wa Mbeya upimaji wa vijiji 171 Wilaya ya Mbozi ulikamilika. Upimaji wa mashamba 11,000 ya Wananchi katika vijiji 6 pia umekamilika. Katika mwaka wa fedha 2003/2004 kazi ya kupima mipaka ya Vijiji itaendelea katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na kupima mashamba katika Vijiji vingine vya Wilaya ya Mbozi kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Serikali za Tanzania na Malawi zimemteua Mtaalamu Mwelekezi (*Consultant*) wa kufanya Upembuzi yakinifu juu ya kudhibiti Mto Songwe. Mtaalam Mwelekezi anatarajia kukamilisha kazi hii Desemba, 2003. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, iliwasiliana na serikali ya Uganda na kufikia muafaka wa upimaji wa mpaka kati yetu. Wizara imepeleka wataalam kwenda kuendelea na upimaji wa mpaka huo. Aidha, wataalam wa Tanzania na Kenya walifanya ukaguzi wa mpaka wote kati ya Tanzania na Kenya na kukubaliana kupima kilomita 20 za mpaka magharibi mwa Ziwa Natron, kupima mpaka katika eneo la Ziwa Jipe na Mto Ruvu/Pangani na kukarabati alama za mpaka zilizoharibiwa, kurejesha alama za mpaka zilizoondolewa na kuongeza alama zaidi ili kurahisisha utambuzi wa mpaka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003 sehemu ya mpaka katika eneo la Ziwa Jipe na Mto Ruvu/Pangani imepimwa. Kila nchi inaendelea na kazi ya uchoraji ramani kutokana na upimaji katika eneo la Ziwa Jipe. Makubaliano mbalimbali yaliyofikiwa hadi sasa kati ya Tanzania na nchi za Malawi, Uganda na Kenya yataendelea kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, chini ya mpango wa kitaifa wa utayarishaji wa ramani za msingi za miji, uliobuniwa na wizara yangu mwaka 1999/2000, uchoraji na uhakiki wa ramani za miji 10 katika kanda ya Kusini umekamilika. Zaidi ya ramani 600 zimetayarishwa na ziko tayari kwa matumizi ya kupanga miji na matumizi mengine ya ardhi. Mkandarasi wa kupiga picha miji 38 katika Kanda ya Ziwa Victoria, inayojumuisha Mikoa ya Mara, Mwanza, Kagera na Shinyanga, ameteuliwa na kazi itaanza mwezi wa Julai 2003. Utayarishaji wa ramani za maeneo hayo utanza Mwezi Septemba 2003. Aidha, matumizi ya picha za *satellite*, kutayarisha na kuhuisha ramani mbalimbali, itafanyika kulingana na uwezo wa kifedha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majukumu mengine niliyoyazungumzia awali, Wizara ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi. Wizara imekuwa inachambua Sera hii na kuchukua hatua mbalimbali za utekelezaji. Tanzania ni moja ya nchi zinazokabiliwa na ukuaji wa kasi wa miji yake. Katika kipindi cha kuanzia miaka ya 1980 hadi sasa, ukuaji wa miji umekuwa ukiongezeka kwa kiasi cha wastani wa asilimia 10 kwa mwaka. Ili kuweza kukabili na kudhibiti hali hii, inabidi miji ipangwe kwa kuzingatia rasilimali zilizopo na kuhakikisha mazingira ya Miji yanalindwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na mamlaka za Halmashauri imekuwa ikiandaa mipango ya kimkakati ya uendelezaji wa miji. Mkazo mkubwa umeelekezwa katika kuandaa mipango ya Miji midogo na Miji ya Makao Makuu ya Wilaya yenye ukuaji wa kasi. Mipango hii chini ya dhana mpya ya ushirikishwaji, hushirikisha wadau mbalimbali katika upangaji na utekelezaji wake.

Aidha, mipango hii huandaliwa tu pale ambapo Halmashauri husika huonyesha uhitaji wake kwa kutenga fedha za maandalizi na utekelezaji. Wizara itaendelea kushiriki na kutoa ushauri wa kitaalamu

katika upangaji na utekelezaji wake ili hatimaye tuweze kuwa na miji endelevu yenye kujitosheleza kijamii, kiuchumi na kiutamaduni.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002 katika Bunge lako Tukufu niliahidi kuwa mipango ya kimkakati ya miji ya Karatu, Shinyanga na Makambako itawasilishwa kwenye Halmashauri husika kwa ajili ya kujadiliwa na kutolewa maoni na wadau. Ninalijulisha Bunge lako Tukufu kuwa mipango ya miji hiyo imekamilika.

Aidha, maandalizi ya mipango ya miji ya Songea na Kibaha nayo yamekamilishwa. Katika mwaka huu wa fedha Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri husika itakamilisha maandalizi ya mipango ya kimkakati ya miji ya Vwawa na Tunduma na pia itaendelea na maandalizi ya mipango ya miji ya Lushoto na Masasi.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya kati ya Miji mingi hapa nchini yanahitaji kuendelezwa upya kwa vile miundombinu iliyopo imechakaa, haitoshelezi na pia haifanyi kazi kama inavyotarajiwa kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu na shughuli zao. Wizara imekuwa ikijishughulisha katika maandalizi ya Mipango ya maeneo ya kati kwa kushirikiana na Halmashauri husika. Mipango hii inalenga katika kuboresha mazingira ya vitovu vya miji ili viweze kuvutia wawekezaji pamoja na wakazi wa miji hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2002/2003, Wizara ilikamilisha mipango ya uendelezaji upya wa maeneo ya kati ya miji ya Morogoro, Mtwara na Iringa na itatangazwa kwenye gazeti la Serikali. Aidha, rasimu za mipango ya kuendeleza upya maeneo ya kati ya Manispaa za Mbeya na Tabora zinatarajiwa kuwasilishwa kwenye Halmashauri za Manispaa hizo kwa ajili ya kupata maoni ya mwisho kabla hazijaidhinishwa na kutangazwa rasmi. Wizara pia kwa kushirikiana na Halmashauri za miji ya Sumbawanga na Kigoma ilianza kuandaa mipango ya kuendeleza upya maeneo ya kati ya Miji hiyo na kazi hiyo itaendelea katika mwaka huu wa fedha 2003/2004. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nia ya Wizara ni kuhakikisha kuwa maeneo ya Miji yaliyotangazwa kuendelezwa upya (*Redevelopment areas*) yanaandaliwa mipango ya uendelezaji upya mapema. Napenda kurudia wito wangu kwa Halmashauri za Miji ambazo hazijawasilisha ramani za mipaka ya maeneo chakavu yanayohitaji kuendelezwa upya, kukamilisha kazi hiyo mapema, ili ziweze kuwekwa katika mipango ya Wizara. Aidha, Wizara itaendelea na ukusanyaji wa takwimu za viwango vya upangaji (*Planning Standards*) vya maeneo mbalimbali kwa nia ya kuboresha viwango vilivyopo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2002/2003, Wizara ilipokea michoro 194 kutoka katika Halmashauri mbalimbali hapa nchini kwa ajili ya kuidhinishwa. Kati ya michoro hiyo, michoro 120 yenye jumla ya viwanja 49,527 vya matumizi mbalimbali imeidhinishwa na kurejeshwa katika miji husika tayari kwa kuendelezwa. Michoro ambayo haikuidhinishwa imerejeshwa kwa ajili ya marekebisho.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililiarifu Bunge lako kwamba, Wizara itaanza kuelekeza nguvu zake katika kuhuisha sheria ya Mipango Miji na Vijiji (Sura 378) baada ya kukamilika kwa Sera ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000.

Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Mtaalamu Mwelekezi aliteuliwa amekwisha wasilisha mapendekezo yake ya awali. Aidha, Wizara iliandaa mkutano wa kitaifa (*National Stakeholders' Consultative Workshop*) wa Wadau kuzungumzia suala hili pamoja na mapendekezo ya Mtalaamu mwelekezi. Wakati huo huo Wizara, kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani ilimwajiri Mtalaamu Mwelekezi kuchambua mapungufu ya Sheria hiyo kuhusu upangaji wa matumizi bora ya ardhi Vijijini. Mapendekezo yaliyotolewa na Mtaalamu huyo na yale yaliyotokana na mkutano wa Wadau nilioutaja hapo juu yataunganishwa na kuzingatiwa katika zoezi la kurekebisha au kutunga sheria mpya ya Mipango ya Ardhi Mijini na Vijijini.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu litakubaliana na mimi kwamba hivi sasa nchi yetu inashuhudia mabadiliko mbalimbali katika sera za uwekezaji, uchumi na teknolojia mpya ili kuendana na mfumo wa kimazingira na kibiashara. Hali hii imesababisha kuwepo kwa ongezeko la wananchi kupenda

kubadilisha matumizi ya ardhi. Uchunguzi uliofanywa na Wizara umebaini kuwa mabadiliko ya matumizi ya ardhi yaliyo mengi hufanyika kiholela katika Mamlaka za Halmashauri bila kufuata Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo iliyopo. Hali hii wakati mwingine imekuwa ikisababisha uharibifu wa mazingira na kuleta kero kwa jamii. Wizara inaendelea kuzikumbusha Mamlaka za Halmashauri nchini kuzingatia taratibu za kisheria katika hatua zote za kushughulikia maombi ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Shirika la Umoja wa Mataifa la Makazi (*UN-HABITAT*), ilimtumia Mtaalamu Mwelekezi kubuni na kupendekeza mfumo wa kutoa mikopo kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa nyumba hapa nchini. Taarifa hiyo ilijadiliwa kwenye kikao cha wadau mwezi Desemba 2002 na baada ya kuboreshwa, imewasilishwa kwenye ngazi za juu za serikali kwa ajili ya kupata idhini ya utekelezaji. Nina imani kuwa mpango huu utakapokamilika wananchi wengi watanufaika na mikopo hii na hali ya makazi itapata sura mpya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha 2003/2004 Wizara itakamilisha maandalizi ya Kanuni za ujenzi wa nyumba (*Building Regulations*) na itaanza maandalizi ya Sheria ya Nyumba, ambayo pamoja na Sheria ya Mipangomiji na Vijiji ndizo nguzo kwa utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2002/2003, Bodi ya Mfuko wa Mikopo ya nyumba kwa watumishi wa Serikali iliidhinisha mikopo mipya 31 ya kiasi cha shilingi 114,758,000.00. Idadi hiyo inafanya watumishi wa Serikali waliopewa mikopo ya nyumba tangu Mfuko uanze mwaka 1992 kufikia 417 ambao ni sawa na asilimia 29.2 ya watumishi wote 1,427 walioomba kupewa mikopo ya nyumba hadi mwezi Mei, 2003.

Kati ya waliopewa mikopo, wanawake ni 144 sawa na asilimia 34.5. Juhudi kubwa inafanywa kukusanya marejesho ya mikopo ili Mfuko uweze kupata fedha za kukopesha watumishi wengine. Hadi kufikia mwezi Mei, 2003 marejesho halisi yalikuwa yamefikia shilingi 209,531,933.10 ambayo ni sawa na asilimia 102 ya marejesho tarajiwa ya shilingi 205,518,670.60. Hata hivyo, kufikia muda huo kulikuwa na maombi 1,010 ambayo yalikuwa hayajashughulikiwa kutokana na ukosefu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi na wadau wengine ina mikakati ya kujenga uwezo kwa Halmashauri za wilaya na Vijiji ili ziweze kuandaa na kutekeleza mipango ya matumizi bora ya ardhi. Katika mwaka wa fedha 2002/2003 Tume imekamilisha kusambaza Kiongozi cha Mwanakijiji cha mipango ya matumizi bora ya ardhi katika Vijiji vyote nchini. Tume katika mwaka wa fedha 2002/2003 imeanza kuandaa mwongozo wa Wilaya. Kazi hiyo inatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003 Wizara imejenga uwezo wa Timu za Wilaya za Kupanga matumizi bora ya ardhi katika Wilaya za Morogoro Vijijini (Mvomero) Ileje, Songea Vijijini (Namtumbo), Sikonge, Kilombero, Musoma Vijijini, Urambo, Nzega, Mpanda, Mkuranga na Mafia. Katika mwaka wa fedha 2003/2004 Tume ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi itaendelea kuisitiza na kuwaelekeza wananchi kuhusu umuhimu wa nafasi ya mipango ya matumizi bora ya ardhi katika kuondoa umaskini Vijijini.

Mheshimiwa Spika, kazi zitakazofanyika ni pamoja na kujenga uwezo wa Halmashauri za Wilaya na Vijiji katika utayarishaji na usimamizi wa mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa kutoa mafunzo kwa timu 10 za Wilaya na Halmashauri za Vijiji 10, kutoa msaada wa ushauri wa kitaalamu (*Technical Backstopping*) kwa timu za Wilaya zilizokwisha anza kutekeleza programu ya *Participatory Land Use Management (PLUM)* ambazo ni Ileje, Namtumbo, Mvomero, Musoma Vijijini, Kilombero, Mafia, Sikonge, Urambo na Mkuranga na kukamilisha miongozo ya utayarishaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya wilaya na pia kutoa mafunzo na ushauri wa kitaalamu kwa Halmashauri za Wilaya katika kuandaa mipango hiyo katika Wilaya kumi na moja ambazo ni Ileje, Kilombero, Morogoro Vijijini (Mvomero), Songea Vijijini (Namtumbo), Musoma Vijijini, Mafia, Nzega, Mpanda, Sikonge, Urambo na Mkuranga.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya msingi ya Shirika la Nyumba la Taifa kama yalivyoainishwa katika Sheria Na. 2 ya mwaka 1990 iliyoliunda upya Shirika ni kama ifuatavyo:-



Mheshimiwa Spika, kwanza ni kutoa huduma za usimamizi wa miliki, kujenga nyumba au majengo ya aina mbali mbali ya kuishi au ofisi kwa madhumuni ya kupangisha na kuuza kwa watu binafsi na taasisi za umma, kutekeleza kama wakala, miradi ya ujenzi wa nyumba itakayokuwa imeidhinishwa na Serikali na kuchukua na kutekeleza kandarasi za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, majukumu haya mawili ya mwisho yanalitambulisha Shirika kama chombo halali cha kufanya kazi za ujenzi wa majengo kama Mkandarasi. Kwa tafsiri hiyo, Shirika lina jukumu la kutafuta, kuomba kushindana na kufanya kazi za ujenzi wa nyumba na majengo ya kibiashara. Ili kutekeleza kwa ufanisi majukumu yote hayo niliyoyataja, nilitoa wito kwa Bodi Mpya ya Wakurugenzi ya Shirika niliyozindua rasmi tarehe 21 Machi, 2003 kuzingatia na kuweka uzito maalum katika masuala yafuatayo:-

Kwanza, kuongeza mapato na mtaji wa Shirika, pili, kuongeza juhudi katika ukusanyaji kodi ya pango, tatu, kukamilisha zoezi la uuzaji wa nyumba ndogo ndogo na za kati ifikapo tarehe 30 Juni, 2003, nne, kuendeleza zoezi la ukarabati wa nyumba, tano, ujenzi wa nyumba za kuuza na sita, kupiga vita rushwa.

Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu kuwa kodi ya pango ya nyumba ndiyo chanzo kikuu cha mapato ya kuendeshea shughuli za Shirika. Ingawa viwango vya kodi ya pango la nyumba ni vya chini, kulinganisha na viwango vya Soko, bado baadhi ya wapangaji hawalipi. Hadi kufikia mwezi Machi, 2003 malimbikizo ya kodi yalifikia shilingi 11,300,088,000.00 katika maeneo mbalimbali nchini licha ya juhudi zilizokwihafanywa na Shirika kuhakikisha malimbikizo hayo yanakusanywa. Hali hiyo imesababisha Shirika kushindwa kujenga nyumba nyingine.

Ningependa kuwakumbusha wapangaji wa Shirika wajibu wao wa kulipa kodi ya pango. Nyumba walizobahatika kupanga ni za Watanzania wote. Kila Mtanzania ana haki ya kupanga nyumba hizo. Hivyo waheshimu wajibu wao wa kulipa kodi ya pango na wale ambao hawataki kulipa kodi hiyo wawapishe wananchi wengine. Baada ya kuanza kutekeleza Sheria Mpya ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi na Nyumba (*The Land Disputes Courts Act* Na. 2 ya Mwaka 2002), kama nilivyokwisha tangaza hapo awali, natumaini Shirika litakuwa na uwezo wakuwabana kisheria wanaokwepa kulipa kodi ya pango la nyumba. Endapo sheria hiyo haitatosheleza, hatuta sita kuleta mapendekezo zaidi ya kurekebisha sheria ya Shirika ili kukidhi azma ya kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, Shirika bado linaendelea na mpango wake wa kuuza nyumba ndogo ndogo na za kati kwa wapangaji. Zoezi hili lilianza mwaka 1993 na kufikia mwezi Juni, 2003 jumla ya nyumba 5,004 zilitarajiwa kuuzwa kwa lengo la kuingiza mapato ya shilingi 5,890,042,249.25. Jumla ya nyumba 2,907 zimelipiwa kikamilifu na kulipatia Shirika mapato ya shilingi 3,948,235,445.35. Nyumba 869 zimeshaanza kulipiwa na nyumba 1,228 bado hazijaanza kulipiwa. Wale ambao wameshaanza kulipia wahakikishe wanakamilisha malipo ifikapo mwezi Desemba 2003. Wale ambao, kwa sababu mbali mbali hawajaanza kulipia nyumba hizo, wanashauriwa kuanza kulipia mara moja, na ifikapo Novemba 1, 2003, hatua za kisheria zitaanza kuchukuliwa kwa mpangaji mmoja mmoja anayehusika.

Mheshimiwa Spika, Shirika limefanya juhudi kubwa kuziweka rasilimali (nyumba) katika hali nzuri kulingana na mahitaji ya matengenezo ya kila mwaka. Katika kipindi cha 2002/2003. Hadi mwezi Mei, 2003 Shirika limefanya matengenezo ya nyumba 3,764 kati ya nyumba 17,700 kwa gharama ya shilingi 2,745,033,228.00. Ongezeko la kodi lililoanza kutumika mwezi Novemba 2001 ndilo limelipa Shirika uwezo zaidi wa kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya nyumba ni makubwa sana katika miji yetu. Shirika linaendelea kutoa mchango wake kwa kujenga nyumba na kuziuzwa kwa wateja wanaohitaji hasa wafanyakazi. Katika kipindi cha mwaka 2002/2003 Shirika liliendelea kujenga nyumba 254 katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha na Mwanza. Kati ya nyumba hizo, ujenzi wa nyumba 43 Boko, nyumba 1 *Regent Estate*, nyumba 6 *Mbezi Beach* Jijini Dar es Salaam na nyumba 1 Kijenge Arusha umekamilika. Katika mradi wa Boko kazi zifuatazo zimekamilika; barabara awamu ya kwanza, uvutaji wa maji, ujenzi wa madarasa manne ya shule ya sekondari, daraja la kuvuka mto kwenda kwenye eneo la mradi na malipo ya fidia.

Katika mwaka wa fedha 2003/2004 Shirika litaendelea na ujenzi wa nyumba 216 za kuuza katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza na Arusha, ujenzi wa majengo 13 ya vitega uchumi, ambapo majengo 11 makubwa yatajengwa kwa njia ya ubia na mawili yatajengwa na Shirika lenyewe. Shirika limeanzisha tovuti [www.nhctz.com](http://www.nhctz.com) pamoja na vipeperushi vya aina mbalimbali ili kuwawezesha wateja kuchagua nyumba wanazohitaji.

Mheshimiwa Spika, sitachoka kuzungumzia suala la vita dhidi ya rushwa kwa upande wa Shirika la Nyumba la Taifa. Shirika bado linalalamikiwa kwa kuwepo rushwa hasa katika maeneo yafuatayo; utafutaji na upangishaji wa nyumba tupu, zabuni katika matengenezo ya nyumba, vibali vya ujenzi wa nyongeza na ufuatiliaji wa kesi mahakamani. Ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hivi sasa Taasisi ya Kuzuia Rushwa inafanya utafiti juu ya rushwa ndani ya Shirika kwa lengo la kutoa ushauri jinsi ya kuziba mianya ya rushwa. Katika suala hili nimeliagiza Shirika lihakikishe kwamba Taasisi hiyo inapewa ushirikiano ili zoezi hili lifanikiwe.

Mheshimiwa Spika, jukumu kuu la Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi ni kutafiti, kukuza, kushauri, kuhamasisha na kusambaza matokeo ya utafiti na utaalum wa ujenzi wa nyumba bora za gharama nafuu. Nia ni kuinua na kuboresha viwango vya nyumba hivyo kuongeza ubora wa maisha ya wananchi Vijijini na Mijini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2002/2003 Wakala ilifanya semina za uhamasishaji kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii ngazi ya Wilaya na Kata, Maafisa Mipango Miji na Maafisa Ardhi wa Wilaya na Madiwani. Wilaya zilizohusika ni Bagamoyo, Iringa Mjini na Kongwa, jumla ya waliohudhuria ni 116. Madhumuni yalikuwa wakishahamasika waanzishe vikundi vya ujenzi kwenye maeneo yao.

Aidha, ushauri na mafunzo ya nadharia na vitendo (*Demonstrations*) yalifanyika kwa vikundi, Taasisi, CBOs na NGOs katika Wilaya za Dodoma, Singida Vijijini, Karagwe, Tarime, Hanang, Kinondoni, Ilala, Mafia na Kahama. Uhamasishaji huu ulihusisha vijiji 24, vikundi 25. Jumla ya watu waliohamasishwa ni 208.

Nashauri vikundi hivi vipewe kipaumbele katika kandarasi za kujenga majengo ya umma kama vile Shule, Vituo vya Afya na Zahanati ambao utakuwa unaendelea katika maeneo yao. Pia Wakala ilitengeneza na kuuza mashine 24 za kutengeneza matofali yanayofungamana (*inter-locking bricks*), mashine 3 za kutengeneza vigea na kalibu za vigea (*moulds*) 300.

Mheshimiwa Spika, ili kupanua wigo wa kujulikana, Wakala ilifanya maonyesho ya tafiti zake kwenye mkutano wa mwaka wa Wizara ya Elimu na Utamaduni uliofanyika Arusha. Aidha, Wakala uliendelea kujitangaza kupitia Vyombo vya Habari vya televisheni, magazeti, kuchapisha na kusambaza vijarida vya Kituo na Kadi za Biashara (*Business Cards & Brochures*). Katika mwaka wa fedha 2003/2004, Wakala utajizatiti zaidi katika usambazaji wa matokeo ya tafiti kwa kushirikiana na Halmashauri za wilaya, watu binafsi, asasi zisizo za kiserikali (NGOs na CBOs), Mashirika ya Dini, Wahisani na Serikali hususan TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kusimamia maendeleo ya watumishi, kuhakikisha kuwa mazingira ya kazi yanaboreshwa ili kuinua ari ya kufanya kazi. Mazingira hayo ni pamoja na kuwapatia mafunzo, kuboresha huduma za Ofisi, kuwapatia stahili zao ipasavyo pamoja na utawala bora. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2002/2003, Wizara imewapatia mafunzo watumishi 190 kati yao 21 walihudhuria mafunzo ya muda mrefu (5 nje ya nchi na 16 ndani ya nchi) na 169 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi (12 nje ya nchi na 157 ndani ya nchi).

Baada ya kukamilisha mafunzo kwa Maafisa Ardhi 98 katika mwaka wa fedha 2001/2002 kuhusu Sheria za Ardhi, Wizara iliahidi kutoa mafunzo ya aina hiyo kwa Maafisa Ardhi 50 katika mwaka wa fedha 2002/2003. Kutokana na kukosekana kwa idadi inayotosheleza ya Maafisa Ardhi wenye sifa, mafunzo hayo hayakuweza kufanyika kama ilivyokuwa imepangwa. Bado naendelea kulisitiza kuwa Halmashauri ziajiri watumishi wenye sifa kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi katika Sekta ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003 Wizara imewapatia watumishi vitendea kazi vya kisasa katika kuboresha utoaji huduma Wizarani. Vitendea kazi vilivyonunuliwa ni pamoja na Kompyuta 36 na Magari matatu. Kwa vile huduma za Sekta ya Ardhi hugusa watu wengi, Wizara ya Ardhi inapokea wageni wengi. Jumla ya wageni 124,786 walifika Wizarani katika mwaka uliopita kwa ajili ya kupatiwa huduma mbalimbali. Aidha, barua 13,054 zilipokelewa Wizarani na kushughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003 watumishi 137 walipandishwa vyeo na Wizara ilipata kibali cha kuajiri watumishi 78 kati ya hao watumishi 57 tayari wameajiriwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003 mafunzo yameendelea kuboreshwa katika Vyuho vya Ardhi Tabora na Morogoro. Jumla ya wanachuo 70 walihitimu katika fani mbalimbali. Katika mwaka wa fedha 2003/2004, Vyuho vyote kwa pamoja vinatarajia kutoa wahitimu 81.

Mheshimiwa Spika, wakati nazungumza kuhusu Shirika la Nyumba la Taifa, nilizungumzia suala la Rushwa linalolikabili Shirika hilo na jitihada zinazofanywa ili kupambana na rushwa hiyo. Ni muda muafaka kuzungumzia juhudi zinazofanywa na Wizara kwa ujumla katika kupambana na Rushwa, katika kufanya hivyo Wizara yangu imefanya yafuatayo:-

Wizara imebuni mradi wa kupima viwanja 20,000 katika Jiji la Dar es salaam. Hivi sasa viwanja vinagawiwa kwa uwazi jambo ambalo limepunguza udanganyifu wa kugawa viwanja visivyokuwepo, imebuni zoezi la kupiga picha kumbukumbu zilizomo katika majalada ya viwanja (*Document Scanning*) na kuingiza kumbukumbu hizo katika kompyuta kwa lengo la kupunguza uwezekano wa kughushi na kunyofoa nyaraka, imebuni mfumo wa kuweka kumbukumbu kwenye kompyuta na mahesabu yote yanayohusu ukadiraji kodi za viwanja kwa madhumuni ya kuzuia udanganyifu, imeanzisha utaratibu wa kutoa barua za toleo (*letter of Offer*) zenye namba maalum na kutoa hati miliki kwa muda mfupi kwa kutumia kompyuta, imeanzisha mkakati wa kushughulikia malimbikizo ya kazi za miaka ya nyuma ikiwemo hati, vibali vya uhamisho na rehani za milki, ukaguzi wa hesabu za upimaji, utatuzi wa migogoro ya ardhi na nyumba na inatoa elimu ya kupambana na Rushwa katika mikutano mbalimbali ya wizara kwa kutumia Wataalamu kutoka Taasisi ya Kuzuia Rushwa na imetenga fedha kwa ajili ya kutoa mafunzo ya maadili kwa watumishi.

Ningependa kutoa rai kwa wananchi kwamba mikakati hii iliyowekwa na Wizara itafanikiwa tu iwapo wananchi watatoa ushirikiano katika kufuata utaratibu wa kupata huduma zinazotolewa na Wizara ya Ardhi na kuwafichua wale wote wanaokiuka taratibu zilizowekwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kupambana na ugonjwa hatari wa Ukimwi katika mwaka wa fedha 2002/2003. Ndani ya Wizara tumekuwa tukikumbushana athari na namna ya kujikinga na ugonjwa huu ambao kwa kiasi kikubwa umeathiri utendaji kazi. Ili kuimarisha mapambano hayo Wizara imezindua rasmi Kamati ya Kupambana na Ukimwi pamoja na kuendesha semina za uhamasishaji. Wafanyakazi wote walioko Makao Makuu wamehudhuria Semina hizo.

Mheshimiwa Spika, watumishi walioko nje ya Makao Makuu watahudhuria semina hizi katika mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kama ilivyokuwa mwaka jana, jitihada zetu zitaendelea kuelekezwa katika matumizi bora ya ardhi kama rasilimali ya msingi katika uzalishaji mali katika Sekta za Kilimo, Mifugo, Misitu na kadhalika. Jitihada zitaendelea kufanywa kuboresha mazingira ya uwezeshawaji wa matumizi endelevu ya ardhi Mijini na Vijijini. Mkakati wa Elimu kwa Umma kuhusu Sera na Sheria za Ardhi, ambao umeandaliwa na kukamilishwa mwaka jana, sasa utanza kutekelezwa kwa vitendo kuanzia mwaka huu wa fedha 2003/2004. Natoa wito kwa Wadau wote waendeleo kushirikiana na Wizara yangu katika utekelezaji wa Mpango huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya majadiliano na mashauriano na Wadau wote, tumekubaliana kufanya marekebisho kidogo katika baadhi ya vifungu vya Sheria Mpya ya Ardhi. Ni matumaini yangu kwamba baada ya marekebisho hayo, vyombo vya fedha, hususan Mabenki yaliyopo nchini, yatatimiza wajibu wao wa kushirikiana na kuwawezesha wateja wao walio tayari kutumia Ardhi yao kama dhamana kwa Mikopo ya Benki.

Mheshimiwa Spika, sera ya Taifa ya Ardhi haijabadilika, Ardhi ya Tanzania ni mali ya raia wote wa Tanzania, Ardhi ya Tanzania haiuzwi kwa wasio raia wa Tanzania. Ardhi inatambuliwa kuwa na thamani, na inatarajiwa kutumika kama dhamana kwa mikopo ya vyombo vya fedha.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Naibu Waziri, Bibi Salome Sijaona, Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara, Taasisi na Wafanyakazi wote wa Wizara. Shukrani kwa wote waliotoa misaada kwa Wizara. Shukrani kwa vikundi vyote vinavyotoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya Sekta ya Ardhi na Makazi.

Mheshimiwa Spika, ili Wizara yangu iweze kutekeleza yote hayo niliyoyaeleza, sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2003/2004 kama ifuatavyo: shilingi 5,430,401,000/= kama Makusanyo ya Mapato ya Serikali, shilingi 5,413,928,900/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 600,000,000/= kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Kabla hatujaendelea, ngoja nirudie tangazo la vikao vya leo, naona sikuliweka vizuri, ni kwamba Kikao cha pamoja na Kamati ya Uongozi na Tume ya Huduma za Bunge kitafanyika saa 6.00 mchana. Baada ya hapo, saa 7.00 mara baada ya kuahirisha Bunge, Mwenyekiti wa Kamati ya Wabunge wote anaomba tuwe na kikao kifupi cha Wabunge wote kwa lengo la kupokea taarifa itakayotoka kwenye kikao changu cha Tume ya Huduma za Bunge. *(Makofi)*

Kwa hiyo ya *TAPAC* mtakutana baada ya Kikao cha Wabunge wote saa 6.00 mchana, Kikao cha Tume saa 7.00 mchana na Wabunge wote. Ahsante. Tunaendelea. Namwita Mwakilishi wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH (k.n.y. MHE. ELIACHIM J. SIMPASA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 81(1) ya Kanuni ya Bunge Toleo la mwaka 2003, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Kilimo na ardhi juu ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2002/2003 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2003/2004.

Kwanza kabisa naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati hiyo ambao ni Mheshimiwa Eliachim Simpasa Mwenyekiti, Mheshimiwa Alhaj Shawej Abdallah, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Anatory Choya, Mheshimiwa Edward Ndeka, Mheshimiwa Musa Lupatu, Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Mheshimiwa Philip Magani, Mheshimiwa Dr. Suleiman Juma Omar, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Salama Khamis Islam, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Robert Mashala, Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mheshimiwa Paul Makolo, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Omar Juma Omar na Katibu Ndugu Elisa Mbise.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nianze na kusema kwamba ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri asilimia mia moja. *(Makofi)*

Pili, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Gideon Cheyo, Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Tatu Ntimizi na Katibu Mkuu, Bibi Salome Sijaona, kwa

ushirikiano wao mkubwa walioutoa kwa Kamati wakati wa kutembelea Wizara hiyo na asasi zake na baadaye wakati wa kujadili bajeti ya Wizara hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujadili utekelezaji wa bajeti ya Wizara hii, Kamati yangu ilipata fursa ya kutembelea Idara mbalimbali za Wizara pamoja na kuona miradi inayotekelezwa na Wizara hiyo pamoja na Shirika la Nyumba la Taifa. Ziara hizi zilisaidia sana Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati yangu kujionea wenyewe na kuelewa kwa undani zaidi baadhi ya shughuli zinazotekelezwa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kutembelea baadhi ya Idara zilizopo Wizarani ikiwa ni pamoja na Idara ya Uimarishaji na Upatikanaji wa Kumbukumbu za Ardhi, Idara ya Ardhi, Idara ya Maendeleo ya Makazi na Idara ya Upimaji na Ramani. Kamati ilijionea hatua kubwa iliyofikiwa na Wizara kwa kuweka kumbukumu nyingi kwa kupitia Idara ya Uimarishaji na Upatikanaji wa Kumbukumbu za Ardhi. Kwa kutumia teknolojia ya kisasa Kamati iliona jinsi ambavyo *Letter of Offer* inavyoweza kuandaliwa na kutolewa kwa muda usiozidi dakika tatu tu na hati kutolewa kwa kipindi kisichozidi wiki mbili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika cha kufurahisha zaidi ni kwamba programu hizi zimetengenezwa na wataalam wa Wizara wenyewe. Kamati inaipongeza sana Wizara kwa hatua iliyofikia ya kutoa huduma kwa wananchi kwa ufanisi mkubwa zaidi jambo ambalo limepunguza sana kama sio kuondoa kabisa tatizo la mianya ya rushwa ambalo kwa muda mrefu lilikuwa kero kubwa kwa wananchi katika Sekta ya Ardhi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ramani na kumbukumbu zilizopo ndani ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi ni hazina kubwa na muhimu na ni sahihi na zenye kuelezea kwa kina michoro mbalimbali ya kijiografia kama uoto, hali ya hewa, mabonde, mito, miinuko na kadhalika. Inashauriwa kwamba itakuwa jambo lenye manufaa kwa Wizara nyingine kutembelea Idara husika ndani ya Wizara hii ili kupata huduma za kumbukumbu hizo za ramani, michoro na kadhalika kwa matumizi ya mipango yao kiwizara. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Kamati pia iliweza kutembelea Idara ya Upimaji na Ramani ambapo ilipata maelezo juu ya hatua mbalimbali zinazotumika kutayarisha ramani ikiwemo upimaji wa viwanja.

Kamati ilijionea jinsi ramani zinavyotayarishwa kwa kutumia teknolojia ya kisasa ambayo imeleta ufanisi mkubwa katika zoezi la upimaji wa viwanja. Kwa kutumia teknolojia ya kompyuta, Wizara sasa inaweza kuweka kumbukumbu za viwanja na kubaini wamiliki na walipa kodi za viwanja.

Mheshimiwa Spika, jitihada hizi zinafaa zipongezwe kwani ikiwa utaratibu huu utafanyika kwa nchi nzima utaondoa kabisa tatizo la kiwanja kimoja kupewa mtu zaidi ya mmoja na pia litapunguza kama sio kuondoa kabisa migogoro ya mipaka ya ardhi ikiwa ni pamoja na mashamba.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu pia ilipata maelezo ya kina juu ya utekelezaji wa mradi wa kupima viwanja 20,000 katika Jiji la Dar es Salaam uliokisiwa kugharimu zaidi ya shilingi bilioni 8.9. Jumla ya michoro 44 yenye viwanja 20,000 ya makazi na 4,000 ya huduma mbalimbali iliandaliwa.

Aidha, Kamati ilipata fursa ya kutembelea eneo la Tuangoma moja ya maeneo ambayo mradi huu unatekelezwa. Katika eneo la Tuangoma ambapo upimaji umekamilika jumla viwanja 3,288 vimekwisha kupimwa kati yake 3,151 ni kwa ajili ya makazi na biashara na 137 kwa ajili ya huduma mbalimbali za kijamii.

Kazi ya kutengeneza miundombinu ya barabara na mifereji ilikuwa inaendelea na sehemu kubwa ya kazi ya kutengeneza barabara ndani ya eneo lililopimwa ilikuwa imekamilika, hadi Kamati ilipopata taarifa hii jumla ya viwanja 13,108 ilikuwa vimekamilika kupimwa katika maeneo ya Tuangoma, Kisota, Mbweni, Mpiji, Buyuni na Mbweni JKT na jumla ya shilingi milioni 7.09 vilikuwa vimeshalipwa kama fidia kwa wananchi katika maeneo mbalimbali ya mradi huu.

Mheshimiwa Spika, mradi wa Shirika la Nyumba la Taifa, Kamati ilipata nafasi ya kutembelea mradi wa ujenzi wa nyumba za maakazi ulioko eneo la Boko Jijini Dar es Salaam. Kamati ilielezwa kwamba mradi huu ulibuniwa kwa lengo la kupunguza tatizo la nyumba za kuishi katika Jiji la Dar es Salaam na ni sehemu ya utekelezaji wa programu wa kujenga nyumba za kuishi katika miji mikuu ya Mikoa ya Tanzania Bara, ambayo inalenga kupunguza tatizo la maakazi bora katika maeneo ya mijini.

Mradi ambao una lengo la kuwafanya Watanzania na hasa watumishi wa umma kuwa wamiliki wa nyumba badala ya kuwa wapangaji. Kamati inaipongeza Wizara na Shirika la Nyumba la Taifa kwa kubuni mradi huu ambao kama utakuwa endelevu utaleta mapinduzi makubwa ya kuwa na makazi bora nchini.

Mheshimiwa Spika, mradi wa nyumba na makazi wa Boko utakuwa na jumla ya nyumba 200 za aina mbalimbali. Tangu ulipoanza mwishoni mwa mwaka 2000 jumla ya nyumba 189 zimejengwa na zinaendelea kujengwa. Ujenzi wa nyumba hizi unaenda sambamba na uwekaji wa huduma muhimu kama barabara, maji na umeme.

Aidha, katika eneo hili yametengwa maeneo ya huduma za jamii, kama Shule, Masoko, maduka, sehemu za kuabudia, sehemu za burudani na kadhalika. Kamati ilielezwa kwamba mradi huu utakapokamilika utakuwa ni kitovu cha mji mpya ndani ya Jiji la Dar es Salaam. Mradi huu unakiswiwa kugharimu jumla ya shilingi bilioni 3.95 ambapo kati ya fedha hizo shilingi milioni 1.5 ni mkopo toka Shirika la *Shelter Afrique* lenye makao makuu yake Nairobi, Kenya. Kiasi kilichobaki kitachangiwa na Shirika pamoja na wateja kupitia malipo ya awali ambayo ni asilimia 25 ya bei ya nyumba.

Mheshimiwa Spika, moja ya mafanikio ambayo Shirika limepata kutokana na utekelezaji wa mradi huu ni kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa kuwa Shirika lijenge nyumba kwa msingi wa *estate* ili kuboresha hali za makazi. Kamati ilielezwa kwamba wanunuzi wa nyumba hizo wamepatikana na wanaendelea kupatikana. Hadi kufikia wakati Kamati inatembelea mradi huu Juni 2, 2003 jumla ya nyumba 159 zilikuwa zimekwishapata wanunuzi ambao walikuwa wamelipia ama malipo ya awali au zaidi na wachache wamekamilisha malipo. Hali hii inaridhisha, hasa kwa kuzingatia kwamba hakuna chombo cha kutoa mikopo ya ujenzi au ununuzi wa nyumba.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya Kamati, katika kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2002/2003 na malengo ya Bajeti ya mwaka 2003/2004 kwa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Kamati ilipata maelezo ya kina na majukumu ya Wizara, malengo ya Wizara na utekelezaji wake kwa mwaka uliopita na mipango iliyowekwa kwa mwaka ujao wa fedha. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuweza kutekeleza malengo na miradi mbalimbali ya kuboresha makazi nchini kama ilivyofanuliwa kwenye maelezo ya Waziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka ujao wa fedha 2003/2004 Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi imepangiwa kiasi cha shilingi milioni 600 tu kwa miradi ya maendeleo. Kiasi hiki ni kidogo sana kulinganisha na majukumu makubwa ya Wizara ya kuboresha makazi nchini. (*Makofi*)

Hili linadhihirishwa na ukweli kwamba mradi mmoja tu wa kupima viwanja 20,000 katika Jiji la Dar es Salaam kama nilivyoeleza awali unagharimu kiasi cha shilingi bilioni 8.9 kwa maana nyingine ni kwamba kiasi cha Bajeti ya Maendeleo ya Wizara hii kwa nchi nzima ni sawa na asilimia 6.7 tu ya gharama ya mradi mmoja wa kupima viwanja 20,000 katika Jiji la Dar es Salaam. (*Makofi*)

Kwa kuzingatia ukweli huu Kamati inashauri Serikali kuongeza Bajeti ya Maendeleo kwa Wizara hii ili iweze kutekeleza majukumu yake ya kuboresha makazi nchini na hasa Mipango Miji ili kuwanusuru wananchi na Taifa dhidi ya maafa yanayotokana na ujenzi holela kama vile mafuriko na magonjwa ya mlipuko hasa kipindupindu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Wizara kwa jinsi ilivyoanza kutekeleza Sera ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 kwa kuwa na mradi wa kupimwa viwanja 20,000 katika Jiji la Dar es Salaam, kama ilivyoelezwa awali mpango huu unakwenda sambamba na uwekaji wa huduma muhimu

kama vile barabara, maji na umeme. Ili kuongeza ufanisi katika mpango nzima wa kuboresha makazi nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kuwa na mpango shirikishi ambapo kila Wizara, Idara na Halmashauri husika itakuwa na jukumu la kupeleka miundombinu husika pale mradi wa kuboresha makazi unapotekelezwa.

Utaratibu huu utaipunguzia gharama Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi na hii ndiyo kuleta unafuu wa bei ya viwanja kwa wananchi, hasa kwa kuzingatia pia kwamba weka huduma kama vile maji na umeme ni sehemu tu ya kupanua biashara kwa Idara husika.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mradi wa kupima viwanja 20,000 Jijini Dar es Salaam, Wizara ilihitaji jumla ya shilingi bilioni 8.9 ambazo Kamati ilielezwa kwamba ni mkopo toka Hazina ili kuweza kurejesha fedha hizi Wizara inalazimika kuuza viwanja vilivyopimwa kwa kati ya shilingi laki tano kwa ujazo wa juu hadi kufikia shilingi milioni tatu laki sita kwa ujazo wa chini kulingana na mahali kiwanja kilipo. Ili kuwezesha wananchi wengi zaidi kupata viwanja hivi, Kamati inashauri kwamba kwanza fedha iliyotolewa na Hazina kama mkopo kwa Wizara, itumike kama *Revolving Fund* ya kuendeleza upimaji viwanja zaidi na wananchi waruhusiwe kulipa kidogo kidogo kwa muda maalum. *(Makofi)*

Pili, Serikali iangalie uwezekano wa kupunguza bei ya viwanja ili kuwawezesha wananchi wengi wenye kipato kidogo kumudu kununua viwanja hivyo. Aidha, ili kuwawezesha wananchi kujenga nyumba bora katika viwanja vinavyopimwa na kununua nyumba zinazojengwa na Shirika la Nyumba la Taifa, Kamati inashauri Serikali kuanzisha mpango kwa kutoa mikopo ya muda mrefu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika maeneo mengi ya miji hasa mikubwa hapa nchini kumekuwa na tabia ya kujenga majengo bila kufuata taratibu zilizowekwa na Mipango Miji. Yapo maeneo maalum yanayotakiwa kujengwa majengo yasiyo ya ghorofa, hata hivyo utaratibu huu umekuwa ukikiukwa na matokeo yake magorofa yamekuwa yakijengwa bila kuzingatia taratibu na hivyo kuharibu kabisa dhana ya Mipango Miji. Kamati inashauri Wizara kufuatilia kwa karibu ujenzi wa makazi mijini ili kuhakikisha kwamba vibali vya ujenzi vinatolewa kwa kuzingatia Sheria na taratibu za Mipango Miji. Aidha, Kamati inashauri kwamba upimaji wa viwanja maeneo ya mijini uzingatie pia sehemu za kuegesha magari ambazo mara nyingi huwa zinasahaulika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu maeneo ya wazi mijini, Kamati inashauri Serikali kukomesha kabisa tabia ya watu kuvamia maeneo haya na kuyajenga. Wale wanaojenga maeneo haya, Kamati inashauri wachukuliwe hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kuvunja majengo hayo bila kuwalipa fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ipo miji midogo hapa nchini ambayo inakua kwa haraka sana lakini haijawekewa taratibu za Mipango Miji na hivyo wananchi wamekuwa wakijenga majengo kiholela. Kamati inashauri Serikali kufanya tathmini na kutambua miji midogo inayokua kwa haraka ili itoe kipaumbele katika kuweka Mipango Miji katika maeneo haya.

Aidha, Kamati inashauri Serikali kuzisaidia Halmashauri zote nchini kujenga uwezo wa kuwa na wataalam wa Ardhi ili ziweze kutoa huduma bora za ardhi kwa wananchi. Pia Wizara iwe inatenga fedha kwa ajili ya kuviwezesha Ofisi za Ardhi Wilayani kutekeleza majukumu yake badala ya kutegemea Ofisi hizi zitengewe fedha na Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1997 inasema kwamba: “Mtu au raia atapewa haki ya kumiliki ardhi na Serikali, Mamlaka iliyopewa madaraka ya kufanya hivyo ni Halmashauri na Vijiji kwa ardhi inayomilikiwa kimila.” Kwa upande wa Vijiji Sera hii bado haijaleweka vizuri hasa mamlaka yaliyopewa Halmashauri za Vijiji kwa ardhi iliyomilikiwa kimila.

Kamati inashauri kwamba wanavijiji waelimishwe kikamilifu juu ya Sera hii ili kuepusha migogoro inayoweza kujitokeza pale mtu anapopewa na kijiji haki ya kumiliki ardhi ambayo pengine ardhi hiyo ilikuwa inamilikiwa na ukoo.

Aidha, kutokana na kuwepo kwa migogoro mingi ya mipaka kati ya Wilaya na Wilaya, Vijiji na Vijiji pamoja na migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji, Kamati inashauri Wizara kupima na kuweka wazi mipaka ya maeneo kote nchini ili wananchi wa nchi moja waache kugombania mipaka. *(Makofi)*

Kamati inashauri kwamba kila kijiji kipimwe na kupewa nakala ya ramani ya eneo lake ili kuondoa migogoro ya mipaka. Aidha, Kamati inashauri Serikali ione kwamba kwa kutumia urafiki na ujirani mwema uliopo kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa na Serikali ya Malawi chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Rais Bakili Muluzi, ni jambo jema na la manufaa zaidi kwa wananchi wa pande zote mbili kwamba wasi wasi juu ya mpaka uliopo wa Ziwa Nyasa utaondolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika maelezo yake kwa Kamati Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, alijulisha Kamati kwamba Serikali inaandaa marekebisho ya Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 ili pamoja na mambo mengine wananchi waweze kutumia ardhi kama dhamana na kupata mikopo kutoka kwenye mabanki.

Kamati inashauri Serikali kuwa makini katika kufanya marekebisho ya Sheria ya Ardhi ili yasifanyike kwa lengo la kuwafurahisha wawekezaji hasa wenye mabanki bila kuzingatia maslahi ya wananchi wetu. Ni vyema wenye mabanki wakaelewa kwamba jukumu lao kufuatilia urejeshwaji wa mikopo wanayotoa badala ya kusubiri kukamata ardhi au dhamana nyingine ya mkopaji pale anaposhindwa kulipa. *(Makofi)*

Kuhusu Hati ya kumiliki ardhi kwa wananchi. Kamati inashauri kwamba Sheria husika zifanyiwe marekebisho ili mwananchi aongezewe muda wa kumiliki ardhi, toka miaka 33 ilivyo sasa hadi miaka 99 kama ilivyo kwa hati miliki wanazopewa wageni.

Mheshimiwa Spika, wakati Kamati yangu ilipotembelea Makao Makuu ya Wizara, Kamati iliona jinsi jengo la Idara ya Upimaji na Ramani lilivyochakaa. Uchakavu huu unahatarisha usalama wa kumbukumbu muhimu zilizopo ndani ya jengo hilo, ikiwa ni pamoja na ramani muhimu za maeneo mbalimbali nchini. Kamati inashauri Serikali kulifanyia ukarabati jengo hilo au kujenga jipya mapema iwezekanavyo ili kunusuru kumbukumbu zilizopo ndani ya jengo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali moja ya kazi ambazo Kamati ilifanya ni kutembelea na kuona shughuli za Shirika la Nyumba la Taifa. Moja ya matatizo ambayo Shirika hili linakabiliwa nayo ni wananchi kutokulipa kodi za pango kwa nyumba za Shirika. Kamati ilielezwa kwamba Shirika linadai malimbikizo ya kodi ya pango ya zaidi ya shilingi bilioni 11. Kiasi hiki cha limbikizo la kodi ni karibu mara tatu ya gharama za kujenga mradi wa nyumba 200 za kuuza kama ule wa Boko, Jijini Dar es Salaam. Kwa maana nyingine fedha hizo zingeweza kujenga mradi wa nyumba 600 za kisasa kama zilivyo za mradi wa Boko.

Kwa kuona udhaifu huu wa ukusanyaji wa kodi za pango, Kamati inaishauri Serikali kupitia upya Sheria zote zinazohusiana na kodi za pango ili kuwezesha Shirika la Nyumba kukusanya kodi bila vikwazo vinavyowekwa na wapangaji wakorofi. Aidha, Kamati inachukua fursa hii kutoa wito kwa wananchi kujenga tabia ya kulipia huduma za umma wanazozitumia na kuacha kasumba ya kuona huduma za umma ni huduma za bure.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Nyumba la Taifa lina jukumu muhimu la kutekeleza Sera za makazi nchini. Pamoja na Shirika hili kuendelea kujenga nyumba mpya za makazi na biashara, Shirika lina nyumba nyingi ambazo wapangaji wake hawaeleweki. Kamati inashauri Wizara kupitia Shirika la Nyumba la Taifa kufanya tathmini maalum ya kuwatambua wapangaji halali wa majengo yake ili kuona kama wamekaa kwenye nyumba hizo kihalali na kama wamelipa kodi zinazostahiki. *(Makofi)*



Mheshimiwa Spika, napenda kumalizia kwa kuipongeza sana Wizara kwa hatua walizofikia katika kutoa huduma ya ardhi hasa katika ngazi ya Taifa kwa kurahisha utoaji wa Hati.

Hata hivyo, ni matumaini ya Kamati kwamba jitihada zinazofanyika katika ngazi ya Wizara zitatekelezwa pia katika ngazi ya Wilaya ambapo bado kuna urasimu na matatizo ya mianya ya rushwa katika upimaji na utoaji wa hati za viwanja na mashamba.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inashauri Wizara kukamilisha haraka utoaji wa hati miliki zote wananchi walizoomba miaka ya nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo napenda kusema tena kwamba kwa niaba ya Kamati na mimi mwenyewe ninaunga mkono hoja ya Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kabla sijamwita Msemaji wa Upinzani, wafuatao ndiyo watakuwa wasemaji wanne wa mwanzo katika hoja hii. Mheshimiwa Kisyeri Chambiri, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Suleiman Juma Omar na Mheshimiwa Halima Kimbau. Sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara hii Mheshimiwa Ali Said Salum. *(Makofi)*

**MHE. ALI SAID SALUM – MSEMAMI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza hotuba yangu nilitaka niseme neno moja. Nimekuwa nikifuatilia utaratibu wa wenzetu hawa ...

**SPIKA:** Subiri kidogo wakitengenezee *microphone*. Hatukusikii sawasawa!

**MHE. ALI SAID SALUM – MSEMAMI WA UPINZANI KWA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikifuatilia utaratibu wa wenzetu wa TVT jinsi wanavyofikisha huduma kwa wananchi. Lakini nataka nichukue nafasi hii kutoa masikitiko yangu mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba imekuwa ni mtindo ikifika wakati wa kuwasilisha mtu wa Upinzani TVT inakata mawasiliano yale na baadaye wanaweka muziki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sijui ni kwa nini kwamba hii hotuba haistahiki wananchi wasikie au sisi hatuna haki ya kusikilizwa na wananchi? Hili nilitaka nilieleze na lirekebishwe ili kuanzia hotuba yangu hii iweze kupata *good coverage* kuanzia mwanzo hadi mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunjalia mimi na sisi sote afya njema hata tukaweza kufika hapa na kushiriki katika shughuli za Bunge asubuhi hii.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuchukua fursa hii kukushuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maoni kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kuhusu Bajeti ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2003/2004 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43 Kifungu kidogo cha (5) (b) na (c) 2003.

Mheshimiwa Spika, ninapenda tena kuchukua fursa hii kuwashukuru wananchi wote wa Jimbo la Ziwani kwa kunichagua kwa kura nyingi na kuweza kushinda kwa karibu asilimia 90. Ushindi wangu ni ushindi wa wapenda haki wote wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa John Malecela, Mbunge wa Mtera na Mheshimiwa Anne Kilango, Mbunge Viti Maalum, kwa kufunga pingu za maisha tarehe 28 Juni, 2003 hapa Mjini Dodoma. Mwenyezi Mungu awajalie kila lenye kheri katika safari yao ndefu ya ndoa na nadhani matatizo mepesi mepesi kuanzia wakati huo yatakuwa yamewapungukia. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mbunge na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, mama mkwe wangu Tatu Ntimizi, kwa ushirikiano walionipa ambao umewezesha kupata urahisi wa kuandaa hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi imeweka dira maalum ya kuweza kuongoza uendeshaji wa shughuli za Wizara hiyo. Dira ya Wizara ni kuwa na huduma bora zaidi za uendelezaji ardhi na makazi, ni jina kijijini ardhi iliyopimwa na ramani kutayarishwa vizuri kwa matumizi mbalimbali na uwekezaji mzuri na upatikanaji wa haraka wa kumbukumbu za ardhi kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona utekelezaji wa dira hiyo utafanikiwa tu ikiwa Wizara husika itazingatia ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, vitengwe fedha za kutosha za uenezaji shughuli za Wizara hasa zile za maendeleo. Katika Bajeti ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2003/2004 fedha za maendeleo ni shilingi milioni 600, wakati Bajeti ya Wizara hiyo katika fungu hilo hilo la maendeleo katika mwaka wa 2002/2003 ni shilingi bilioni 10. Kwa hali hiyo bajeti ya mwaka 2003/2004 ya Maendeleo ya Wizara imepangiwa fedha pungufu ya zile za mwaka 2002/2003 kwa shilingi karibu bilioni 9.4 sawa na asilimia 94.

Mheshimiwa Spika, ningemwomba Mheshimiwa Waziri atakapofanya majumuisho atueleze ni kwa nini kikatolewa kiasi hiki kikubwa kwa mwaka uliopita kwa Sekta hiyo hiyo leo ikapungua kwa asilimia hii kubwa ya kutisha.

Mheshimiwa Spika, usambazaji wa kitabu cha Kiongozi cha mwana kijiji katika utumiaji wa Sheria ya Ardhi Vijijini Na. 5 ya mwaka 99 siyo ya kuridhisha. Kitabu hicho hakijasambazwa katika Mikoa yote nchini kama ilivyoonyeshwa katika Jedwali Na. 1 katika kitabu cha Bajeti ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi katika mwaka 2001/2002 kwa Mikoa kama Kagera, Kigoma, Rukwa, Lindi na Shinyanga. Ili kuleta maendeleo na kupunguza mizengwe isiyo na sababu katika Sekta ya Ardhi, ni vyema vitabu vya Sheria hiyo vikasambazwa Mikoa yote na Wilaya zote na idadi ikaongezwa.

Mheshimiwa Spika, dira hiyo iliyowekwa na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, itashindwa kutekelezeka kama suala la ardhi na viwanja halitafanyiwa marekebisho ili kuleta nafuu kwa wananchi. Kwani hiyo ada ya kiwango cha shilingi laki tano ni kubwa sana ukilinganisha na kipato cha wananchi wengi ambacho hakifikii hata shilingi laki moja kwa mwaka. Hali hiyo inaweza kusababisha viwanja hivyo kunyang'anywa na hatimaye kuchukuliwa na watu wachache sana wenye uwezo wa kipesa.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa kushirikiana na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ihakikishe kuwa watu hawaweki makazi katika sehemu za mabondeni ambazo ni rahisi kukumbwa na mafuriko. Hivyo kuleta hasara kubwa kwa wananchi hao. Ada kubwa za kulipia viwanja na urasimu katika kupata viwanja ni kichocheo kikubwa cha watu kujenga mabondeni.

Mheshimiwa Spika, dira ya Wizara hii itaonyesha mafanikio ikiwa itawekwa umuhimu wa kuweka alama zilizo wazi na za kudumu katika mipaka ya Wilaya na Mikoa. Utekelezaji wa suala hilo utapunguza migogoro ya mipaka kati ya Wilaya na Wilaya au Mkoa na Mkoa.

Mheshimiwa Spika, hati za umilikaji ardhi wa miaka 33 zitolewazo kwa wazawa zibadilishwe na umiliki uwe ni wa miaka 99 kama ilivyo kwa wageni. Kwa kuendeleza utaratibu huo wa zamani wazawa wanakandamizwa wakati wageni wananeemeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakulima na wafugaji kugawiwa ardhi sehemu moja huleta migongano ambayo inafanya utekelezaji wa dira ya Wizara hiyo usiweze kupata mafanikio mazuri kama vile ilivyotokea katika Wilaya ya Kilosa mwaka 1999. Hivyo ugawaji wa maeneo tofauti ya ardhi kwa wakulima na wafugaji ukutiliwa maanani utaepusha migogoro na mizozo isiyo na sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile katika suala la ugawaji wa ardhi kwa wananchi watokao kwenye Mikoa yenye upungufu wa ardhi ya kulishia mifugo ni vyema usiingiliane na sehemu ambazo wanamiliki wenyeji husika ambao hao wafugaji wanataka kuhamia. Kuwaweka sehemu moja wageni na wenyeji kunaweza kuleta migongano kati yao hasa kutokana na tofauti za kiutamaduni, maslahi ya kiuchumi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kusaidia kuinua maisha ya wananchi wa Tanzania hasa katika kuwa na nyumba bora salama, ni vyema Serikali ikafanya juhudi za makusudi kuhamasisha uundaji zaidi wa Mashirika ya Ujenzi wa nyumba (*Housing Corporation*) na vyama vya Ushirika vya Ujenzi wa Nyumba za bei nafuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa wananchi ambao wamegawiwa viwanja lakini uendelezaji umechelewa kutekelezwa kutokana na gharama kubwa za uchoraji wa ramani na ada na ada kuwa kubwa ya kupata kibali cha kuruhusiwa kujenga. Ni vyema vikatafutwa taratibu za kuwakwamua kuliko kuwakomoa. (*Makofi*)

Baadhi ya wananchi ambao hugawiwa viwanja, hukaa bila kuviendeleza kwa zaidi ya miaka mitano, wakati kuna wananchi wengi wenye shida na viwanja na wana uwezo wa kujenga nyumba kwa angalau muda usio mrefu sana. Ni kwa nini Serikali isiweke utaratibu maalum kwa mtu yoyote atakayepewa kiwanja na ajenge kwa miaka mitano, kiwanja kigawiwe kwa mtu mwingine mwenye kuhitaji na ambaye yuko tayari kukiendeleza kwa muda usio mrefu sana na mmiliki wa mwanzo atatafutwa namna nyingine ya kupata kiwanja atakapokuwa tayari kujenga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo litawezesha dira ya Wizara itekelezwe kwa urahisi ni kwamba upimaji wa viwanja na hasa vijijini unaendelea polepole sana kutokana na Serikali kutokuwa na wataalam wa kutosha wa shughuli za upimaji wa ardhi. Suala hilo linaweza kurekebisha kwa Serikali kuruhusu wapimaji binafsi kupipima viwanja. Serikali iwe na kazi ya kufuatilia utendaji kazi wa wataalam hao binafsi kama ni sahihi na unafuatwa maadili ya kazi ya upimaji au laa. Kwa kuruhusu wataalam binafsi kupimwa viwanja watu wengi wanaweza kupata viwanja vilivyopimwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna migogoro mingi mijini na vijijini uhusuyo umilikaji wa ardhi, aidha kwa kiwanja kimoja kumpa mtu zaidi ya mmoja au kuvamiwa na mtu mwingine kwa nguvu. Hali hiyo inaweza kurekebisha kwa kuunda Mahakama Maalum kama ilivyo Mahakama ya Biashara. Mahakama ziundwe kuanzia ngazi ya Kijiji au Kata hadi ngazi ya Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kupunguza muda wa maandalizi ya hati kumiliki ardhi kutoka siku 180 za kusubiri mpaka siku 14 wiki mbili, ni jitihada nzuri zenye kuleta matumaini. Ni jukumu la Wizara kupunguza zaidi muda huo kwani matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano yanaruhusu muda huo kwa mfupi zaidi. Hizi ni zama za *Administration* na hii ni *Government*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara kuweka mikakati ya kutokomeza na kupiga vita ugonjwa wa Ukimwi ni suala lenye kuonyesha mwelekeo wa Wizara kutekeleza dira yake kwa mafanikio mazuri na yenye matumaini. Ukimwi usipodhibitiwa kwa makusudi utamaliza wataalam wote wa Wizara ambao wamesomesha kwa gharama kubwa na Taifa. Kuwapunguzia shida wananchi ni pamoja na kuwa na Sera za kulinda maisha ya wataalam wa Wizara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji zimekuwa na uwelewa wa kuweza kutenga fedha maalum za upimaji na uenezaji shughuli za viwanja. Bado Wizara inalo jukumu la kusimamia kwa karibu zaidi zoezi hilo.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeweka msukumo mkubwa kwa shirika lake la Taifa la Nyumba kuendelea kujenga nyumba za kununua au kupangisha kwa wananchi. Ni ishara kubwa kwa Wizara hiyo kuwa inatekeleza vyema dira yake.

Pia Wizara ishikamane zaidi na *NHC* kuhakikisha ujenzi wa nyumba nyingi zilizo bora na za bei nafuu kwa ajili ya kuuza na kupangisha, haziishii kule Boko Dar es Salaam tu, nyumba hizo zinahitaji kujenga nchini kote kuanzia Mbamba Bay mpaka Kiaka. Tandahimba mpaka Namanyere na Micheweni na Kiembe Samaki mpaka Sirari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bei za nyumba zinazouzwa zilitiwe maanani umaskini mkubwa wa Tanzania. Lengo lilikuwa ni kuwapa makazi bora walala hoi wa nchi hii na siyo kuwaneemesha zaidi wenye nacho tayari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara kuweka mikakati mizuri ya kuhakikisha kuwa Ofisi za Ardhi Wilayani zinaimarishwa ni suala la kutia moyo kwani huko ndiko kwenye matatizo makubwa na ndiko wananchi wengi waishiko. Utekelezaji huo utawezesha matatizo ya ardhi huko Wilayani na Vijijini kupungua kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara imepewa pongezi nyingine kwa utekelezaji wake nzuri wa majukumu yake na kuongeza idadi ya watumishi muhimu na vile vile kwa utaratibu wake wa kuendeleza kielimu wataalam wake. Wataalam hao ni nyenzo kubwa sana katika kuifanya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi itekeleze dira yake kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imedhamiria kuwapunguzia wananchi tatizo la uhaba wa viwanja, kwa kuwapatia viwanja katika mradi wa viwanja 20,000, namwomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana akumbuke kwamba wananchi walio wengi wana hamu ya kupata viwanja. Utaratibu alioufanya ni nzuri, kwenye matangazo yanatolewa mara moja, baadhi ya wataalam yaani wapima viwanja kukamilisha zoezi hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunachoomba ni kwamba Serikali ikubali wananchi kulipia kidogo kidogo kwani wengi wanaoomba ni watumishi wa Serikali na mashirika ya umma na wananchi wa kawaida. Kwa hiyo, kulipa kwa mara moja ni kitu kigumu. Tunaomba Serikali ifanye utaratibu wa kuruhusu malipo hayo yafanywe kwa awamu angalau tatu kuliko hivi sasa. Ikumbukwe kuwa nchi hii si ya matajiri tu bali watu wengi zaidi ni walio katika dingi la umaskini wa kutupwa au wa kupindukia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi kubwa za Wizara kupambana na rushwa ndani ya Wizara ieleweke wazi bado rushwa haijang'olewa katika Wizara hiyo. Juhudi za kufutulia mbali rushwa ya aina zote ni lazima zipambe moto zaidi mkishirikisha na Waziri Kivuli wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zipo habari kwamba wazungu wanaoikimbia Sera ya Ardhi kupewa wazawa kule Zimbabwe na Rais Robert Mugabe, wanaikodolea macho Tanzania wakidai wao ni wawekezaji. Tunaomba Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi iwe makini sana na wawekezaji wageni katika ardhi ili kukwepa matatizo yanayoikabili Zimbabwe sasa hivi kwa maslahi ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuishi katika nyumba bora ni haki ya msingi ya kila binadamu. Hata hivyo, bado kuna Watanzania wengi sana wanaoishi katika nyumba duni mno Mijini na Vijijini. Lipo pia tatizo hasa katika Miji yetu la watu wengi kutumia chumba kimoja jambo ambalo ni hatari kwa afya lakini pia linazo athari za kimaadili. Wapo pia Watanzania wengi tu wanaoishi viambazani na hata pembezoni mwa barabara na kwenye maeneo mengine mengi yasiyopendeza kwa mwanadamu kuishi. Tatizo kubwa ni umaskini uliokithiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi ivalie njuga tatizo la watu kukosa makazi bora. Kati ya mbinu zinazopendekezwa ni pamoja na sekta binafsi kuwezesha na kuhamasishwa kujenga nyumba nyingi hasa Mijini ambazo zitapangishwa kwa watu wenye vipato vya kawaida na zitakuwa na gharama ndogo kwa sababu ya ruzuku itakayotolewa na Serikali kwa wajengaji na vifaa vyote vya ujenzi ikiwa ni pamoja na mabati, misumari, saruji na mbao na kadhalika vipunguziwe sana kodi ili vipatikane kwa bei ya kawaida na hali hii imwezeshe mwananchi wa kipato cha chini angalau kumudu kujenga nyumba ya kawaida lakini iliyo bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna watu wengi wanaofanya biashara ya kufyatua na kuuza matofari ya saruji hasa katika Miji mikubwa. Juhudi yao si mbaya japokuwa mara nyingi wanaingilia maeneo ya barabara na Mijini. Tatizo kubwa na linalohitaji kutupiwa macho haraka, ni utengenezaji wa matofari yenye ubora wa chini sana huku mchanga ukiwa mwingi na saruji ikiwa ni ya kubabaisha tu. Watu wengi huyanunua matofari hayo bila kujua ubora wake ni wa chini na matokeo yake yamekuwa ni nyumba zilizojaa nyufa na wakati mwingine nyumba kubomoka na kuwaumiza kama si kuwaua watu. Wizara ihakikishe watu wanaofanya biashara ya matofari wanafanya shughuli hiyo siyo tu kwa lengo la kuganga njaa bali pia kuzingatia viwango sahihi na kulinda maslahi ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hitimisho, Kambi ya Upinzani inaendelea kuishauri Wizara ihakikishe kuwa mikakati yote iliyowekwa inasimamiwa vizuri na inatekelezwa. Vile vile, inashauriwa ifanye kazi kwa makini na ushauri wa mara kwa mara uwe unatolewa na Kambi ya Upinzani kupitia kwa Msemaji wake Mkuu, Mheshimiwa Ali Said Salim. Lengo la jumla ni maendeleo ya kisasa kwa Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka pia nichukue nafasi hii kumpongeza Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, japo simjui pamoja na timu yake ya wataalam katika kuandaa hotuba hii. Nategemea Mheshimiwa Waziri atanjulisha tukimaliza hafla hii. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kumaliza hotuba hii ninaomba nichukue nafasi maalum nikupongeze wewe, Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na Wenyeviti, Mheshimiwa Eliachim Simpasa na Mheshimiwa Anne Makinda, kwa jinsi mnavyoliendesha Bunge hili kwa usawa na umakini wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. KISYERI W. CHAMBIRI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza asubuhi hii ili niweze kutoa mchango wangu kwa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Spika, napenda nianze kwa kusema hivi, azma ya Taifa ni kupunguza umaskini. Kwa sisi ambao tuko Vijijini njia pekee ya kupunguza umaskini ni unapokuwa na ardhi unalima, unaifanyia kazi na unapata mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuelekeza mchango wangu hasa kwenye Jimbo langu na kwa maeneo ya Kata ya Kemambo ambayo inajulikana kama Nyamongo ambapo kuna mgodi wa dhahabu.

Mheshimiwa Spika, watu wanaoishi katika maeneo ya mgodi wa dhahabu wana bughudha kubwa hasa kuhusu maeneo ambayo wameyakalia na kuyamiliki kwa muda mrefu sana. Watu wana familia kubwa, wanahamishwa na hawajui wanahamishwa kwenda wapi.

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida na kulingana na Sheria zetu kama mgodi umeanzishwa sehemu ni sawa, kwamba tathmini ya mali itafanywa na wananchi wakishatathminiwa mali yao watahama kusudi waache nafasi mgodi uchimbwe. Lakini watu wanaochimba mgodi huwa ni wageni ambao wamekuja ndani ya nchi na pale wananchi wanapohamishwa, mtu ulikuwa na familia yako, wake zako na ng'ombe wako unalipwa fedha ambazo hazikithi kwa mfano unapewa shilingi laki moja unaambiwa hama na huelezwi unahamia kwenda wapi, ni kuwafanya wananchi wetu wawe wakimbizi ndani ya nchi yao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naongea kwa niaba ya hayo wananchi wa Nyamongo ambao mara kwa mara wanatolewa kwenye maeneo yao na fidia wanayolipwa haitoshi ili kusudi waweze kuanza maisha mapya. Hata kwa kawaida kwa mtu wa Serikali kama anahamishwa kutoka Mji mwingine kwenda Mji mwingine ni kawaida apewe *disturbance allowance* kabla hajapata muda wa kukaa, aishi azoe katika maeneo yale. Unapomhamisha mtu mwenye familia yake na usimweleze aende wapi badala ya kupunguza umaskini tunazidisha umaskini.

Kwa hiyo, watu wa maeneo hayo ya madini hasa watu wa Vijiji vya Kewanja na watu wa Vijiji vya Nyangoto, wengi wamehamishwa na wengi wana malalamiko, hawajaridhika kwa zoezi zima lilivyofanywa kwa maana hawaamini kwamba walivyolipwa ni sawa na ni haki.

Mheshimiwa Spika, kwa wakati tulionao haijulikani thamani ya ardhi. Tunaelewa wazi kwamba mtu akinunua kiwanja pale *Somara Independence* na mwingine anunue kiwanja Tarime, yote ni Miji lakini anayenunua kiwanja pale Dar es Salaam barabara ya Somara atalipa pesa nyingi kuliko atakayenunua Tarime. Thamani ya ardhi inapanda kulingana na kwamba inatumika kwa nini na sasa hii thamani ya hawa watu chini kuna dhahabu na juu wanaishi, kwa hiyo naamini kwamba thamani yake itakuwa kubwa zaidi kuliko sehemu nyingine ambapo ardhi haina kitu chochote chini na mtu angetaka kuishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hawa hawajaridhika, waliposikia kwamba kuna Bunge wakapenda kuwaleta wawakilishi wao, wawili wako hapo wamekaa, kuja kuleta malalamiko kwa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwamba tathmini yao ifanywe upya ili waelewe ni nini haki yao. Kwa mfano, mtu mmoja alishakaa akajenga, ana nyumba za kudumu, ana wake zaidi ya mmoja yaani watatu na pia ana ng'ombe lakini anaambiwa ahame na tathmini imefanywa bila yeye hata kujua ametathminiwa nini, anapewa shilingi laki tatu au shilingi laki nne anaambiwa toka na haelewi anakwenda wapi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunachotaka na tuchoomba ni kwamba mtu kama alikuwa anaishi sehemu toka hii dunia iumbwe na iwe dunia amekaa katika maeneo yake, unamhamisha, nilifikiri kwamba ilikuwa ni jambo la busara tu kwamba hata kama anahamishwa kwa eneo alilionalo, ni bora akaeleza kwamba ukitoka hapa ni bora uende eneo lingine.

Kwa hiyo, kwamba mtu hawezi kuhamishwa bila kuelewa kwamba anakwenda wapi, mtu mwenye familia. Hatutegemei kwamba tutawahamisha watu wetu kusudi waende kuishi mitini au waende kukaa sehemu nyingine ambayo hawaijui kwa sababu kwanza kwa Tarime ni kwamba ardhi imebanana sana, watu wamejaa, unapowaambia watu kwamba hama na wewe hukueleza kwamba toka hapa uende hapa, sasa unategemea kutakuwepo na nini? Ni kwamba tutawapata watu ambao hawana ardhi, tutawapata watu ambao hawana sehemu ya kukaa na kwa hiyo tutazidisha umaskini na tutaongeza ujambazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilichokuwa naomba kwa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri awasilikilize hawa ambao wamekuja kwa niaba ya wenzao, aone hoja zao na kuzisikiliza, amchague mtu mwingine aende akawafanyie tathmini na kama ni haki yao walipwe haki yao inayostahili na waonyeshe kwamba wakihama toka eneo hili waende eneo lipi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, si kwamba hao wananchi hawana hoja lakini hoja zao zote wakijaribu kuzieleza inaonekana kwamba hazisikilizwi. Diwani wao ambaye alikuwa anawatetea alitafutiwa kesi akafungwa, kwa hiyo hawana Msemaji kwa maana ya Diwani na pia Mwenyekiti wao wa Kijiji aliyekuwa anawasemea, alitafutiwa kesi naye akafungwa, kwa hiyo hawana mtu kwa maana ya Msemaji wao wa kuweza kuwatetea. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, si kwamba hili halijulikani kwa sababu hata hii mikutano ya kuhamisha, mikutano ya Kijiji mingine mpaka Mkuu wa Wilaya alishiriki lakini kauli inayotoka ni kwamba hameni bila kujua kwamba hao watu watakwenda wapi. Si kwamba ni mtu mmoja au ni watu wawili, ni Kaya karibu 100 au 120, sasa unahamisha wingi wa watu hao bila kujua watakwenda wapi.

Kwa hiyo, nimesimama niseme kwa niaba ya hao watu kusudi hii hoja ifike kwa Mheshimiwa Waziri na Wizara yake kwa sababu ndiyo mnaoshughulika na kutathmini. Lakini pia mna jukumu la kuhakikisha kwamba sisi raia wa Tanzania sababu ya *investors* hatuwezi kuwa watu ambao hatuna ardhi yaani hatukuwakaribisha *investors* kuja ndani ya nchi yetu kusudi watufanye *land less*.

Mimi naamini kwamba tuliwakaribisha *investors* kuja ndani ya nchi yetu watusaidie ili tupate maendeleo, tuneemeke lakini siyo kwamba tuteseke na tuwe na mateso kwa sababu ya kuwaleta *investors*. Kwa hiyo, niliona nitumie nafasi hiyo kutoa kilio cha wananchi wa sehemu hiyo ya Nyamongo kwamba

watendewe haki kwa sababu kwa kiwango kikubwa mimi nahesabu kwamba wako katika manyanyaso makubwa wakati umeshafukuzwa nyumbani kwako na hujui kesho utalala wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumaliza kwa kusisitiza tena kwamba, Mheshimiwa Waziri naomba uwasilikilize hao watu waliokuja kwa niaba ya wenzao na kama wana haki inayotakiwa, watendewe haki zao ili waweze kulipwa kinachostahili na waonyeshwe kwamba wataishi katika eneo gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na mimi kwa kunipa nafasi asubuhi hii ya leo ili niweze kuchangia machache katika hoja hii ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda nieleze tu kwamba mimi ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, kwa hiyo, taarifa iliyotolewa mbele ya Bunge lako Tukufu na Mwakilishi wa Mwenyekiti, basi na mimi nimeshiriki kuchangia maoni yangu hapo. Ila ninachosema sasa ni kwamba yako machache nitayazungumza na pengine mengine nitayakazia kidogo ambayo yako kwenye Kamati.

Mheshimiwa Spika, napenda nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Naibu Waziri na pia Katibu Mkuu, kwa kazi nzuri sana ambayo wanaifanya katika Wizara hiyo.

Mheshimiwa Gideon Cheyo, ukikutana naye na hata ukizungumza naye, unajua kwamba ni kweli ni mtu ambaye hana utani, ni mtu wa kuchapa kazi. Kwa hiyo, tunapenda kumpongeza sana kwa msimamo wake na uchapaji kazi wake mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema mimi ni Mjumbe wa Kamati hii, lakini ningependa pengine kueleza masikitiko yangu kidogo kwamba Wizara hii haijulikani sana kule Vijijini, Wizara hii inaelekea inaweka mkazo wake mkubwa zaidi kwa maendeleo ya Miji badala ya kule Vijijini. Mimi napenda kuishauri Wizara hii kwamba baadhi ya Vijiji vyetu hivi sasa ndivyo vinavyotegemewa kuwa Miji. Kwa hali hiyo, ni vizuri Wizara ipeleke jitihada zake kule chini Vijijini ili wajue ni namna gani wanaweza kupanga Miji yao midogo, Vijiji vyao, hivi watapataje hata ramani za ujenzi wa nyumba bora na hizi tafiti ambazo zimefanyika za ujenzi nafuu na rahisi, zinafikaje kule Vijijini?

Kwa hiyo, hayo ni mambo ambayo ningependa Wizara hii itueleze ni namna gani itasogea karibu na maendeleo ya Vijiji badala ya kupima tu vile Vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ninalotaka kuzungumzia ni kwamba, Vijiji vinavyopimwa hivi sasa, tutamaliza lini kazi hiyo ya kuvipima? Maana kama tunavyojua Vijiji vikiwa na hati ni rahisi sana kushiriki katika maendeleo mbalimbali na hata katika mikopo mikubwa ya Benki. Ni lini tunatarajia ya kwamba nchi nzima Vijiji vyetu vitakuwa vimepimwa na vimepewa hati?

Mheshimiwa Spika, lakini lingine pengine tuelimishwe kwamba hivyo Vijiji ambavyo vimeishapimwa tayari, mipaka yao kweli inajulikana na ramani zipo maana mimi kule ninapoishi ninajua baadhi ya Vijiji vyangu lakini mwisho wa mipaka yake rasmi nimetafuta sikuipata. Ninaomba ufafanuzi uwekwe wazi ili mipaka ya Vijiji ambavyo tayari vimeishapimwa ifahamike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nizungumzie sasa suala la viwanja Mijini. Sisi ni wawakilishi wa wananchi na tunapopita Mijini na hata Vijijini tunaulizwa maswali mengi na pengine ni kazi yetu sasa kuiuliza maswali hayo Serikali iweze kujibu ili wananchi waelewe. Yako maswali machache kwa mfano, uko upimaji wa viwanja na hata maeneo ya Miji yenye viwanja vile ambavyo vinapewa hati ya miaka 33 na vile ambavyo vina hati ya miaka 99.

Sasa watu wanauliza, vigezo hasa vya kunipa mimi miaka 33 ninayekaa Temeke, Buguruni, Manzese na yule anayekaa *Oysterbay*, Masaki na kuendelea akapewa miaka 99, vigezo hasa ni nini? Tunataka mtufahamishe na huko *Oysterbay* na kwingineko kule baharini wanakaa viongozi waliochaguliwa

na watu, sasa maana yake ni kwamba viongozi hawa sasa wamekuwa *citizen number one* na wale wengine ni *citizen number two or what?* Tupeni maelezo wananchi waelewe haya kwa nini viwanja vingine vya wazalendo wanapewa miaka 33 na vingine miaka 99. Wageni wote, wawekezaji watakaokuja wakinunua mashamba, wakipewa viwanda na pia wakipewa maeneo ya kujenga lazima itakuwa ni miaka 99, hawa wengine wana matatizo gani. Tunaomba maelezo ili wananchi waelezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, wanauliza, hivi mtu ana shida akanunua nyumba ya ndugu yake mmoja ya miaka 33 au ya miaka 99, amenunua. Baada ya kununua hakufahamu nyumba ile tayari hati yake imemalizika muda wake, je, wakati analipia kodi zote za Serikali huwa ile hati akibadilishiwa inaachwa vile vile ilivyo au anapewa kama ndiyo kwanza anapata kiwanja?

Mheshimiwa Spika, naomba maelezo kwa hayo ili wananchi waweze kujua kwamba muda umekwisha, miaka 33 au miaka 99 anaanza upya ama vipi?

Mheshimiwa Spika, napenda kuendelea kusema kwamba, ninamwomba pia Mheshimiwa Waziri atupe ufafanuzi wa mambo kadhaa hasa yale yanayohusu mipaka ya nchi yetu. Ningependa kuzungumzia mipaka ya ndani ya nchi, mipaka ya Kata, Tarafa, Majimbo, Wilaya, Mikoa na kadhalika. Ni muda kidogo sasa kumekuwa na migogoro mingi sana katika mipaka hii, hivi kumeharibika nini?

Mheshimiwa Spika, tumefika mahala watu wanaanza kuuana kwa ajili ya kugombea mipaka na pia tumefika mahala chuki inazidi kuenea kwa ajili ya kugombea mipaka, lakini tangu Waheshimiwa Wabunge wameuliza maswali ndani ya Bunge kuhusiana na mambo haya, majibu yanayotolewa ni kama rahisi tu, kwamba bwana hakuna tatizo la mpaka kuna *GN* namba fulani.

Mheshimiwa Spika, hivi kwa nini Serikali inapenda kutoa majibu rahisi ya namna hiyo? Mahala ambapo Mtanzania anapoteza maisha yake kwa sababu ya kugombea mpaka tu na kwa nini agombea mpaka leo na siyo jana?

Mimi katika suala hili naiomba Serikali nzima na wala siyo Wizara hii tu, ilishughulikie kwa haraka kabisa suala hili, Watanzania wasishikane mashati kwa sababu ya mipaka ya ndani, Kata, Tarafa na kadhalika kwani kumetokea nini?

Mheshimiwa Spika, ni lazima hatua za Kisheria zichukuliwe na pia ni lazima hatua za kisiasa zichukuliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani kuna kasoro, haiwezekani watu jana walikuwa ndugu leo wanagombea mipaka, wanauana, hivi maana yake nini? Mimi sielewi, lakini nina hakika kuna kasoro kubwa ambayo imetokea hapa, watu wanaanza kuonana wale si wetu na sisi si wao, watu wanaanza kuonana kwamba wale ni kabila lingine na hawa ni kabila lingine.

Sasa mambo ya namna hii kwa kweli tusiyaendekeze yatatuharibia nchi, tutatoka kwenye nchi ya amani, utulivu na mshikamano, twende kwenye nchi ambayo hatuielewi kabisa. Chama cha Mapinduzi ukizungumza jina hilo, ni chama cha amani, chama cha upendo, chama cha mshikamano na chama cha maendeleo. Sasa kama watu wake wanaanza kushikana mashati kwa ajili mipaka tutakwenda kueleza nini?

Mimi naomba hili Serikali ilifanyie kazi kwa nguvu zote na limalizike mara moja. *Regardless* ya kauli ya sijui *GN* ngapi lifanyiwe kazi ya Kisheria na pia kazi ya kisiasa maana sisi tumeletwa hapa kwa sababu ya siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nizungumzie lingine ambalo pengine haliko moja kwa moja chini ya Wizara hii lakini linaigusa pia, ni suala la nyumba. Kwanza, napenda kwa niaba ya wenzangu na wananchi wa Wilaya yangu nitoe ombi maalum kwamba, zile nyumba za Serikali ambazo zinauzwa hasa pale kwenye Hospitali yetu ya Wilaya, tafadhali sana ninaomba Serikali isitishie mpango huo.

Mheshimiwa Spika, zile nyumba naomba Serikali iikabidhi Halmashauri yetu ya Wilaya, sisi watu wa Lushoto hatuna ardhi ya kutosha, ukiishatoa zile nyumba chache ambazo zinaizunguka ile hospitali



pale, inakuwa umeuza pamoja na ardhi na upanuzi wa hospitali ile na hata ujenzi wa nyumba nyingine za Madaktari watakaokuja hazitapatikana. Ninapenda kuiomba Serikali kwamba tafadhali, isifanye jambo hili kwa kufunika nchi nzima kama blanketi, sisi tuna shida ya msingi. Naomba suala hilo liangaliwe upya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini pia hata ugawaji wenyewe wa nyumba zile namna ya kuziua, kwa kweli haukuwa wa halali, mimi nadhani Serikali imefanya makosa. Sasa si vibaya Serikali ikifanya makosa ikajisahihisha, kuna utaratibu huo. Mmetuambia mara nyingi kuna maeneo *prime* hayajauzwa nyumba lakini tunajua hata *Oysterbay* nyumba zimeuzwa, tunajua. Hivi wenzenu watakaokuja baada ya ninyi watakaa wapi? Maana yake kuna maeneo yanayochaguliwa maalum kwa ajili ya viongozi, dunia nzima mambo haya yapo na nyumba zinajengwa, sasa wale wanaokuja wakati ninyi hampo, wao watakaa wapi?

Mimi nafikiri uamuzi ule ulikuwa wa haraka sana, pengine muufikirie tena, nyumba zile zirudishwe Serikalini, mtu anayetaka apewe eneo akajenge nyumba mahala pengine. Hili ni la muhimu sana, Serikali hii imefanya kazi kubwa sana, mambo mengi mazuri imefanya na pia maendeleo mazito imeyafanya lakini kama haitaangalia katika suala hili la uuzaji wa nyumba hizi za Serikali, kuuziana wenyewe kwa wenyewe, kwa kweli matokeo yake yatakuwa ni mabaya sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kuiomba Serikali ifikirie upya juu ya mpango wake huu wa kuendelea kuuza nyumba hizi za Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo napenda nizungumzie kidogo juu ya suala la rushwa. Suala la rushwa ni gumu, kusema kweli rushwa haiwezi kumalizika mara moja na hata kwenye vitabu vya misafu miaka mingi tu huko nyuma iliyopita kulikuwa na rushwa. Lakini katika Wizara hii ninayoizungumzia Mheshimiwa Gideon Cheyo na mwenzake Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Tatu Ntimizi na viongozi wengine akiwemo Katibu Mkuu, ni dhahiri wamepigana na rushwa waziwazi, unaona.

Kwa hiyo, mimi napenda Mheshimiwa Waziri yeyote akisimama tuondoe mashaka kwamba huyu kweli yuko mstari wa mbele katika kupambana na rushwa. Lakini yako majibu tunayopewa siku zote hayapendezi na hayatajaribu kusaidia kuondoa rushwa, kwamba jamani tuna mashaka pale kuna matatizo, wanasema lete ushahidi, jamani pale tunawaambieni iko rushwa, wanasema lete ushahidi.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza kaka yangu, Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya, kama yeye ameweza kufanya yake aliyotambia juu. Lakini si wote tutakaoweza kuyafanya hayo, kuna vyombo vya Serikali, Serikali ni kubwa, Serikali ina macho mengi na pia Serikali inafahamu kila kitu, kwa hiyo waache kutusingizia kwa kuleta ushindi. Tukisema kuna rushwa pale, wafanye kazi ya kupambana na hiyo rushwa kama ndugu yangu Mheshimiwa Gideon Cheyo, anavyofanya katika Wizara yake, Wizara ile sasa hivi ni Wizara safi, kazi zinakwenda haraka kama zilivyopangwa, hati sasa pale haimalizi hata wiki moja, mnapata hati. Hii ni kazi ya kusimamia na kupambana na tabia hii mbaya kabisa ya rushwa ya kuwakosesha haki maskini ambao hawana chao. Kwa kweli lazima hili ifanyike. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, viongozi wetu wasiendeleo kutuambia leta ushahidi, ndiyo maana tumekubali wenzetu wawe mstari wa mbele hapo. Tukiwapa taarifa ya mambo machafu, mambo mabovu, wakimbie kushughulika kutafuta ukweli ulipo siyo kurudi nyuma tena na kutuambia mmefanya makosa bwana, hapa hakuna chochote, sijui lete ushahidi, ushahidi kweli, kweli ushahidi mimi nitaupata wa kutosheleza? Naweza kupata ushahidi kiasi lakini ushahidi wa kutosheleza kuna vyombo vya usalama pale kazi yao ni hiyo ya kuingia mpaka uvunguni, mimi niweze kulieleza hilo, haiwezekani.

Kwa hiyo, napenda kuiomba Serikali na viongozi Waheshimiwa Mawaziri wote hapo mbele kwamba, wasikwepe wajibu wao, tuendeleo kushirikiana kupambana na rushwa hatimaye tutaipunguza sana kiasi kwamba haitaweza kuleta madhara kwa watu wetu. Kule kwetu Mlalo, Mtae na pia Mnazi ni matatizo, rushwa ipo, kwenye Mahakama za Mwanzo rushwa ipo na pia kwenye Vijiji rushwa ipo. Walituambia mwaka fulani leteni majina, tumeandika majina mara tatu hakuna jibu wala hakuna lolote lililofanyika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, safari moja nikaja hapa Bungeni nikamsifu Hakimu wangu mmoja wa Mahakama ya Mwanzo kwamba amefanya kazi nzuri sana na mmoja wa Mahakama ya Wilaya, Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, Mheshimiwa Harith B. Mwapachu, ndugu yangu akaniandikia barua kwamba hongera sana. Akasema, wewe bwana ni mkweli, kumbe yakifanyika mazuri unasema, nikwamwambia nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, nimetoka hapa nimerudi nyumbani, Hakimu yule wa Mahakama ya Mwanzo niliyemsifu alihamishwa nje ya Wilaya mara moja, yule mla rushwa kupita kiasi wakati huo huo ameongezewa na mipaka Tarafa mbili. Mimi niliyesimama hapa, nikaja nikamwambia mwenzangu, ndugu yangu, Mheshimiwa Harith B. Mwapachu, kaka yangu kumetokea nini? Akasema bwana mambo magumu haya! Sasa mambo magumu haya tufanyeje jamani?

Tunaomba wote tuchangamke tupambane na rushwa ya wazi. Nimemsifu mtu, nafika nyumbani nakuta amehamishwa, siku hizi simsifu Hakimu yeyote wala mtu yeyote, nitakunong'oneza tu kaka yangu, Mheshimiwa Harith B. Mwapachu kwamba bwana huyu anafanya kazi nzuri, nikisimama hapa kusema kweli watafukuzwa wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia haya machache. Ahsante sana na naunga hoja mkono. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kabla Mheshimiwa Dr. Suleiman Juma Omar, hujaanza kuchangia, namwomba Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Anne Makinda, anipokee kazi ya kuongoza Bunge. *(Makofi)*

*Hapa Mwenyekiti(Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**MHE. DR. SULEIMAN JUMA OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia mawili, matatu katika Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naweza kusema ya kwamba ni Mjumbe wa Kamati hii na nimechangia katika haya yaliyoelezwa na Kamati yangu baada ya Mheshimiwa Waziri kuzungumza au kuwasilisha hotuba yake. Kwa hiyo, kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati hii kabla sijaenda mbali, napenda kusema kwamba naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, mimi nina oni langu moja nalo ni kwamba, jina la Wizara hii badala ya kusema Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi iwe Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi yaani iwe *double a* kwa sababu kutokana na neno kukaa haiwi “a” moja inakuwa *double a*. Kwa hiyo, naomba ikubalike jina hilo liongezwe “a” moja hapo iwe makaazi, kiswahili hatusemi makazi, ni makaazi. *(Makofi)*

Tatu, ni kwamba nchi nyingi zinaingia vitani kutokana na matatizo ya mipaka. Nadhani tumeona hapa kunako miaka ya 1960 ilikuwa karibu Tanzania na Malawi kupigana na pia miaka ya 1970 au 1980 Uganda na Tanzania zimepigana na nchi nyingine nyingi zinapigana, zinaingia kwenye vita kutokana na mipaka. Kwa hiyo, ni kwamba jambo hili la mipaka si jambo la maskhara. Juzi tu kama miezi miwili au mitatu hata kule kwetu Zanzibar mipaka ya Vijiji imefikia hadi watu kukatiana mazao na kucheana nyumba kutokana na mipaka tu ya Vijiji.

Kwa hiyo, suala la mipaka naomba Wizara ilichukulie kuwa ni suala muhimu sana, isidharau. Hata Somalia na Ethiopia walipigana kutokana na mipaka, mipaka ni kitu muhimu sana iwe ya Kimataifa au ndani ya nchi. Kwa hiyo, naomba Wizara mambo ya mipaka isiseme tu Halmashauri au vijiji vyenyeve vinaweza kupanga lazima iangalie kama mambo yanakwenda sawa na mipaka lazima iwe ya kudumu sio mawe ya kubiringishwa yanapelekwa kule mpaka una-*change*. Nakumbuka tangu miaka ya 1960 mpaka wa Malawi na Tanzania mpaka sasa hivi ni tatizo ilifikia mpaka tulitaka kupigana na Malawi lakini mpaka leo haujatatuliwa bado. Kwa hiyo, suala la mipaka ni jambo muhimu sana, Wizara tafadhali isidharau ilichukulie hatua madhubuti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nikumbushe hivi karibuni tulikuwa na matatizo ya mpaka baina ya Kenya na Zanzibar. Ramani ya zamani ipo lakini Wakenya wakataka kusogeza mpaka hadi kwetu. Nadhani suala hilo Wizara inalishughulikia na naomba ilitatue vilivyo mpaka wa Kenya na Zanzibar hasa kupitia kwenye maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni kuhusu mipango miji, hata nilipokuwa kwenye Kamati nililizungumza. Kamati imetoa maoni yake kwamba, Wizara sasa inapopanga miji lazima ipange maeneo ya kuegesha magari, viwanja vya michezo na *recreation park*. Kwa sababu leo Dar es Salaam ukipita mchana kama saa sita au jioni, njia za mjini huwezi kupita linapita gari moja kwa sababu magari yame-*park* barabarani na hakuna hatua yoyote inayochukuliwa kwa sababu hakuna *parks*, hoteli hazina *parks* na *recreation parks* sijui kama tunazo, *national stadium* tunayo moja hata kukiwa na mechi nyingi hapa labda moja tuipeleke Mwanza nyingine tuiache Dar es Salaam kwa sababu hatuna viwanja vya michezo. Kwa hiyo, nasisitiza kwamba, mipango miji na hasa kule Wilayani lazima mambo kama haya yapelekwe kwa sababu michezo haiko mijini tu hata Wilayani, Vijiji, mashuleni michezo ipo. Kwa hiyo, nafasi za michezo, za *recreation parks* ni muhimu sana katika upangaji miji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizingumzie kuhusu utafiti wa nyumba bora na vifaa vya ujenzi. Utafiti huu ni muhimu sana na kujenga nyumba bora na madhubuti ni kitu muhimu sana. Kwanza ni *very costly* kwa sababu nyumba ikiweza kuishi miaka 20 na mwingine akajenga nyumba ikaishi miaka 30 ni gharama. Kwa hiyo, atakayeweza kujenga nyumba itakayoweza kuishi miaka 30 au 100, huyo ni mjenzi mzuri na vifaa vyake ni vizuri. Vile vile na wajenzi wawe wazuri sio vifaa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba, utafiti huu wa vifaa vya ujenzi uendelee lakini kwanza tuna vituo vingi vya kufyatulia matofali na ubora wa matofali hauwi-*tested*, watu wananunua tu matofali, mchanganyiko, mchanga kiasi gani, saruji kiasi gani, hauna kipimo watu wanafanya biashara. Nashauri wenye vituo vile vya kufyatulia matofali, lazima Wizara ifanye mpango wa kuvindikisha na wapewe *formula* hii ya kufyatua matofali madhubuti. Lazima vituo vile visajiliwe na wapewe utafiti huu uliofanyika wa kutengeneza matofali bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri kwamba, hawa wajenzi nao wajulikane. Serikali ina mpango wa kuandikisha *contractors* au *engineers*. Sawa hawa wanajenga lakini na hawa wajenzi wadogo wadogo nao wanajenga. Kwa hiyo, itakuwa ni vizuri na hawa wajenzi wadogo wadogo ikiwezekana hata kama Kiwilaya waandikishwe na wao wapewe ujuzi huu namna ya kuchanganya saruji na mchanga unaounganisha tofali na tofali ile nayo ina *formula* yake ya kuchanganya. Kwa hiyo, wenye vituo vya kutengeneza matofali wasajiliwe, wapewe ujuzi huu na wale mafundi wale waandikishwe. Kwa mfano, hata madreva wanaandikishwa na wanakuwa na leseni, kwa nini hawa wasiwe na leseni kwa sababu wanachukua *life* ya watu wanajenga nyumba, nyumba zinaweza kuanguka.

Tunakumbuka miaka michache iliyopita kuna ghorofa moja kule Korea ya Kusini lilianguka likaua watu chungu nzima kutokana na ujenzi mbovu. Kwa hiyo, nashauri nao hawa wapewe utaalum huu ili kuwajengea nyumba madhubuti, ziishi kwa muda mrefu zaidi na zisibomoke hovy hovy kwa sababu ni maisha ya watu na watu wanatumia gharama kubwa kujenga nyumba zao. Kwa hiyo, nao hawa wasidharauliwe wapewe ujuzi huu, waandikishwe na wawe na usajili, mimi mjenzi namba yangu ni hii naweza kukujengea nyumba yako kiasi fulani, kwa hiyo, unajua mjenzi wangu ana ujuzi na amesajiliwa. Nashauri Wizara ifikirie suala hilo na ilifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetembelea Wizara na kuona nyumba zile ambazo kuna mitambo mingi ya uchapishaji, mambo ya *computer*, kuweka kumbukumbu za ramani, usajili. Nyumba ile kama ilivyosema Kamati, ni nyumba ya zamani, nakumbuka kuna mashine moja tumeonyesha nadhani ilitumiwa tangu Vita ya Kwanza na Ujerumani kuchorea ramani ya vita mpaka leo mashine ile inakwenda. Kwanza nawasifu sana watu wa Wizara kwamba, mashine ile mpaka leo inafanya kazi. Lakini kusifu hivyo haina maana kwamba waachiwe wafanye nalo shughuli. Ni vizuri Wizara ikaanza kupewa Bajeti ili mitambo yake iwe ya kisasa, watu hawa waweze kufanya kazi kwa ufanisi mzuri zaidi. Tunasifu wanafanya kazi vizuri lakini mashine nyingi zimekuwa za zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ofisi zile karibu na Pwani na nyingine alizojenga Mjerumani, zinaanza kubomoka zimeshazeeka, ni vizuri ama zikakarabatiwa au wakapewa sehemu yao binafsi kwa

sababu wana kumbukumbu muhimu sana kwa nchi nzima wakajenga ofisi zao na mitambo mizuri ili twende na mambo ya kisasa. Kusema kweli ni shughuli nzuri lakini mitambo mingine ni ya zamani, nyumba yenyewe inavunja moyo. Ni vizuri Serikali nadhani inanisikia, kama Waziri Mkuu hayupo, lakini mwakilishi wake yupo, nasifia kwamba Wizara hii inafanya kazi nzuri na kitengo kile kipewe kipaumbele angalau mwakani wawe na Bajeti ya kukarabati au ya kujenga ofisi mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye mradi wa nyumba wa *National Housing* zinazojengwa sasa. Ni jambo zuri sana kwa sababu watu wana matatizo ya nyumba na miji yetu yote nadhani *birth rate* yetu imeongezeka, watu tunaendelea kuzaa, watu watahitaji nyumba. Kwa hiyo, ni vizuri mradi huu wa ujenzi wa nyumba ukaendelea. Lakini labda *National Housing* ianze kufikiria nafasi ya kujenga nyumba moja moja kama tulivyoona kule Boko, wafikirie nyumba za ghorofa kwa sababu kila ukijenga nafasi kama ile ardhi nayo inakwenda tutasema Dar es Salaam lakini kusema kweli ni *almost* karibu na Bagamoyo. Kwa hiyo, mfanyakazi akikaa pale kama ni Mkurugenzi au nani kanunua nyumba kule, *transport* kutoka Dar es Salaam mpaka kufika kule kumleta ofisini na kumrudisha na *Bagamoyo Road* ile iko *very busy* ni *very costly*. Nadhani itakuwa ni vizuri kwa baadhi ya sehemu *National Housing* wakafiria kujenga maghorofa kama walivyojenga hapa Dar es Salaam ili kupunguza nafasi ya ardhi na umbali wa watu kwenda hasa kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia *National Housing*, ipitie Sera yake vizuri zaidi kwenye ukodishaji na upangaji wa nyumba. Nyumba za Dar es Salaam hasa zile za mjini, ukitazama wapangaji wake wengi wao sio watu wenye shida ya nyumba na lengo la nyumba zile ilikuwa ni kuwapa watu wenye shida ya nyumba wapate nyumba za kukaa. Mara nyingi Maafisa wa Serikali kutoka sehemu mbalimbali za Mikoa wanaletwa Dar es Salaam wanapata shida ya nyumba, lakini nyumba zile zilizokodishwa sasa hivi waliomo sasa hivi hawana shida ya nyumba, nyumba wanazo wamekodisha lakini wao wanapanga pale wale wenye shida ya nyumba wanakuwa hawazipati. Utakuta *National Housing* mpangaji waliyempangisha baada ya miaka mitano pengine wameshapishana mara sita, siye kabisa yule wa mwanzo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sera ya upangishaji hasa kwa nyumba kama zile waifikirie upya kwa sababu kuachiana nafasi kama vile sio vizuri. Kuna Maafisa wa Serikali wanakaa mbali sana ametoka Mkoani amepata uhamisho wa kuja Dar es Salaam anakaa Sinza na sehemu nyingine inasababisha kuchelewa kufika kazini. Nyumba zile ingewezekana kupangishwa yeye lakini waliopangishwa sasa hivi wana nyumba zao wamezipangisha wanapata kodi, wale wenye shida ya nyumba wengi wao sio waliopangishwa kwenye nyumba zile. Kwa hiyo, naomba Wizara ipitie tena mpango huu wa ukodishaji nyumba hasa zile za mjini kwa sababu wakodishaji wao wa zamani sio kabisa waliopo sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, naomba Wizara izifahamishe Halmashauri na watu wote wanaohusika na kugawa au kuuza ardhi hasa Wilayani au vijijini, inasemekana kuna wageni wengi sasa ambao sio Watanzania wanauziwa ardhi, jambo hili hulikuti katika nchi nyingine. Ukienda Kenya tu hapa, wewe Mtanzania kununua ardhi au nyumba haiwezekani pana kazi nzito na kuna watu wanasema bwana Kenya hupati labda kwenu tu huku ndio sisi tunanunua nyumba na ardhi. Kuna Waganda, Wakenya, Warwanda, wananunua ardhi hii baadaye itakuja kutuletea matatizo. Naomba Wizara izifahamishe Halmashauri au watu wanaohusika na kutoa ardhi vijijini au Wilayani kwamba, Sera ya Ardhi ni lazima waitazame upya na waelewe kwa sababu kumuuzia mgeni ardhi sio jambo la kawaida wasije kutuletea matatizo baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naunga mkono hoja na nashukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia asubuhi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi kubwa sana kwa Wizara ya Ardhi, kwa kazi kubwa inayoifanya. Kazi hii inaonyesha jinsi Sera za CCM zinavyofanya kazi na inaonyesha jinsi Serikali ya CCM ilivyo sikivu kwa vilio vya wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka mingi imepita kila ikija Wizara hii, neno kubwa tulilokuwa nalo ni pimeni viwanja, pimeni viwanja, kwa kweli Wizara imekuja na mradi wake huu ambao umetushangaza hata sisi wananchi wenyewe jinsi walivyopanga vizuri na jinsi *computer* zinavyofanya kazi vizuri na tunapata hati kwa wakati muafaka, nawapongeza sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitalirudia hilo la viwanja lakini kwanza niendeleo kuwapongeza na kuzungumzia mambo mengine kwa kuwa naamini wananchi wa Dar es Salaam, wakisikia nimesimama kwa mambo ya viwanja wanataka nizungumzie pia viwanja 20,000. (Makofi)

Naomba nianze kwa kuzungumzia *National Housing*. Serikali imeanzisha utaratibu wa kuuza nyumba ingawa utaratibu ule una hitilafu hapa na pale lakini ni mwanzo mzuri. Wananchi wengi hasa wa Dar es Salaam wanajiuliza sasa nyumba zile kubwa zimeuzwa ziko maeneo mazuri sisi tuko kwenye vieneo vidogo vidogo kwenye *quarters* za Ilala, Magomeni, Temeke lakini tunauziwa. Kwa kweli wanafikiri na sisi wanasiasa wao tunawafikiriaje? Kuna, *quarter* zimeisha kabisa, mnaonaje kama Serikali haikutoa bure sasa? Wananchi wamekaa katika *quarter* zile zaidi ya miaka ya 30 -40 wamejukuu na vilembwe wanavyo mle mle lakini *quarter* zile zimekuwa hazipati huduma yoyote. Wao wenyewe wamebadilisha vigae, wametengeneza *quarter* zenyewe, wamechimba vyoo vipya wamezihudumia sana *quarter* hizo na hazipo Dar es Salaam tu ziko katika kila Makao Makuu ya Mikoa, ambazo tumezirithi ziko nyakanyaka kweli, zile bado tunawauzia wananchi? Naishauri Serikali tufanye kama alivyofanya Mzee Mandela, alipotoka jela zile nyumba ndogo ndogo zilizopo Soweto na sehemu nyingine zinazofanana na Soweto aliwapa bure kwa sababu zile kodi ambazo wamelipa miaka yote na thamani ya nyumba zile wanazokaa kwa kweli ni kuzirudisha na kuwapa wananchi bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia kuhusu nyumba kubwa za *National Housing*. Wakati sasa umefika na hizi nyumba nyingine ziuzwe kwa sababu wale ambao wanakaa katika zile nyumba hawatahama hata siku moja. Kwa sababu tatizo la nyumba bado ni kubwa *National Housing* itakapouza nyumba zile itakuwa na uwezo wa kujenga nyumba nyingine, kama Serikali inavyofanya imeuza nyumba imepata uwezo wa kujenga nyumba basi zile nyumba ziuzwe wale Wahindi hawatahama pale katikati ya miji lakini wana uwezo wa kununua nyumba zile ili *National Housing* iweze kujenga *estate* nyingine na kutoa *service* muhimu ya upangishaji nyumba kwa wananchi wengine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia wananchi tunatazama bei gani nyumba hizo za *National Housing* zitauzwa, pamoja na kwamba tunajua zipo nyumba nyingi za *National Housing* zimekuwa zikiuzwa kinyemela bila wengine kujua. Tunaambiwa tu mimi hii nyumba nilikwishanunua ingawa tunajua nyumba za *National Housing* zile kubwa zilikuwa haziuzwi, basi Serikali ijijue kwamba imeshafungua *Pandora's Box*. Wale ambao wako katika nyumba za *National Housing* wanategemea siku watakapouziwa wauziwe kwa bei nafuu. Naomba *National Housing* ifikirie suala hilo, iuze nyumba ijenge nyumba nyingine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudi kwenye viwanja 20,000. Naomba Waheshimiwa Wabunge, walione jambo la viwanja 20,000 vinavyopimwa Dar es Salaam sio la watu wa Dar es Salaam tu ni la wananchi wote, kwa kuwa utaratibu huu umeanza Dar es Salaam kama *pilot project*, ukitoka pale utaenda na Mikoa mingine. Yale yanayotendeka Dar es Salaam tujue kwamba katika Mikoa mingine yatawafikia. Kwa mfano, Dar es Salaam wenye mashamba pembezoni mwa mji, mashamba yao yamepimwa viwanja, naamini pia siku moja utaratibu ule utafika Kilimanjaro, Arusha, Singida na Mwanza. Kule Kilimanjaro kuna vihamba, Serikali ikienda kupima kiwanja kwenye kihamba kilichokuwa karibu na mji uambiwe ondoka unalipwa fidia kwa migomba yako ile halafu ukishalipwa fidia kama shilingi milioni mbili uje ununue kiwanja kwa shilingi laki saba au shilingi milioni mbili, unakumbuka kwamba katika kile kihamba ndizi ulikuwa ukila kila mwaka sasa unakwenda kuanza maisha upya. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tulichukulie hivyo. (Makofi)

Naishauri Serikali isiwanyang'anye wananchi wa Dar es Salaam mashamba yao kwa kuwaambia tunawalipa fidia halafu baadaye ununue kwa kiasi fulani, huo ni unyang'anyi. Haki ni kwamba, napima shamba lako kiwanja kimoja nitakupa, japo kimoja apewe yule mwananchi kama anataka zaidi anunue. Lakini kumwambia ondoka ukitaka nunua ni ngumu jamani! Mtu anapita anaona ule ulikuwa mwembe wangu, pale kulikuwa na makaburi yetu, sisi Waafrika kuna *sentimental feelings* na viwanja hivi pia. Kwa

hiyo, kwa kumwambia mtu wa Dar es Salaam ondoka mji unapanuka hatukatai, tunaomba wapewe japo kiwanja kimoja. Narudia tena wenzetu Zanzibar mashamba yalipochukuliwa ili wapime viwanja katika kila viwanja vitatu kimoja alipewa mwenye shamba. Sasa kwa nini mambo haya yasiwezekane kwa Dar es Salaam kuna nini? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Waambie!

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Matatizo haya jamani narudia tena yatatufikisha pabaya naomba tuanze vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka nilizungumzie ni ushirikishwaji. Niliuza swali hapa nikajibiwa kwamba sisi viongozi wa Dar es Salaam tumeshirikishwa, ni kweli tumeshirikishwa mwisho wakati wa kutaka kugawa viwanja, *at what stage* tumeshirikishwa ndio *important*? Tungeambiwa toka mwanzo itakuwa hivi na hivi, kweli huu ushauri ninaousema mimi sio wangu ni wananchi, tungeweza kushauri vema, pimeni lakini hakikisheni japo kiwanja kimoja tunapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale mashamba ni kweli mengine ya ukoo na hatutaki maneno ya kusema kwamba hatujengi mji wa ukoo, sawa ni ya ukoo, sasa unapowaambia ukoo ule umewalipa fidia shilingi milioni mbili unawaambia wana ukoo kila mtu anunue kiwanja kidogo sana kwa shilingi laki tano, akitaka kubwa la kuweza kuwa na mwembe wake nyuma itakuwa shilingi milioni moja na zaidi. Pengine wale katika ukoo wamezaliwa watu watano kila mtu anunue kiwanja kwa shilingi milioni moja itawezekana? Wagawieni basi angalau kiwanja kimoja katika maeneo yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa majibu yanaweza kutokea yakasema hakuna aliyekutwa na hayo, wapo. Watu sasa hivi wana makaratasi wamelipwa fidia ndio, tena fidia nzuri, lakini ana karatasi kwenda kulipa anashindwa unalipa nini? Umemkuta mtu pale na mwembe au mkorosho wake kila mwaka anapata pengine shilingi laki mbili, laki tatu na uko pale pengine zaidi ya miaka 20 iliyopita, urithi na ile ni *source* ya *income* yake, ujue umechukua kiwanja lakini *at the same time* umemkatia *means* yake ya kuishi. Sasa hivi vyote tumevifikiria tunavyosema aaondoke halafu aje anunue?

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge tulitazame suala hili linakuja huko kwenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumaliza naomba tena Mheshimiwa Waziri atakapojibu asema anawafikiriaje wale wananchi ambao wamechukuliwa mashamba yao. Hiyo ni kwa wale waliochukuliwa mashamba yao lakini na hawa wengine wanaotaka kuboresha maisha yao wawe na nyumba nzuri, wajenge vizuri kwa mpangilio, tatizo ni bei kubwa na wengi kwa kweli wana makaratasi, wengine Wabunge hapa wengi tu viwanja wamepata, kulipia wanashindwa, kwa sababu mishahara yenyewe na uwezo wenyewe kwa ujumla ni mdogo. Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Waziri, amamke kwamba watu waweze kulipa kwa *installment* tatu au nne, sina maana wasilipe kabisa lakini ifikiriwe ile *element* ya kulipa kwa *installment*, wananchi wanavitaka viwanja lakini wanaomba kama ikiwezekana, kwa usikivu ule ule wa Serikali ya CCM wawezeshwe waweze kulipa kidogo kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA O. KIMBAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii. Nasema Wizara hii kwa kweli inafanya kazi nzuri na inawezakana nikasema kwamba Uongozi wake na hasa ukizingatia kwamba kuna akina mama wawili inathibitisha ule uwezo wa wanawake katika kuongoza na katika kufanya kazi wanapopewa kazi, nawapongeza sana. Lakini pia napenda kuwapongeza hawa wanaomsaidia Mheshimiwa Waziri kwenye shughuli zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi jambo kubwa ambalo liko mbele yetu ni suala la upimaji viwanja 20,000 katika Jiji la Dar es Salaam. Napenda kuwapongeza wote walioko kwenye Halmashauri zote bila kusahau kumpongeza msimamizi mkuu wa mradi huu, Ndugu yetu Mgemuzi. Yuko pale Wizarani halali mimi mwenyewe nikiwa shahidi yaani ni watu asubuhi na jioni wanataka kumwona kwa hili na lile lakini huyu baba bado hajachoka kuwahudumia watu hawa. Napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana. Wakati mwingine inabidi akimbie ajifungie mahali lakini sio kujifungia kwenda kulala kujifungia kwenda kuweka mambo sawa. Kazi hii sio ya mchezo huduma ya kuhudumia watu hasa kwenye maisha yao ya ardhi ni jambo zito sana, napenda kuwapongeza wote lakini hasa ambao nimewataja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuungana na wenzangu waliotangulia kitendo hiki ni kizuri lakini kwenye masuala mazima ya bei kwa kweli bei tunayolipia viwanja hivyo ni kubwa mno. Kama walivyosema wenzangu, basi tuone ni njia gani ya kuweza kuwasaidia watu kulipa kwa *installment*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwa mfano mzuri ambao ameutoa Mheshimiwa Sophia Simba, suala la mtu mwenye shamba lake anapofidiwa anafidiwa mimea iliyopo pale siyo thamani ya ardhi, lakini yeye anapokuja kugaiwa ardhi anapewa na thamani ya ardhi. Mimi ninaye mtu ambaye nilimsikia akilalamika kwamba, amenunua shamba mfano kwa shilingi milioni moja, kwa kuwa palikuwa hapana mazao ya kutosha ni michongoma na mnazi mmoja au miwili, matokeo yake amelipwa fidia ya shilingi laki tatu, nne, kiwanja ambacho amepewa anatakiwa kulipia shilingi milioni moja na zaidi. Sasa hapo mtu anajikuta amenunua shamba kwa shilingi milioni moja, amepata fidia ya shilingi laki moja tu, lakini anatakiwa tena kulipia kiwanja anachopewa shilingi milioni moja nyingine. Kwa kweli hii sio haki, tuone ni jinsi gani tunaweza kuwasaidia watu hawa ambao wako pale kwa miaka mingi na mtu shamba lake ilikuwa ndio maisha yake na ni mategemeo yake ya kupata angalau senti kwa kuza mazao ambayo yapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiongelea hilo hilo suala la viwanja, sasa hivi tupo kwenye kulipia mamilioni, muda wa kumiliki ni miaka 33, tunajua unaweza kuomba tena na ukapewa tena lakini mwenye kuomba anaomba, tuliomba viwanja muda mrefu ndio sasa hivi utaratibu mzuri unafanywa wa kuweza kupatiwa viwanja. Sasa ikifika miaka 33 umeshakuwa mzee, kwa mfano, nikijichukulia mimi mwenyewe nina miaka 57, miaka 33 nitakuwa tayari nina miaka 90, kama nitakuwa hai, sasa miaka 90 uniambie tena niwe na uwezo wa kuomba, kwanza akili zenyewe za kuomba tu nitakuwa sina lakini bado nataka niishie pale nilipo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha hivyo, ujenzi tunapewa muda wa miaka mitano tuwe tumeshajenga, ukichukua mkopo utalipia miaka ishirini kwa hiyo tayari miaka 20 unalipia mkopo umebakia na miaka 13 ya Hati Miliki, ukimaliza mkopo nyumba ile haiwezi tena kuwa kama ilivyokuwa wakati unakabidhiwa na huyu mjengaji, utahitaji pengine miaka mitano mingine ya kupata pesa za kuifanyia ukarabati, tayari miaka mitano imeondoka, umebakiwa na miaka mingapi? Sasa ukifikiria hiyo miaka mitano mingine iliyobaki ya kuishi kwenye nyumba ambayo umeigharamia kwa miaka 25 halafu unakuja kuomba tena, naomba Wizara ilifikirie suala hili kama kuna uwezo wa kuwapa watu miaka 99 basi na viwanja hasa hivi vya sasa hivi ambavyo tunalipia hela nyingi visogee basi angalau miaka 66, miaka 33 tungeze na miaka 33 na hao wenzetu wakubwa waongeze hiyo miaka 33 mingine kufanya miaka 99.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema tuongezewe? Kama tuna uhakika mtu akiomba muda wa nyongeza atapewa, hivi kuna sababu gani tungojee kuomba? Tunaomba sasa hivi basi, tunaomba kabisa kuanzia sasa, badala ya miaka 33 mtuogeeze hiyo ambayo mnaweza kutuogeeza. *(Makofi)*

Lingine ambalo napenda kuongelea ni suala la Shirika la Nyumba. Nashukuru Mheshimiwa Waziri, amekiri hapo bado tatizo la rushwa lipo na tunampongeza kwa jitihada yake ya kukomesha rushwa katika Wizara. Sasa tuone na sisi kama wananchi tunaopata huduma za Shirika la Nyumba, ni jinsi gani ya kumsaidia Mheshimiwa Waziri, pamoja na Wizara yake katika kuweza kuondoa rushwa kwenye Shirika la Nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema moja ambalo linawezekana likawa ni tatizo, mbali ya kusema kwamba tusaidie, lakini bado sheria ya rushwa inasema ni mwenye kutoa na kupokea. Sasa hili neno la mwenye kutoa na kupokea nalo lina matatizo yake. Sasa leo mtu akiwa amewajibika kutoa na kwa kweli kuna wakati unawajibika kutoa kwa shida yako, halafu uende tena ukaripoti kwamba nimempa fulani rushwa, wakati sheria inasema na wewe mwenye kutoa pia umu hatiani, sasa hili nalo linakuwa gumu kwa watoaji. Lakini pia linakuwa gumu kwamba hata ukisema ukachukue pesa za Polisi, hizo pesa zenyewe wangapi ambao tumepata elimu ya kutosha kujua zinapatikana vipi. Wenzetu wengine wa Mjini wanaweza kujua lakini wa Vijijini hawawezi kujua na Shirika la Nyumba haliko tu Dar es Salaam liko karibu nchi nzima. Sasa basi tupate elimu ya kuweza kupata hizo hela za Polisi. Lakini pia nafikiri kwamba, kama mtu atakuwa ametoa hela yake mwenyewe ili kuweza kutekelezewa jambo analohitaji kwenye hili shirika ambalo tunakubali kwamba rushwa bado ipo, huyu mtu kumtia hatiani na yeye kwa kuwa ametoa, aangaliwe kwa jicho la huruma kwa sababu tayari ameisaidia Wizara kumkamata mtu ambaye anapokea rushwa.

Lingine ni kuwaomba hawa ndugu zangu wa *National Housing*, kwanza nawapongeza kwa kazi nzuri wanayofanya ya ujenzi wa nyumba ambazo baadaye wanakodisha na zingine wanawauzia wananchi. Sasa mimi ningeomba kuwaombea ndugu zangu wanaoishi mabondeni Dar es Salaam. Hawa watu wamejaribu kuomba kupitia kwa Wabunge wao, kupitia Serikali zao za Halmashauri kwamba, waweze kubaki na wapo tayari kujitolea kutengeneza miundombinu wakisaidiwa na Wizara ili waendeleo kuishi katika maeneo wanayoishi.

Nafikiri hili siyo kwa sababu wanapenda wao kupata shida wanazozipata, tatizo kubwa ni uwezo kwamba, mtu amekwishaanza kujenga kibanda chake cha vyumba viwili, anaishi na watoto wake. Anapoambiwa aondoke aende Ununio kwenda kuanza upya, hapo ndiyo inakuwa shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi ningeomba Wizara kupitia hili Shirika la Nyumba wafanye ule mtindo ambao niliushuhudia kwenye miaka ya 70 pale Mwenge, kile Kijiji au sijui Kitongoji cha Mwenge, ambacho sasa hivi kimeshakuwa ni Mji mkubwa. Ilijengwa misingi ya nyumba halafu kikajengwa chumba kimoja na ukumbi, watu wakauziwa kwa bei nafuu, baadaye ikatumika njia ya kusema watu wanajengeana lakini angalau mtu anatoka anakwenda mahali ambapo anapo pa kujisitiri, ana chumba na ukumbi. Baadaye mwenyewe anaendelea kujenga taratibu. Sasa ningeomba Wizara kupitia hili Shirika, lijaribu kuona ule mpango wa kuweza kufanya mambo kama hayo kutenga hayo maeneo maalum kwa hawa wanaoondoshwa mabondeni Dar es Salaam, lakini pia kuwashauri Shirika la Nyumba kujenga misingi ya nyumba za bei nafuu na kuwamalizia angalau chumba na ukumbi. Halafu wawakopeshe kwa masharti nafuu ili wenyewe wanapokuwa wanajisitiri watakuwa pia wanaendelea kumaliza ile sehemu nyingine ya nyumba ambayo msingi wake umeshajengwa. Kwa hiyo, hili nafikiri lingeweza kuwasaidia hawa wenzetu ambao ni wengi. Tumesikia wakitamkwa hapa zaidi ya shilingi laki mbili, ambao wapo kwenye matatizo ya kuishi mabondeni Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ningependa sana tena sana, kuishukuru Wizara kwa sababu kipindi cha nyuma niliwahi kuongelea suala zima la *National Housing*, juu ya ukodishaji wa nyumba zake. Kuna watu ambao wameishi kwenye nyumba hizi lakini sasa hivi hawapo, lakini bado nyumba zilikuwa zinaendelea kukodiwa na wao na wengine walikuwa wanaendelea kukodisha kwa wenzao au kuzifanya kama ni nyumba tu za kufikia wageni kwa sababu kulikuwa hakuna Mikataba ya muda maalum. Kwa hiyo, watu walikuwa wanaendelea tu kuishi kana kwamba zile nyumba wao wamemiliki kabisa. Sasa nawashukuru kwamba angalau sasa hivi kuna Mikataba, lakini bado kama walivyosema baadhi ya Waheshimiwa waliotangulia kuchangia kwamba, tuiangalie upya. Hawa wateja wa *National Housing* hatukatai kwamba mpangaji naye ana haki zake, lakini pia kuna watoto wetu na vijana wetu ambao sasa hivi ndiyo wanainukia, wanaanza maisha. Analetwa Dar es Salaam anakwenda kukodi nyumba au chumba kwa bei kubwa kuliko ile ya *National Housing*, lakini kuna watu wamekwishakaa kwenye nyumba hizo kwa miaka mingi tu.

Sasa Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kuna mikopo na viwanja vinatolewa, hawa watu kwa nini hawaondoki na wao wakaenda kutafuta huko kujenga. Baadhi ya wapangaji wa *National Housing* wanauwezo, lakini kama alivyosema Mheshimiwa Dr. Sulaiman Juma Omar kwamba, wamejenga majumba yao mazuri, wanayapangisha, wanapata kodi kubwa lakini bado wanaendelea kukaa kwenye nyumba za



*National Housing*, ambazo kwa kweli sasa hivi wao hawastahili kukaa. Naomba tuwasaidie vijana wetu, watumishi wa Serikali na Mashirika ya Umma wanaohamishiwa kwenye Miji mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa tupite kuanza tena kujua nani yupo kwenye nyumba gani na ameishi kwa miaka mingapi na je, huyu kweli hana nyumba yake na kama aliomba kiwanja ili ajenge nyumba ya kuishi nafikiri hati ndiyo zinavyosema. Mama Kimbau nimeomba kiwanja kwa ajili ya kujenga nyumba ya kuishi siyo nyumba ya kukodisha. Sasa kama hiyo sheria ipo na yeye ameomba kiwanja na amejenga nyumba kwa ajili ya kuishi, kwa nini asiende kuishi, aendelee kuishi kwenye *National Housing*. Aende kuishi kwenye nyumba yake aliyojenga na hiyo nyingine wapewe wenzetu ambao bado hawajakuwa na uwezo wa kujenga nyumba zao. Maana lile ni Shirika la Taifa siyo la watu wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo, machache narudia kusema nawapongeza sana Waziri na Watendaji wake wote, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, pamoja na wale wote walioshirikiana naye katika kuondoa tatizo la viwanja Dar es Salaam, juu ya kuwa bado tumeomba kwamba bei iangaliwe ili watu waweze kulipa kwa *installment* na pia hatimiliki ziongezewe muda kwani ujenzi sasa hivi ni mgumu. Kwa hiyo, kumpa mtu miaka 33 kwa kweli bado muda huo unakuwa ni mfupi na hatuna sababu ya kuomba tena, tunaomba kuanzia sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kusema kwamba, naunga mkono hoja mia kwa mia. Nawatakia kazi njema na ushirikiano wa karibu na Waheshimiwa wenzao, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika hoja iliyo mbele yetu. Naomba niungane na wasemaji walionitangulia kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, Mama Ntimizi, kwa hotuba nzuri ambayo imeletwa kwetu kisayansi. Toka tumeanza mkutano huu ni Waziri pekee aliyeweza kumaliza kusoma hotuba kabla ya dakika thelathini. Mimi sishangai kwa sababu ninavyomfahamu Mheshimiwa Cheyo, ni mtu mahiri, mwenye maneno machache, lakini utendaji mzuri na hata akiingia hapa Bungeni huwa hatoki mpaka unapoahirisha kikao. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia salaam za pongezi ziwafikie Watendaji wake Wakuu, Mama Salome na Kamishna Msangi, Wakurugenzi Mgweno, Molell na wengine. Hapo ndiyo ilipo siri ya utendaji, ningependa niwapongeze kwa kazi nzuri ambayo wanafanya ikiwa ni pamoja na kupunguza sana tatizo la rushwa katika Wizara hii ambayo ilikuwa inalalamikiwa sana. Pia mambo yanakwenda haraka zaidi, watu wanapotaka kupata viwanja au hati. Mimi mwenyewe nimeshuhudia, ningependa niwapongeze sana wafanyakazi wote wa Wizara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazungumzo yangu ningependa nimkaribishe Mheshimiwa Waziri katika Jimbo langu la Rungwe Magharibi. Kama wote mnavyojua, tumekumbwa na matetemeko mengi katika miaka ya hivi karibuni Wilayani Rungwe. Mwaka 2002 mwanzoni, Kata tano zinazozunguka ule mlima ziliathirika Kata ya Suma, Katumba, Isongole, Kandete, Kabula, zote zilipata matatizo, nyumba nyingi zilianguka au zilipata mipasuko, shule nyingi ziliathirika, zahanati, majenfo ya Mahakama na nyumba za kuishi watu, familia nyingi zikakosa mahali pa kukaa katika kipindi kile kilichokuwa cha mvua nyingi sana, kwa hiyo, ilikuwa vurugu kubwa sana. Niseme tu tulikuwa na bahati katika matatizo yote hayo tuliweza kumpoteza mtu mmoja tu, ndiye aliyekufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawashukuru wahisani wote waliotusaidia katika maafaa haya ikiwemo Serikali, Mashirika mbalimbali na Balozi mbalimbali. Baada ya hapo tuliletewa Kamati ya Maafa kuja kuchunguza ikihusisha Kitivo cha Jiolojia pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Walifanya utafiti lakini walichotuaambia ni kwamba, matetemeko mahali popote duniani hayatabiriki. Huwezi ukajua tetemeko litakuja lini, litakuwa na ukubwa gani na litatokea sehemu gani na tukaambiwa kwamba hata Japan ambayo ni nchi iliyoendelea na wenyewe wanapata haya maafa ya matetemeko, lakini hawawezi wakatabiri lini watapata tetemeko lingine. Mpaka hapo mtajuliza kwa nini nimelizungumza hili, ni kwa sababu matatizo makubwa tunayoyapata ni nyumba kuanguka na kuangukia watu na wanyama wanaokaa katika hizo nyumba.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipomsikiliza Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 30 kuna suala la utafiti wa nyumba bora, nikaona hapa ni mahali pake nimwombe Waziri kama kuna kitengo cha namna hii afike yale maeneo au hata kwenda kwenye nchi zingine ambazo zinapata matatizo ya matetemeko, akaangalie ni nyumba za namna gani ambazo zinaweza zikatufaa. Mwaka 2002, Shirika la Kidini linaloitwa *CARITAS*, walitujengea nyumba 40 za mbao, tunaziita nyumba za mfano, kuna sementi chini kama kawaida lakini kuta ni za mbao na tumeezekea mabati, tunafikiri nyumba hizo zinaweza zikafaa kwa maana ya kwamba, zinaweza zikahimili matetemeko lakini pia kama zitaanguka athari kwa wananchi na wanyama zitakuwa kidogo. Kwa hiyo, rai yangu ni kwamba, Wizara itusaidie kwa hilo, itume wataalam wake na watupe miongozo, tuelewe tufanye nini ili tujenge nyumba ambazo zinaweza kuhimili matetemeko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, nilitaka kumfahamisha Mheshimiwa Waziri kwamba, tuna mgororo wa ardhi katika Jimbo langu katika Kata inayoitwa Kisondelo, Kijiji cha Bugoba. Eneo linalogombewa lina hekta zaidi ya elfu moja. Serikali ilikuwa imejenga hospitali ya ukoma ambayo imeendelea kwa muda wa miaka mingi na huko nyuma hili eneo lilikuwa chini ya Chifu Kasunga. Sasa wagonjwa wa ukoma wamepungua na kama mnavojua, sera sasa hivi ya kushughulikia wakoma ni kwamba watibiwe katika hospitali za kawaida kama wagonjwa wengine. Kwa hiyo, Serikali ikaamua kuifunga ile hospitali. Sasa Kanisa Katoliki waliomba eneo hilo na Halmashauri ikawapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wananchi wa Bugoba wanalalamika na wanaona hawakutendewa haki kwa sababu kwa sheria ya mwaka 1999, eneo la ardhi ni mali ya Kijiji. Kwa hiyo, wao wanalalamika kwamba hawakushirikishwa wakati eneo hilo wanapewa Kanisa Katoliki. Wanakijiji wengi hawana mahali au maeneo ya kujenga au kulima lakini pia kutokana na mwamko uliopo sasa hivi, walitaka kujenga sekondari katika eneo hilo. Walifanya mawasiliano na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi wa Halmashauri na ikakubalika kwamba, kiasi cha lile eneo wapewe wananchi. Viwanja vikaanza kupimwa, watu wakapewa na wakaanza kupanda migomba na pia waka-*identify* sehemu ya kujenga sekondari, wakakusanya mawe, matofali na wakanunua saruji. Lakini mwezi Aprili, 2002 wakaambiwa wasiendeleo na ujenzi vinginevyo wataletewa Polisi, kwa hiyo, wakaacha. Sasa kumekuwa na mvutano na wananchi wanalalamika na sasa hivi tunajaribu kujenga sekondari katika kila Kata, kuna sekondari kumi ambazo zinajengwa katika Jimbo langu hivi sasa na wao wanaona wanaachwa nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili limefika ofisini kwa Mheshimiwa Waziri, lakini kama nilivyosema, huu mvutano umeanza toka Aprili, 2002 na kumekuwa na uhasama kati ya wanakijiji na Serikali waliyoiweka madarakani wao wenyewe. Kwa hiyo, nilikuwa naomba tu kwamba, tunachohitaji kutoka kwa Mheshimiwa Waziri na Ofisi yake ni uamuzi. Tungependa uamuzi utolewe haraka ili kuepusha mvutano huu au uhasama unaoweza kutokea na pia hawa wananchi waweze kujenga sekondari kwa sababu wameazimia na wapo tayari na wanaona wenzao wanawapita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na hayo ambayo nilitaka nichangie na naishia kwa kumshukuru tena Mheshimiwa Waziri na kama nilivyosema, ni mtu mahiri. Kwa hiyo, nina imani kwamba, haya niliyoyasema atayashughulikia. Naishia kwa kuunga mkono hoja yake kwa asilimia zote mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie kwenye hotuba hii. Kwanza, nitoe shukrani zangu na kwa kweli pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Watendaji wote wa Wizara na taasisi zake, kwa kazi nzuri sana ambayo kwa kweli wanafanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imebadilika sana kwa miaka ya karibuni chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Waziri Cheyo na kwa kweli hata katika mazungumzo yangu sitakuwa na mengi au kuikodolea macho Wizara. Lakini hasa hasa anayetakiwa kukodolewa macho ni Serikali kwa ujumla. Nasema Serikali imechangia sana katika majukumu ya Wizara hii kutokwenda vizuri. Nianze kwa kusema kwamba, katika mipango ya Serikali ya kuondoa umaskini, Sekta hii ya ardhi na nyumba imeachwa kabisa. Inasikitisha sana kwamba hata katika hii *Poverty Reduction Strategic Paper*, hakuna hata mstari mmoja unaoelezea jinsi umaskini utakavyoondolewa kwa njia ya kuboresha makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uboreshaji wa makazi ni njia mojawapo ya kuondoa umaskini wa Tanzania. Lakini hili inaonekana halionekani katika mipango yetu. Mheshimiwa Waziri wa Mipango, ametoa hapa mipango mingi na mizuri ya kuondoa umaskini, lakini hakuna hata mpango wa kujielekeza katika kuboresha nyumba na makazi kwamba ni njia mojawapo ya kuondoa umaskini na hii kwa kweli inasikitisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapokuwa na hati ya nyumba yako utakuwa umeondolewa umaskini kwa kiasi kikubwa sana kwa sababu hati inakuwezesha kupata mikopo na kuweza kujiondolea umaskini kwa njia mbalimbali, lakini vile vile nyumba yako unaweza ukaiboresha zaidi na ukapangisha ukapata mapato kutokana na pango. Hii ni njia mojawapo ya kuondoa umaskini. Lakini vile vile unapokuwa na nyumba ambayo ina hati, mazingira yake yako katika hali nzuri hasa suala la afya ambalo kwa kweli ni njia mojawapo ya kuondoa umaskini, utakuwa umelikabili. Sasa tusizungumzie tu Mijini ili kuondoa umaskini ni upatikanaji wa ajira, kuboresha maji, afya na kadhalika tukasahau suala la nyumba kwamba makazi bora yanaondoa umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeandika kitabu jinsi ambavyo nyumba bora au makazi bora yanaweza kuondoa umaskini. Sijui wangapi wamesoma kile kitabu. Bei yake shilingi 7,000/= tu. Lakini ningependa kwa kweli Serikali ikisome kile kitabu ili ielewe ni namna gani nchi hii inaweza kuondoa umaskini kwa kukazania suala hili la kuboresha nyumba na makazi. Sasa hivi tuna mikakati ambayo Shirika la *UN-HABITAT* limeweka ya kuondoa matatizo haya kwa mfano, kuna *Global Campaign on Urban Governance* na vile vile kuna *Global Campaign for Secure Tenure*. Sisi tumeweka saini kwenye Mikataba hii, lakini huoni mikakati kwenye mipango ya Serikali ni namna gani tutatekeleza masuala haya ya kuhakikisha kwamba, wakazi wa Mijini wanapata *Secure Tenure*, wanapata hati za nyumba zao. Sasa kumbe tumeweka au tumetia saini kwenye Mikataba ile ya nini kama sisi wenyewe tunawapa Wizara shilingi milioni 600 kwenye mipango yao ya maendeleo. Itatufikisha wapi kwenye kampeni hizi ambazo nazizungumzia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa nilizungumzie ni hili suala la kuanzisha vyombo vya kutoa mikopo na juhudi zimefanyika lakini toka mwaka 1995 wengine tulihusika katika kuzungumza sana namna gani tuanzishe vyombo hivi vya kutoa mikopo ya nyumba. Mpaka sasa Mheshimiwa Waziri, amesema mkakati upo, lakini mkakati upo neno hilo au maneno hayo yamekuwa yakizungumzwa karibu miaka kumi sasa. Sasa tufike mahali kweli mambo yaanze. Mimi ningependa kuyashukuru sana Mashirika ya *NSSF* na *PPF*, kwa juhudi wanazofanya, pamoja na *National Housing*, lakini bado juhudi zile hazitoshelezi Watanzania wengi na hasa wa Mjini kupata nyumba kwa njia rahisi. Ndiyo maana sasa tunakuwa na mipango ambayo ni ya kubahatisha tu na hii kwa kweli haiwezi kutuondolea adha hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Nyumba linafanya kazi nzuri lakini mimi nilikuwa nadhani kwamba kuna haja ya shirika hili kuangaliwa upya na kupewa majukumu mengi zaidi na ningependekeza kwa sababu sasa hivi tuna *Building Agency* kwenye Serikali kwenye masuala ya nyumba za Serikali. Lakini kungekuwepo na *agency* nyingine na *National Housing* ingekuwa kwenye nafasi nzuri ya kuweza kuwa *agency* ambayo itakuwa haishughulikii tu masuala ya ujenzi wa nyumba, lakini vile vile na masuala ya ardhi. Kwa hiyo, majukumu mengine yatatoka pale Wizara ikapewa taasisi hii kwa sababu hizi *agency* zinafanya kazi kama *private institution* na wangeweza kufanya kazi nzuri zaidi lakini kwa kupewa nguvu zaidi kwa maana ya uwezo.

Sasa tungekuwa kwa mfano na *National Lands and Housing Development Agency* na *National Housing* ndiyo ikageuzwa ikafanya kazi ile badala ya kazi nyingine hizi kufanywa na Wizara na unajua tena matatizo ya Wizara kufanya mambo haya. Ndiyo maana kwenye Wizara nyingine tumeanzisha *Building Agency* ili kuondoa katika ule mkono wa kawaida wa Serikali ili ufanisi upatikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu *National Housing* sasa hivi kwa kweli sana sana inakusanya kodi. Mimi naamini kwa sera hii ya Serikali ya kuuza nyumba za Serikali, itafika mahali itasema tuze nyumba zile za *National Housing*, zile zilizotaifishwa wauziwe wale wanaozimiliki kwa sababu kuna tofauti gani kama tunauza nyumba za Serikali na wanaouziwa ni wale wale wanaokaa kwenye nyumba zile za *National Housing* vile vile ni wafanyakazi wa nchi hii au ni wananchi wa nchi hii ambao

vile vile wangependa wafaidi matunda ya nchi yao. Kwa hiyo, mimi naamini itafika mahali na zile nyumba tutaziuza, *National Housing* itabaki inafanya nini kama uwezo wake wa kujenga ni mdogo mpaka sasa, basi wangepewa majukumu zaidi ya kutafiti, kuweka mikakati ya kupima viwanja na kuuza viwanja vile vile na kujenga badala ya kuangalia na kukusanya kodi ambayo kwa kweli kama sera hiyo ikipitishwa watakuwa hawana kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwenye suala hili la ukosefu wa viwanja. Tulikuwa na *Master Plan* huko nyuma lakini kwa bahati mbaya sasa hivi *Master Plan* haziwezi kufanya kazi kwa sababu *Master Plan* inatakiwa mpango utangulie watu, yaani Serikali ipime viwanja na ndipo watu waje. Bahati mbaya watu wameingia Mjini bila Serikali kupima na sasa hivi tunakwenda na mpango unaoitwa *Strategic Plan*, ambao unabahatisha tu kwamba, leo nakwenda kupima viwanja 2000, Buyuni - Chanika, kule kwenye Jimbo langu na kadhalika. Sasa mipango hii ya *Strategic Plan* kwa kweli haitatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa lazima tuwe na mikakati ambayo itawawezesha wananchi kuwa na viwanja vyao au nyumba zao zilizopimwa na ningependa nipendekeze kwamba, tuwe na mpango wa *regularization* ya maeneo haya ambayo ni makazi holela kama vile Buguruni, Kiwalani, Vingunguti, Ukonga na Kipawa kwenye Jimbo langu kule. Tu-*regularize* yale maeneo watu wapate hati, tutakuwa kwanza tumewaondolea umaskini kwa kiasi kikubwa. Sasa Mradi wa *Regularization* unahitaji hela nyingi na lazima Serikali ichukue majukumu kabisa sasa ya kutoa pesa za kutosha na si za mkopo kama hizi ambazo Mheshimiwa Mramba, ambaye bahati nzuri yupo hapa na nitasema kuhusu vile viwanja 20,000. Tusimlaumu Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, tumlaumu Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Kwa sababu unapotoa fedha kwa mkopo wa mwaka mmoja unavunja *bond*, sasa tunamlaumu Mheshimiwa Cheyo, wakati yeye ameambiwa shilingi bilioni tisa zile zirudi *within one year*, atafanya nini? Sasa ni nani, ni Serikali ndiyo imeamua kwamba ule ni mkopo. Kama Serikali ingekaa, Waziri wa Fedha akatoa hoja kwamba hizi shilingi bilioni tisa ziende na zirudishwe baada ya miaka mitano wananchi wangeweza kulipa hela kidogo kidogo ambazo Waheshimiwa Wabunge wanapiga kelele hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Mramba, amesema hizi hela nazihitaji mwaka mmoja, nimezikopa na mimi kutoka mahali. Sasa hilo ndilo tatizo la kukopa mahali na kukopa, Serikali iwe na mkakati wa kutafuta fedha za kutosha na kuweka *funds* ambayo kwa kweli ni *revolving* ya muda mrefu siyo mkopo wa mwaka mmoja. Kwa hiyo, mradi huu si wa kuondoa umaskini wa nyumba ndiyo maana matajiri ndiyo wanaweza kununua vile viwanja. Kwa sababu maskini gani atanunua kiwanja cha shilingi laki tano au milioni moja kwa kipindi cha mwezi mmoja au miezi miwili, hakuna. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mradi ule lazima tukubali *as long as* Mheshimiwa Waziri wa Fedha, anatoa mikopo ya kurudishwa kwa mwaka mmoja tukubali kwamba ni mradi wa matajiri na wala siyo mradi wa maskini. Sasa tubadilishe kwa maana ya utaratibu mzima kutoka kwenye mipango yetu na utojaji wa fedha zile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini kabisa kwamba, huu mpango wa *regularization* utatusaidia zaidi badala tu ya kukimbia kule maporini kwa sababu wananchi wanachotaka ni kuwa na hati zao, ukiwapa hati zao watakuwa na raha vile vile na hii *regularization* inaweza kufanyika vile vile mabondeni kama ambavyo nimesema. Mimi naamini kabisa na kwa kweli nitakuja siku moja niwe *proved right* kwamba kuwaondoa wananchi kwenye mabonde hasa Jangwani siyo tena Boko, wameshamia kule, ni wengi sana. Siyo wale karibu na *Morogoro Road* kule mnaowaona, pita bonde lile mpaka Ukonga kule kwangu wananchi wapo kule maelfu kwa maelfu, njia ni kudhibiti mafuriko na mradi kama ule Serikali inaweza kuuwekea mkakati.

Wananchi wenyewe wameshaanza kwa mfano, kuweka mitaro lakini nguvu zao ni kidogo. Mimi nina hakika tukidhibiti mafuriko na miradi hiyo inafanyika duniani mahali pengi tu, gharama yake ni ndogo kuliko gharama ya kuwahamisha wananchi pale. Gharama yake ni ndogo kuliko kuwahamisha watu 200,000 wanaoishi mabondeni Dar es Salaam na tukawafanyia *regularization* pale. Sasa angalia kinachotokea, taasisi zinazofanya biashara kama *TANESCO* wanawapelekea umeme kwa sababu wao wanataka biashara. Kwa hiyo, umeme mnapeleka lakini barabara mnakataa kuwajengea tunafanya nini. Kwa kweli mimi nilikuwa nadhani kwamba hilo lazima lifanyike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho mimi nadhani Wizara ishirikiane na Manispaa zetu hasa za Mkoa wa Dar es Salaam, kuangalia matatizo ya mipaka kwenye Wilaya zetu na kwenye Kata zetu. Kuna migogoro mingi sana pale Dar es Salaam ya mipaka na inaletwa wakati mwingine wananchi kwa wananchi hata wakati mwingine kufikia hatua ya kugombana na kutojua wanakwenda wapi. Sisi kwa mfano, kwenye Wilaya yetu ya Ilala sasa hivi tunasema kwamba, Wilaya ya Kinondoni wametujengea shule. Kuna shule moja ambayo imejengwa na Manispaa ya Kinondoni kwenye eneo ambalo tunaamini ni ndani ya Manispaa ya Ilala na sasa hivi tunashukuru tunaongeza idadi ya shule na tutawaambia kwa herini hii shule mmetujengea na tunawashukuru. Sasa mgogoro kama ule ni vyema uweze kutatuliwa kwa kushirikiana na Manispaa zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa kweli nilitaka nichangie hayo, na hasa nisisitize kwamba, Bajeti ambayo Serikali inaipangia Wizara hii kwa shughuli za maendeleo ni kidogo sana na hatutaweza kufika mahali tukaondoa umaskini wa nyumba kwenye Miji yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka 20 ijayo nusu ya Watanzania watakuwa wanaishi Mijini. Tukiendelea na mipango hii ya kupeleka shilingi milioni 600 kwenye Wizara nyeti kama hii tutashindwa kufikia azma yetu ya kuondoa umaskini kwa mwaka 2025. Kwa sababu uwezo huo hatutakuwa nao na hatutaweza vilevile kushirikiana na Mashirika ya *UN-HABITAT* katika kampeni za kuondoa hali mbaya ya makazi kwenye Miji yetu na kuondoa umaskini kwenye Miji yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, mimi ninaunga mkono hoja hii nikiitaka Serikali iangalie upya Bajeti inayopelekea Wizara hii. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. MONICA N. MBEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Kwanza kabisa, naomba kusema naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba niipongeze Wizara hii kwa kazi nzuri sana ambayo Mheshimiwa Waziri na msaidizi wake Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na wafanyakazi wote wamekuwa wakiifanya. Kwa hakika sasa hivi kazi mbalimbali zilizofanywa na Wizara hii ni tofauti kabisa na ilivyokuwa huko nyuma. Mambo mengi sasa hivi yanakwenda kwa upesi na kwa hakika ukifika Wizarani unakuta huduma zinakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niipongeze Wizara pia kwa kuchukua hatua ya kuweza kuanzisha utaratibu wa kompyuta kwa ajili ya kuweka kumbukumbu za viwanja. Kwa sababu kwa namna hii itasaidia sana hasa pale ambapo palikuwa na tatizo la kuweza kubadilisha Hatimiliki kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mtu mwingine, kwa sababu kama huna taarifa kamili basi inakuwa ni vigumu sana kuweza kujua hiki kiwanja au nyumba ilikuwa ni sahihi ya mtu fulani kwa maana hiyo inakwenda kwa mtu mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine upo katika ukurasa wa 27 kwa upande wa Shirika la Nyumba. Mheshimiwa Waziri anajua kabisa kwamba, nataka kuchangia nini. Lakini naomba niseme kwa sababu ni masuala ya wananchi wangu katika Manispaa ya Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika ukurasa wa 27 anasema kwamba: “Hadi kufikia mwezi Machi, 2003 malimbikizo ya kodi yalifikia shilingi 11,300,088,000/= katika maeneo mbalimbali nchini licha ya juhudi zilizokwisha kufanywa na Shirika kuhakikisha malimbikizo hayo yanakusanywa.” Sasa kama nilivyosema, mimi naseme tu kwa ajili ya Manispaa ya Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hapa pamoja na kwamba deni ni kubwa sana, lakini je, deni hili linahusu nini; je ni kodi halisi au kuna kitu kingine? Deni hili limechanganywa na faini ambayo wanalipishwa wale wapangaji kwa kutokulipa kodi kwa wakati. Sasa kwa nini watu wanashindwa kulipa kwa wakati, kuna sababu mbalimbali. Wengi wanakuwa hawana uwezo, wengine labda wakati ule ambao walipaswa kulipa walikuwa na matatizo mbalimbali ya kiuchumi na kwa maana hiyo, wameweza

kulimbikiza na hivyo wanashindwa kulipa. Sasa kama walishindwa kulipa kabla ya kuwekewa riba, je, wakiwekewa riba wanaweza kulipa haiwezekani.

Mimi nasemea kwangu katika Manispaa ya Iringa, ukiangalia nyumba ambazo zilikuwa za Msajili wa Majumba, wale wapangaji wake kwa kweli hali zao kwa sasa hivi kiuchumi ni mbaya sana, lakini wanadaiwa kodi kubwa kwa sababu ina-include interest kwa maana kwamba ni faini ambayo walipaswa walipe kwa wakati ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi naomba chini ya uongozi imara kabisa ambao Mheshimiwa Waziri anao, achukue hatua kwa hawa ambao mimi nawaomba ya kuweza kusamehe riba ili kodi halisi inayobakia waweze kupewa muda wa kuweza kulipa. Mimi nadhani hiyo itakuwa ni motisha kubwa kabisa na hivyo kuweza kuwasaidia ili waweze kulipa, bila hivyo kwa kweli wataendelea kudaiwa na mwisho wake kama alivyosema wanaweza wakachukuliwa hatua za kufikishwa Mahakamani. Sidhani kama Serikali ingependa kuona wananchi wake ambao kwa kweli ni wanyonge wananyanyasika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni hapo kwenye upande wa *National Housing*. Mheshimiwa Waziri, amesema katika ukurasa wa 28 kwamba: “Wale ambao wameshaanza kulipia wahakikishe wanakamilisha malipo ifikapo mwezi Desemba, 2003. Wale ambao, kwa sababu mbalimbali hawajaanza kulipia nyumba hizo, wanashauriwa kuanza kulipia mara moja na ifikapo 1 Novemba, 2003 hatua za kisheria zitaanza zitachukuliwa kwa wapangaji hao.” Sasa ukiangalia katika jedwali namba 10 nasemea wananchi wangu wa Manispaa ya Iringa. Katika jedwali namba 10 unakuta katika Manispaa ya Iringa watu ambao bado hawajaweza kununua nyumba wapo 26. Sasa ni sababu ipi inayofanya hao watu wasiweze kununua hizo nyumba, siyo kwamba hawapendi wangependa sana kuzinunua hizo nyumba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba Wizara kwa kutumia Ofisi zake zilizoko Mikoani, wafanye utafiti kuona ni kwa nini hawa watu wameshindwa kununua nyumba hizo. Wameshindwa kununua hizo nyumba kwa sababu aina ya watu wanaoishi katika nyumba hizo ni wale watu ambao hawana uwezo kabisa. Naomba nitoe mfano. Kwa mfano, kuna nyumba nyingine wanaishi akinamama wajane, ambao waume zao walikuwa wanafanya kazi wamefariki sasa hawana uwezo, wangetamani sana kununua nyumba zile lakini hawana uwezo.

Kwa hiyo na wengine kwa mfano ni wastaafu walikuwa wanafanya kazi zamani. Sasa hivi wamestaafu kazi nyumba zile wangependa kwa kweli kuzinunua, lakini hawana uwezo wa kuzinunua kwa sasa. Sasa kwa nini Shirika la Nyumba basi au Wizara isiwaruhusu hawa wakaendelea kuwa wapangaji? Kwa sababu wakiambiwa waondoke katika hizo nyumba na hivyo kama walivyopewa muda mpaka mwezi Novemba, 2003 wataenda wapi na sisi tunasema kwamba Sera ya CCM ni kuhakikisha kwamba tunaondoa kero kwa wananchi wetu na hii ni mojawapo ya kero ambayo wananchi hawa hawana mahali pa kuishi na waliweza kupanga katika nyumba za Shirika la Nyumba, kwa wakati huo na walishukuru na kwa kweli mpaka sasa hivi wanafurahi sana kwamba angalau Serikali ilikuwa imewajali na waliweza kupata nyumba. Sasa hivi wanaambiwa kwamba kufikia mwezi Novemba, 2003 wawe wameshaondoka ili watu wengine waende wakazinunue hizo nyumba!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna huyo mama mmoja mimi alinifuata akaniomba kabisa kwamba niko chini ya miguu yako, nikamwambia naomba usimame usikae chini ya miguu yangu, kwa sababu mimi ni kiongozi wako, akasema hapana naomba unisaidie. Kwa sababu mimi nina watoto wengi na mume wangu alifariki, naomba ukamwone Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, anisaidie niwe mpangaji. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, wakati unahitimisha hoja yako naomba utueleze hao watu ambao kwa kweli wameshindwa kununua na wangependa kununua hizo nyumba kwa sababu toka mwaka 1993 mpaka leo kwa nini wasinunue, wangependa kuzinunua hizo nyumba, lakini kwa kweli hali ya maisha ni mbaya, basi waruhusiwe kuwa ni wapangaji. Kwa sababu kama watakuwa ni wapangaji wataweza kulipa kodi na hata kama mnadhani kwamba inawezekana kodi sasa hivi wanayolipa pengine ni kidogo, kwa ajili ya kulipia zile gharama mbalimbali ambazo Shirika linazipata, basi waweze kungezewa kodi, lakini wako tayari kuweza kulipa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mchango wangu ulikuwa huo. Kwa sababu wananchi wa Manispaa ya Iringa waliniomba sana kwamba wale wanaoshindwa kuzinunua nyumba hizo, kwa kweli

Wizara iweze kuwasaidia waendeleo kuishi katika nyumba hizo kwa sababu kama ni kuuziwa wangeweza kuzinunua, lakini wameshindwa kuzinunua kutokana na hali ngumu ya maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. RHODA L. KAHATANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu nilikuwa sijajua kama nitapewa nafasi ya kuongea sasa hivi, ndiyo maana uliona hapa nayanyuka kwa kushtukashtuka. Lakini nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya kila binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka mingi watu wengi wamekuwa wanailalamikia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, kwa mambo mbalimbali hasa mambo ya ugawaji wa viwanja, utoaji wa Hatimiliki na rushwa ambayo walikuwa wanasema kila mara kwamba Wizara hii imekuwa kiongozi kwa rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tangu Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, wapanie kwamba watapambana na rushwa na watahakikisha kwamba wananchi wanapata migao ya viwanja kwa usawa, tunaona maendeleo yapo na tunaona haki jinsi inavyotendeka. Kwa hiyo, nina sababu zote za kumpongeza Mheshimiwa Waziri na uongozi wake katika Wizara, kwa kazi njema wanayoifanya. Kama Waheshimiwa Mawaziri wote watafanya hivyo, nchi hii itabadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mtu mwema anaonyesha matendo yake siyo maneno yake, maneno kila mtu anaweza kusema kwa sababu si tunatumia midomo yetu, kila mtu ana mdomo wake na una kipaji chake. Sasa midomo inaweza kusema mengi kwenye majukwaa lakini kwenye utendaji tukawa vingine. Kwa hiyo, tunawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri, wale wanaojitahidi kama Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuzungumzia juu ya viwanja hivi 20,000 ambavyo wamevipima ili kuwasaidia wananchi wapate viwanja. Lakini vilevile sijakupata viwanja tu ni kuwa na mipango mizuri katika mji na miji yetu yote ya Tanzania. Jiji la Dar es Salaam ambalo ni Jiji kubwa na Manispaa zake tuwe na viwanja vilivyopimwa kuliko hivi vya kuvamiavamia. Napenda kuwapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja nilikuwa Uganda, Spika wa Uganda akasema hivi nyie Jiji la Dar es Salaam mmelifanya nini, nilikuwa angani kwenye ndege nimeona nyumba za zamani lakini ziko kwenye mistari na barabara unaziona hata ukiwa kwenye ndege. Mimi nikamwambia bwana umepita mahali padogo tu, Magomeni bila shaka, lakini ukiangalia sehemu nyingine bado zinaendelea kuvamiwavamiwa kwa hiyo hata barabara ukiwa kwenye anga huwezi kuziona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi viwanja 20,000 ni vile vitakavyotuletea sifa hata kama watu wanapita tu kwenye anga zetu wataona hapa kuna binadamu wenye ubongo, maana ubongo si lazima ukakae kimya kwenye kichwa ufanye kazi. Nawashukuru sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika viwanja hivyo kuna mambo mawili makubwa ambayo nimeona yamejitokeza ambayo ni sifa kwa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi na ni sifa pia kwa nchi yetu. Moja, ni lile la kwamba viwanja vilivyopimwa na vile vingine vilivyopimwa zamani Hatimiliki zimeanza kutolewa haraka. Ilikuwa shida sana kupanda ngazi za jengo refu la Makao Makuu ya Wizara, hata kuna wakati jengo lile lilikuwa halina umeme, sasa fikiria mtu kama mimi kupanda ngazi zile mpaka kwenda kumpata yule mpima wa ramani ghorofa ya sita ilikuwa shida. Lakini sasa hivi kazi imerahisishwa viwanja vimepimwa na Hatimiliki wamepata na hata wale wa zamani mpaka wanatangazwa kwenye magazeti kwenda kuchukua Hatimiliki zao. Hili ni jambo la maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine katika upimaji huo huo wa viwanja ni lile kuwasaidia wananchi kuondoa umaskini. Sheria ya Ardhi imetusaidia kwamba watu kumbe wanaweza kutumia ardhi kuondoa umaskini wao. Watu walipopata fedha pale Dar es Salaam baada ya kupima vile viwanja wakapata fidia, wameifurahia sana Serikali na wanaishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwamba, kweli kuondoa umaskini ndiyo hicho, ingawa wengine wamezitumia vibaya zile fedha. Lakini fedha zimekwenda kwa watu wenye ardhi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitawaambia kitu kimoja cha kuchekesha nilikiona kule Mbweni, wakati napita watu wakaniita njoo nyie mnawapa watu fedha bila mpangilio ona wanavyofanya. Mzee mmoja ana wake watatu alikuwa na ardhi yake kubwa na amepata fedha nyingi, nasikia alipata zaidi ya shilingi milioni 20/= na hajawahi kushika hata shilingi 300,000/=, yeye mwenyewe alikuwa anamwambia Mwenyekiti wa Kijiji kwamba katika maisha yangu sijawahi kushika shilingi 300,000/= sasa ameshika shilingi milioni 20/=. Mnaona alivyofanya anaagiza vijana wawili wa kike waende pale Boko kila siku jioni kumnunulia bia mbili ili apate kunywa pale nyumbani anapoishi kwenye nyumba mbovu. Sasa hapo ndiyo tatizo linapokuja sasa mnawapa fedha kwa ajili ya ardhi, lakini wengine ndiyo hawawezi kuzitumia, lakini walio wengi wanashukuru. Sasa kwenye Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, nashauri kiwepo kitengo cha kuwashauri hao wachache ambao hawezi kuzitumia fedha hizo vizuri. Mimi nafikiri kiwepo Kitengo kabla hamjatoa fidia watu wanaohitaji ushauri muweze kuwashauri kwamba kama wamepata hizi fedha, Shirika letu la nyumba liwajengee nyumba nzuri zaidi itawasaidia. Sasa kunywa bia mbili kila siku, hizo shilingi milioni 26 si zitakwisha. Sasa kulipa fedha za fidia ni vizuri, lakini pia mtusaidie ili wananchi wazitumie vizuri fedha zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilikuwa napenda kulizungumzia ni kuhusu suala la rushwa. Katika Makao Makuu ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, mimi nafikiri wamejitahidi sana kuondoa rushwa, mafaili hayapotei kama yalivyokuwa yanapotea huko nyuma. Nilikuwa kwenye Jimbo langu na mimi watu wakasema jamani fulani alikwenda wiki moja tu Wizarani amerudi na hatimiliki yake na za wenzake mambo yamekuwa mazuri. Kwa hiyo, yale mafaili yalikuwa yanapotea sijui shimo lilikuwa wapi katika Wizara hii sasa lile shimo limefukiwa. Kwa hiyo, tunawashukuru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba utaratibu huo ambao mmeutumia Makao Makuu ya Wizara, mkautumie hata kwenye Halmashauri zetu na wenyewe wafundishwe kwa sababu ukienda pale wanakwambia njoo kesho, njoo kesho na hii hali ipo katika Halmashauri zetu. Vilevile hata Wenyeviti wengine wa Halmashauri wanakuwa ni kipingamizi kikubwa sana katika ugawaji wa ardhi kule kwenye Halmashauri zetu. Nao naomba kama kuna uwezekano wa kuwasaidia kuwaelimisha basi wapate kuelimishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni la Shirika la Nyumba. Kwenye Shirika la Nyumba nataka kuzungumzia kipengele kimoja tu. Naishukuru Kamati imelipongeza Shirika la Nyumba kwa kazi zake nzuri za kujenga nyumba za kuuza. Shirika hili katika Bunge hili humu ndani walisema tusilibinafsishe ili waweze kuendelea kujenga nyumba kwa faida ya wananchi na ndiyo kazi ambayo Shirika la Nyumba inaifanya na nadhani wanafanya vizuri. Lakini uwezo wa biashara unakuwa mzuri unapokuwa na mapato ya kutosha. Sasa Mashirika ya kukopesha Shirika ya Nyumba ni machache na ni ya kuhangaika sana. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naiomba Serikali kwa kushirikiana hasa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, asaidie kuharakisha kuanzisha *Institution* ambazo zitakuwa ndizo za kukopesha Watanzania kwa ajili ya kujenga nyumba kwa kupitia Shirika la Nyumba basi watakuwa na unafuu wa kujenga nyumba ili wananchi waweze kupata mahali pazuri pa kuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yetu ya Ujenzi imeza nyumba zake za Serikali nyingi kwa watu ambao walikuwa wanaishi kwenye nyumba hizo. Sasa Wizara inahitaji kujenga nyumba nyingine, najua wanatumia *National Service* kuwajengea nyumba.

Mimi ombi langu ambalo naona ni muhimu waweze kushirikisha Shirika la Nyumba na wenyewe waweze kupata *contract* kwa sababu katika shughuli zao wanawajengea nyumba hata watu wengine hata wewe Mheshimiwa Mwenyekiti, kama una kiwanja chako unataka wakujengee watu wa Shirika la Nyumba



watakujengea nyumba nzuri sana. Kwa hiyo, naomba Wizara ya Ujenzi badala ya kupeleka fedha zote mahali pamoja, nyingine wazipeleke kwenye Shirika la Nyumba waweze kupata *contract*, waweze kujenga nyumba za Serikali. Kwa sababu kwanza watejenga nyumba za bei rahisi kwa sababu wao ni sehemu ya Serikali. Kwa hiyo, ningeomba labda Wizara iweze kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache ambayo nilikuwa nayo, naomba nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi na vilevile niunge mkono hoja hii ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa asilimia mia moja. Nakushukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge wale ambao tulitaka wazungumze asubuhi wamemalizika. Jioni tukirudi tutakuwa na wachangiaji wafuatao: Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Prof. Juma Mikidadi na Mheshimiwa Frank Magoba na hawa watakuwa wanatosha, baadaye tutamwomba Mheshimiwa Naibu Waziri, aanze kujibu hoja halafu atafuata mtoa hoja mwenyewe.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.57 Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Eliachim J. Simpasa) Alikalia Kiti*

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nitumie nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi niwe msemaji wa kwanza mchana huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nataka nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, kutokana na hotuba yake nzuri ambayo kwa kweli ukiiangalia nadhani kwa mara ya kwanza unaweza ukapata orodha ya vijiji kwenye hotuba ya Waziri imeambatanishwa. Hii kwa kweli sasa tunafika mbali, ni safi sana. Tunakupongeza sana Mheshimiwa Waziri kwamba, tunaweza tukaona hata vijiji vyetu vile ambavyo tayari vimepata hati na kadhalika. Kwa kweli tuna takwimu nyingi nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba niseme kwamba, nitajielekeza zaidi kwenye matatizo ya ardhi Wilayani Babati na hasa kwenye Jimbo la Babati Mashariki. Nataka nielezee kutoka mwanzo kwamba, historia ya migogoro ya ardhi au matatizo ya ardhi kwenye Wilaya ya Babati ni ndefu kidogo. Mimi kabla ya kuingia Bungeni nimeikuta na nilipoingia vile vile tumeendelea kushauriana na kuona namna ya kutatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri atakumbuka kwamba, yeye mwenyewe aliwahi kufika Babati. Lakini vile vile kwenye mwanzo wa mwaka 1997 aliyekuwa Jaji Mkuu, Mheshimiwa Francis Nyalali, ambaye sasa kwa kweli ni marehemu na Mungu amrehemu, aliwahi kuondoka kwenye kiti chake cha kuwa Jaji Mkuu na kutembelea Wilaya na hasa wakati ule za Mkoa wa Arusha na Babati ikiwemo. Alitembelea vijiji na mimi nikiwa naye na wote tunakumbuka alipomaliza ziara kwenye Wilaya ya Babati, Mbulu, Karatu na nadhani na Arusha, alisimamisha kesi zinazohusiana na matatizo ya ardhi na hasa zinazohusu Operesheni Vijijini. Alisimamisha kesi kwa muda na hatimaye baada ya kuona matatizo yale alitoa maelekezo na shughuli ziliendelea.

Lakini vile vile Mheshimiwa Rais, amefika kweli Babati kati ya 1995 mpaka 2000 karibu mara nne hivi. Mara zote alikuwa anapewa matatizo makubwa mawili. Moja ni mashamba yaliyotekelezwa na wamiliki wake na wakati huo huo wananchi wakiwa na uhaba wa ardhi. Lakini la pili lilikuwa tatizo la kuwaweka wananchi kwenye mashamba hayo yaliyotekelezwa wakati ambapo hatimiliki zake zilikuwa hazijafutwa hapo miaka ya nyuma. Kwa hiyo, kulikuwa na matatizo ya aina hiyo. Namshukuru vile vile Mheshimiwa Waziri naye amefika, Mheshimiwa Waziri Mkuu naye alifika kufuatilia utekelezaji. Nataka niseme Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipofika alifika na Mheshimiwa Tatu Ntimizi, ambaye wakati ule alikuwa Naibu Waziri wa Afya, lakini leo ndio Naibu Waziri wa Ardhi, kwa hiyo vile vile anayafahamu

matatizo hayo. Kama nilivyosema na Mheshimiwa Waziri naye alifika na hata wakati mmoja alitusaidia kuona jinsi *plot* moja ilivyokuwa inajengwa kabisa ndani ya ziwa, yaani eneo ambalo ziwa linafikia na kwa kweli tunamshukuru baadaye aliweza kubatilisha ile hati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa leo ningependa nijielekeze kwenye maeneo mawili. Nitazungumzia kwa ufupi sana suala la utwaaji wa ardhi na ubatilisho wa Hatimiliki. Katika kipindi hicho cha mwaka 1995 mpaka 2000, Mheshimiwa Rais kwa kweli alibatilisha Hatimiliki ya baadhi ya mashamba hasa kwenye Jimbo la Babati Mashariki. Yako mashamba matatu ambayo alibatilisha hati yake ambayo ndiyo nilitaka niyasemee. Moja ni *Babati Sisal Estate* na lingine ni *Manyara Estate* na la tatu *Kinyume Estate*. Taratibu zilifuatwa, Wizara ya Ardhi, nashukuru ilituma wataalamu wakafanya kazi kubwa sana ya kubainisha mashamba yaliyotelekezwa na yale yanayohitaji kwa kweli kumegwa. Wataalamu walikaa karibu mwezi mzima wakati ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka niseme kwamba, yapo mafanikio na bado yapo matatizo. Eneo ambalo limeonyesha mafanikio katika hati ambayo ilikuwa imebatilishwa umiliki wake ni Shamba la *Manyara Estate*, baada ya kufutwa utaratibu wake umekamilika na Serikali ilishakabidhi shamba hilo kwa wananchi wa Kijiji cha Maghala. Kwa hiyo, tunaishukuru Serikali kwamba, kazi hii ilikamilika na hakuna sijasikia matatizo mengine, nadhani wananchi wanaendelea na utaratibu wao wa namna ya kuona kwamba watatumia vipi maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Kinyume Estate* bado, lakini leo nataka nizungumzie tatizo kwenye Shamba la *Babati Estate*. Baada ya Mheshimiwa Rais kubatilisha hati ya *Babati Sisal Estate*, yalifuata maelezo ya Serikali kwamba, wananchi ndio wanaopaswa kulipa fidia. Wakati ule wananchi walitangaziwa kwamba walipe fidia ya shilingi milioni 15. Taratibu za kuwafikishia wananchi taarifa hizo zilifanywa na Kamati ya Ushauri wa Ardhi ya Wilaya, ambayo Mwenyekiti wake ni Mkuu wa Wilaya na ikaamuliwa kama fidia ya shamba hilo ni shilingi milioni 15, basi kila ekari ambayo atapewa mwananchi ilipiwe shilingi 10,000 na katika hilo shilingi milioni 28 zilikusanywa na wananchi na shilingi milioni 15 zikapelekwa Wizarani kama fidia ya shamba hilo. Sehemu iliyobaki nina hakika itakuwa Halmashauri ya Wilaya kwa ajili ya shughuli nyingine za upimaji na shughuli nyingine za ardhi kwa shamba hilo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Wizara kupokea shilingi milioni 15, ndipo baadaye ilijitokeza kwamba kuna utata kwenye suala la fidia. Kilichotolewa maelezo kama fidia ya shilingi milioni 15 sio fidia ya shamba hilo. Ni maalezo tu ya awali ya kufanya tathmini katika kubatilisha hati hiyo. Hayo ndiyo maelezo ambayo mimi nimeyapata, kwa hiyo sasa lina matatizo. Tukaambiwa kwamba thamani ya shamba hilo ni lazima ithibitishwe na Mthamini Mkuu wa Serikali. Sasa fedha hizi shilingi milioni 15 zimepelekwa Wizarani, nadhani zipo tangu mwisho wa mwaka 2002 mpaka sasa. Wananchi wanachosubiri ni kuelezwa uamuzi wa Mthamini Mkuu ni nini sasa juu ya fidia hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shamba hilo lenyewe ukiliangalia kama wanavyosema viongozi wote, wanalijua na wengi waliofika wanalifahamu na wote tunalijua, hatutazamii kwamba itakuwa thamani ya ajabu sana. Wananchi kwa kuwa tayari wameshalipa shilingi milioni 15 sasa nadhani unaweza ukaona lilivyo zito kwamba wananchi wanadhani tayari wameshalipa fedha shilingi milioni 15 na zipo Serikalini, lakini bado shamba hawalipati huku maelezo yanakuja kwamba bado kulikuwa na utata, jambo hilo lilikuwa halijaisha. Sasa ningemwomba Mheshimiwa Waziri basi awafahamishe awaambie wananchi wa Babati kwamba thamani ya fidia ya shamba lile ni shilingi ngapi na tunatakiwa kufanya nini ili kero hii iishe. Hakuna sababu ya kuendelea na jambo hili kwa muda mrefu ujao. Tunachohitaji ni hicho, kufahamu ili tufikie mwisho wa kero hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni suala la mashamba ambayo Serikali yenyewe iliaweka wanavijiji wakati wa Operesheni Vijiji mwaka 1974/75 kwenye maeneo ambayo yametekelezwa na wenye mashamba. Lakini wakati huo huo Hatimiliki za hayo mashamba hazikufutwa. Lakini nafahamu kwamba, yalikuwepo maagizo kwamba maeneo yale ambayo sasa wananchi wamekwishakaa kwa miaka mingi sana yamegwe. Nafahamu Wizara ilishatuma wataalamu wake na walifanya kazi na Maafisa walibainisha maeneo yapi yamekaliwa na wananchi na yapi ambayo yanaweza yakaachiwa wahusika. Sasa baada ya zoezi hilo wako wamiliki ambao wamekubali kwamba eneo lile ambalo wananchi wamekalia na wamekwishajenga zipo shule, zipo huduma mbalimbali yapo Makanisa, Misikiti na kadhalika basi maeneo

yale yamegwe. Wako wamiliki ambao wamekubali. Lakini mpaka leo Serikali haijakamilisha kazi hii. Sasa hilo ni tatizo. Namwomba Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, basi hebu tujue tatizo sasa liko wapi. Ukiuliza Wizara, Wizara inasema kwa kweli wanaohusika ni Halmashauri ya Wilaya. Ukiuliza Halmashauri ya Wilaya naona kama bado tatizo ni Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka jambo hili liishe, wananchi waondokane na kero hii. Serikali ni moja na kama Serikali ni moja tunataka kujua kwamba Serikali lazima ina namna ya kufanya kazi kuhakikisha kwamba kero ya wananchi inatatuliwa. Serikali haiwezi kuendelea kutupiana mpira kwamba mara Wizara mara Halmashauri, inakuwa kweli si jambo zuri. Mashamba yanayohusika ni mashamba kama matatu ninayoyafahamu ambayo kwa kweli shamba moja la Endonaike tunalikubali, lakini mashamba mawili ya *Amiri Estate* na *Miombo Estate* wao wamekataa. Lakini taratibu za sheria ziko pale zinaeleza. Mheshimiwa Rais, anayo Mamlaka ya kumega na kwamba akimega ni nini kinafuata, inaeleza pale. Sasa kwa nini taratibu hizi zisifuatwe ili jambo hili liishe. Wananchi hawa sasa wanakabiliwa na matatizo mengi, mara washtakiwe mara wafukuzwe, basi ni kero, usumbufu karaha nyingi na adha kwa kweli nyingi sana. Kwa hiyo, tungependa mambo haya kwa kweli yamalizike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho na mimi nataka nikubaliane na Mheshimiwa Sophia Simba, aliyezungumzia suala la ugawaji wa *Plot*. Mji wa Babati sasa ni Makao Makuu ya Mkoa Manyara. Ni mji unaopanuka kwa haraka, unahitaji kupimwa vizuri kwa utaratibu wa kisasa na ikumbukwe kwamba Babati ni eneo la Kilimo. Kwa hiyo, mashamba yalikuwa mpaka kwenye maeneo ambako mji uliko sasa. Kwa hiyo, unapochukua eneo lile na kufanya eneo la mji, kwa vyote vyote vile maana yake unachukua na mashamba ya watu walio karibu pale. Sasa ni vizuri jambo hili likawekwa wazi vizuri. Kama mtu ana eka moja, mbili au tatu. Kama eka moja inapewa *plot* kwa mfano nne au sita, kwa nini mwenye kiwanja, haki ya kwanza asifidiwe kabisa?

Lakini ya pili apewe na yeye *plot* pale. Mimi nadhani lazima kuwe na uwiano kama kuna *plot* 4 basi walau yeye apewe moja au moja kwa tatu. Zikiwa 6 apewe 2. Pamoja na kwamba kuna lile wazo la kwamba hatutaki kuweka watu wa eneo moja katika eneo moja. Lakini basi mmiliki anaweza akapewa moja lakini kama ana watu wake, vijana wake zaidi ya umri wa miaka 18 wanaweza wakapewa katika eneo lingine la mji lakini haki hiyo wapewe. Kwa hiyo, la kwanza wapewe fidia na la pili vile vile kwa kweli wapewe *plot*. Hii ndiyo namna ya kuendeleza jamii kwa usawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi baada ya kusema hayo, kama nilivyosema nahitaji tu maelezo ya Mheshimiwa Waziri, ili kwa kweli kero hii iishe kwa wananchi wa Babati, basi naomba nisaidie maelezo na kwa kweli na sisi tuone kwamba tunayo haki sawa na watu wengine katika kugawana raslimali ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja mia kwa mia. (*Makofi*)

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi ili niweze kuchangia katika hoja hii ya ardhi. Ningependa nianze na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, rafiki yangu, *College-mate* wangu, *Class-mate*, wangu ambaye mimi ninamfahamu sana kwa umakini wake kulikoni Waheshimiwa Wabunge wengi hapa. (*Makofi*)

Ningependa kumpongeza na Naibu wake, ambaye ni mchumba wa Wazaramo, ambaye umahiri wake unajulikana sana. Pia vile vile nimpongeze Katibu Mkuu, ndugu yangu Bibi Salome Sijaona na viongozi wao, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi. (*Makofi*)

Nawapongeza pia kwa hotuba safi, fupi, lakini yenye kina kwa sababu imepanuliwa sana katika vielelezo. Sasa pamoja na hayo niseme machache tu ambayo yatasaidia kuboresha. Nilikuwa nikiangalia katika vielelezo, kielelezo Na. 5, 9 na 12, ambavyo vinaonyesha vijiji vyenye *plan* za upimaji, masuala ya mafunzo ya kujenga nyumba bora na kadhalika. Lakini katika kuangalia nimeona kwenye Mkoa wa Pwani kwenye kielelezo Na. 5 ni Wilaya 2 tu Bagamoyo na Mafia ndizo ambazo zimeweza kufanya chochote. Kwenye kielelezo Na. 6 ni Wilaya 2 vile vile Mkuranga na Mafia na kwenye kiambatanisho Na. 12 nimeona Pwani ni Wilaya moja tu. Sasa swali je, ni uzembe wa Maafisa wa Wilaya kule au Wizara

haikodolei macho katika maeneo yote ya Tanzania? Labda Mheshimiwa Waziri atanjibu katika hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiacha hilo nataka niipongeze Wizara kwa kazi nzuri iliyofanyika ya kugawa viwanja ambavyo zamani ilikuwa ni matatizo makubwa sana. Lakini nilitaka kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba, bado tatizo lipo pamoja na kwamba kuna *improvement* kutokana na *computerisation*, lakini bado viwanja vinagawiwa kimoja kwa watu zaidi ya wawili au watatu na migogoro bado ipo. Naamini kabisa kwamba, sababu kuu tatu zinachangia katika hili. Ya kwanza ni kutokuwa na kumbukumbu kamilifu za kuaminika ingawa sasa hivi zimeanza kuongezeka. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba maafisa pengine kwa nia nzuri tu wanajikuta wanagawa kiwanja kimoja kwa zaidi ya mtu mmoja.

Pili, ubabaishaji wa baadhi ya maafisa hasa wale ambao Mheshimiwa Waziri, mmewafukuza kazi na kuwaachisha. Wanavijua hivi viwanja na matokeo yake ni kwamba, wanakwenda tena kuviuza kwa njia ya pembeni. Lakini hapa lazima nikiri kwamba, bado kuna mabaki katika Wizara ambayo wanashirikiana nao. Kwa sababu zinatolewa *documents* ambazo zinakuwa ni *fake*. Kwa hiyo, nafikiri ile kazi nzuri mliyoifanya ya kuwasafisha wale waovu bado muendelee kupangusa pangusa ili hali hii isiendelee kutokea.

Sababu ya tatu ni uvamiaji. Kuna watu tu wanaamua kwenda kuvamia akiona kiwanja hajui ni cha nani na nini anavamia. Sasa hivi najua kwamba Wizara haina uwezo wa kuweza kulizuia. Lakini moja tu ni kwamba, inapotokea hivi wale ambao ni wamiliki halali ndio wanaachiwa kupigana vita hii na wale wengine. Ningefikiri kwamba, Wizara ingechukua jukumu la kuhakikisha kwamba watu wa namna hii wanashikishwa adabu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye Sheria namba 4 na 5 za mwaka 1999, pamoja na mapungufu ambayo yamejitokeza katika sheria hizi lakini sheria nzuri na zilikuwa na nia nzuri na hapana budi zitekelezwe. Nimeangalia katika ukurasa pale wa 13, jitihada zimefanywa kutoa elimu kwa umma na yote yaliyoelezwa pale. Lakini inapelekea nadhani kama vile nilipoanza mwanzo kwenye maelezo, inaelekea kuna baadhi ya Mikoa na Wilaya bado elimu hii haijafikishwa. Kule Wilayani kwangu Kisarawe, bado yapo matatizo baadhi ya Maafisa wa Ardhi wanatoa ardhi kinyume na taratibu na pengine kwa sababu ya kutokuelewa kwa Serikali za Vijiji majukumu yao, basi wanazitumia hivyo. Mahali pengine utakuta viongozi wa Serikali katika ngazi ya Wilaya na Mkoa, wanaamrisha tu kusema itolewe ardhi nje ya utaratibu. Sheria ambayo imepita miaka yote hii karibu minne sasa, lakini bado utekelezaji wake hatujawa mzuri.

Nitoe mfano tu kule kwangu nina migogoro hivi sasa katika Kijiji kinachoitwa Muhaga Wilaya ya Kisarawe. Tayari ardhi imetolewa kwa mtu mmoja eka 1,000 na eneo hilo ndani yake kuna makaburi. Sasa matokeo yake ni kwamba wanakijiji hawaridhiki na hali hii na hii imetokana na *collusion* baina ya Afisa Ardhi na Mwenyekiti wa Kijiji, ambaye vile vile hajui sheria zake. Kwanza hata katika ngazi ya Mkoa sheria inasema hakuna mwenye mamlaka ya kuweza kutoa zaidi ya ekari 500. Lakini utakuta Afisa mmoja tu na Mwenyekiti wa Kijiji wanatoa ekari 1,000. Sasa mimi ningeomba Mheshimiwa Waziri, kwanza elimu isambazwe katika maeneo yote kama jitihada unazozionyesha pale katika ukurasa 13, lakini zifike katika Wilaya mbalimbali. Lakini la pili pale ambapo zinapoonekana dosari kama hizi tunazozisema, ningemshauri Mheshimiwa Waziri afuatilie ili kuondoa migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia vile vile katika Wilaya yangu kuna tatizo moja ambalo ningemwomba Mheshimiwa Waziri, alipatie jibu ili wananchi wa Kisarawe pale Mjini waelewe na lisipopatikana hata kwenye Kamati ya Matumizi nadhani itabidi niulize swali ili kusudi nafahamu kwamba huenda akawa hana jibu hilo hivi sasa lakini anipe nafasi mimi labda na baadhi ya viongozi wa pale Wilayani tukamzungumze kusudi aelewe. Kwenye miaka ya 1980 Mji wa Kisarawe ulipimwa kwa maana ya kutaka kuuboresha kuwa Mji wa Kisasa. Wananchi wakavunjiwa nyumba zao wakaahidiwa fidia na Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa bahati mbaya toka wakati huo mpaka hii leo, fidia ile haijatolewa na wananchi wangu wamehangaika wamemtumia aliyekuwa Mbunge wakati ule, Marehemu Prof. Malima na mpaka nimefika mimi lakini bado jawabu halijapatikana. Naomba lipatikane jibu lini wananchi hawa watapewa fidia?

Lakini kwa upande wa pili, ningependa kumpongeza Waziri na kuipongeza Serikali kwa jumla, kwa kutatua tatizo kama hilo hilo ambalo limetokea pale katika Vijiji vya Tondoroni na Kiluvya, ambako eneo lilichukuliwa na Serikali kwa ajili ya matumizi ya Jeshi na kukawa na mgogoro mkubwa lakini baada ya muda mrefu fidia zimeanza kutolewa. Sasa namshauri Waziri kwamba, ashirikiane na Wizara zile nyingine zinazohusika kama ni Wizara ya Fedha au TAMISEMI na kadhalika, tupate ufumbuzi wa fidia za wananchi wa Mji wa Kisarawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nizingumzie juu ya utoaji wa Hatimiliki. Ni kweli kuna *improvement* lakini bado zipo Ofisi ambazo kule katika ngazi za Wilaya hazijatekeleza kikamilifu. Nitoe mfano tu namfahamu mwananchi ambaye amepewa kiwanja toka mwaka 1993 kule Bagamoyo Mjini mpaka hivi sasa amefuatilia Bagamoyo Mjini, kule Mkoani na amefuatilia kila mahali, lakini hati haipatikani na ameshalipa kila kitu. Sasa hii haieleweki mahali karibu sana na Makao Makuu kama vile inawezekana namna gani wananchi washindwe kupata Hatimiliki ambazo hivi sasa katika sehemu nyingine kwa mfano pale Dar es Salaam jambo hili limeanza kupatiwa ufumbuzi mzuri. Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Waziri, hebu aelekeze nguvu zaidi katika maeneo ambayo yanaharibu kazi nzuri inayofanywa na Wizara kwa kutoa dosari kama hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa sina mengi sana, kubwa naipongeza Wizara kwa kazi nzuri lakini wafanye masahihisho katika maeneo ambayo yanatia dosari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naiunga mkono hoja hii mia kwa mia, ahsante.

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami nichangie katika Wizara hii ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

Naunga mkono hoja hii kabla sijaenda mahali popote, kwa sababu kwanza, Waziri Cheyo, namfahamu kuwa ni mchapakazi kweli kweli, pamoja na Naibu wake Waziri na Mama Salome pia namfahamu kwa uchapaji wake wa kazi. Kwa hiyo, sina wasi wasi kuhusu masuala ya utekelezaji wa mambo ya zamani. (*Makofi*)

Lakini linalonitia moyo zaidi ni katika hotuba ya Waziri pale ukurasa wa 3, ibara ya 8 kuhusu matumizi ya kawaida ya Wizara ukilinganisha na fedha za maendeleo, utaona matumizi ya kawaida mishahara na kadhalika ni madogo zaidi kuliko fedha za maendeleo. Kwa sababu matumizi ya kawaida shilingi 4.8 bilioni wakati fedha za maendeleo ni shilingi 10.03 bilioni mara mbili na robo ya kiwango kinachotakiwa. Kwa hiyo, huu ni mfano mzuri sana kwamba fedha za maendeleo ziwe nyingi kuliko fedha tunazotumia kwa ajili ya mishahara na shughuli nyingine. Huu ni mfano mzuri, nasema Mheshimiwa Cheyo, ameimulika Wizara hii vizuri sana. Maana yake hata jina lake linajulikana hivyo Asimulike, lakini amemulika hasa. Kwa hiyo, mimi namsifu kwa kazi anayoifanya na kwamba mimi nampongeza sana pongezi nyingi kweli kweli. Fedha za maendeleo ni nyingi zaidi kuliko fedha za matumizi ya kawaida. Hilo ni jambo la kwanza. (*Makofi*)

Jambo la pili nakwenda katika hotuba yake Mheshimiwa Cheyo kuhusu ule ukurasa wa 24 ibara ya 46 hasa hasa mimi nataka kuzungumzia juu ya ujenzi wa nyumba bora kwa gharama nafuu. Kusema kweli suala hili ni zito kwa Tanzania. Mimi siujui nchi yoyote ulimwenguni ambayo watu wanajenga nyumba kwa uwezo wao tu bila ya mikopo. Sasa hili nitazungumzia katika hatua ya pili. Lakini hatua ya kwanza ni hili la ujenzi wa nyumba bora kwa gharama nafuu. Pale Ikwiriri - Rufiji kulikuwa na majaribio hayo wenzetu wa Iran walitaka watusaidie na wananchi wenyewe washiriki katika suala hilo. Zikajengwa nyumba mbili wakaja watu kutoka Dar es Salaam sijui ni wataalamu au vipi kutoka Wizarani walipoona mradi ule wakasema hawa Warufiji kwanza hawastahili kukaa katika nyumba bora namna hii wao wanajenga madungu tu! Sasa walifikiri Warufiji pengine ngedere, kima wanakaa katika madungu, kumbe ustaarabu ambao sasa hivi ulikuwa umeenea ulimwenguni katika miji na kadhalika umeanza na wazo hili la Mrufiji la kujenga dungu, hayo maghorofa yamekujaje? Ni wazo letu sisi Warufiji eti. Wajukuu zetu Wasukuma wangelipataje maghorofa pale Mwanza, kama si sisi kupeleka wazo hili ulimwenguni kote? Sasa sisi wazo lile la ghorofa limetokea kwetu kutokana na madungu tunayojenga. (*Makofi*)

Sasa tatizo watu hawa hawasaidii watu vijijini. Sio wakiwaona wamekaa katika madungu maana ya kuwadharau hata hawastahili kuishi katika nyumba bora, nani aliyesema hivyo? Kwa hiyo, mimi nasema hili wazo na sisi dungu tunalojenga haliwezi kuporomoka hivi hivi, ghorofa nyingi ziliporomoka Dar es Salaam pale, waje Rufiji kuona, waje kujifunza tena mara nyingine, jinsi gani ya kujenga ghorofa imara lisiloporomoka. Madungu yetu hata siku moja hayajaporomoka kwetu. (Makofi)

Kwa hiyo, mimi nasema ujenzi wa nyumba bora vijijini utiliwe mkazo na tutafanya jambo lolote liwezekanalo ili suala la ujenzi kwa gharama nafuu vijijini litekelezwe. Pale Nairobi nilikuwa na Mwenzangu Prof. Saad Yahya, yeye alikuwa katika upande wa Jiolojia. Lakini alichukuliwa na *Shelter Afrique* na ni Mtanzania yule. Amechukuliwa katika *Shelter Afrique* anafanya kazi ya kuweza kuona jinsi gani na utafiti huo wa kuweza kujenga nyumba bora tena kwa gharama nafuu kweli kweli. Sasa sisi sidhani kama tumo katika *Shelter Afrique*. Nadhani katika *UN-HABITAT*, lakini katika *Shelter Afrique* sina uhakika. Lakini pengine ningependa tu Waziri kama kuna uwezekano, sisi tukaingia katika *Shelter Afrique* tukanufaika na taratibu zinazofanyika kule. Kwa sababu yule ambaye anashughulikia kule ni Mtanzania, ni kijana wetu kwa hiyo tunaweza tukalishughulikia jambo hilo na tukachukua na sisi tukapata utaalumu wa kujenga nyumba za gharama nafuu kule vijijini.

Halafu jambo lingine, nitakwenda haraka haraka, nitatumia dakika 5 au 7 tu, sina mambo mengi. Jambo hilo ni kuhusu vyombo vya mikopo kwa ujenzi wa nyumba. Katika ukurasa wa 24, ibara ya 46 na 47, kinachosemwa hapa ni kwamba: “Watumishi wa Serikali waliopewa mikopo ya nyumba tangu Mfuko huo uanze mwaka 1992 ni 417 ambao ni asilimia 29.7 kati ya watumishi wa Serikali 1,427 walioomba mpaka kufika Mei, 2003.” Mikopo hii ni mikopo michache kweli kweli! Sasa katika hali hii napenda kusema kwamba, Wizara ingeangalia jinsi ya kuongeza kasi ya kutoa mikopo kwa sababu vyombo vya kukopesha hakuna. Tangu ile Benki ya Nyumba ilipofilisika na kuvunjika, hali ikawa mbaya, yamekuwa yakisemwa tu maneno jinsi gani ya kuweza kupata vyombo vya kutoa mikopo ya ujenzi wa nyumba. Hakuna nchi yoyote duniani watu wake wanajenga wenyewe kwa kubangaiza bangaiza tu kama Tanzania. Tanzania pekee ndiyo hatuna vyombo vya mikopo, lakini nchi zote zina vyombo vya kutoa mikopo ya ujenzi wa nyumba. Naomba suala hili lishughulikiwe kikamilifu na lifanyiwe kazi ili watu wawe na vyombo vya kutoa mikopo ya ujenzi wa nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalipongeza Shirika la Nyumba chini ya Uenyekiti wa Balozi Hemed. Ninamfahamu sana, ni mtu mchapakazi kweli kweli na ameonyesha mfano mzuri, Shirika la Nyumba sasa limekwenda mbele. Watu walikuwa na malalamiko makubwa, nyumba zilikuwa ovyo, chakavu na kadhalika, lakini sasa tunaona maendeleo, mambo yanakwenda vizuri, nyumba zinapakwa rangi na kuna *review* zinafanyika nyingi sana na kadhalika. Kwa hiyo, nalipongeza Shirika la Nyumba chini ya Uenyekiti wa Balozi Hemed, anafanya kazi nzuri sana. Nashauri kasi ya ujenzi wa nyumba iongezeke na mipango ipangwe vizuri ili Wananchi wengi zaidi waweze kupata nyumba za makazi kama itawezekana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo napenda kuzungumzia ni kuhusu matumizi bora ya ardhi. Amenifilisi Mheshimiwa Janguo, kwa kuongelea ile Sheria Namba 4 na 5 ya mwaka 1999, kuhusu matumizi ya ardhi kule Vijijini na hasa katika Vijiji vyetu. Katika Jimbo langu kuna Vijiji vingi sana vya ujamaa, vingine vimekufa, lakini kufa kwake maana yake ni kwamba, bado watu wanaishi mle kama Vijiji, siyo vya asili, lakini sasa havijulikani viende katika mwenendo wa ujamaa na ujamaa wenyewe ndiyo kama mnavyoona, tunaelekea sijui niseme katika ubepari au wapi, sina hakika!

Maendeleo yetu ni ujamaa katika sura mpya, lakini Vijiji vile vilivyokuwa chini ya ujamaa tunavifanya nini sasa ili viingie katika ile Sheria Namba 4 na 5 na utekelezaji wake uwe mwepesi zaidi na uwe katika utaratibu mzuri? Kwa maana hiyo basi, naomba Sheria ile Namba 4 na 5 baada ya kutafsiriwa katika lugha ya Kiswahili, naona kazi imekwishafanyika, isambazwe na elimu yake ienezwe kwa Vijiji na waweze kuelewa kinachotakiwa kufanyika ni nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo lilikuwa ni jambo langu la mwisho, ninaipongeza sana Wizara, kwa kazi nzuri na iendelee vizuri. Kwa hayo machache niliyosema na hasa ujenzi wa nyumba kwa gharama nafuu, basi Wizara itilie mkazo na ishughulikie suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. FRANK G. MAGOBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Bajeti hii ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kutoa pongezi kwa Waziri mwenye dhamana ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Naibu wake, Katibu Mkuu, Mama Salome Sijaona, *Project Manager*; Bwana Mugemezi na timu yake pamoja na kijana wetu Duduma, ambaye yuko Manispaa ya Temeke. Kwa kweli ni lazima nitoe pongezi kwa sababu hawa vijana wamefanya kazi yao vizuri na ambayo inatoa picha nzuri kwa Serikali kwamba sasa inafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mradi wa kupima viwanja 20,000 unianza, nilikuwa nina wasiwasi nao sana, kwani nilifikiria kwamba baadaye nitakuja kupata matatizo ya kujieleza. Lakini baada ya Viongozi, hasa Mkuu wa Wilaya, Mheshimiwa Baraka Komisaga, Meya wa Manispaa ya Temeke, Mkurugenzi wa Manispaa, pamoja na mimi mwenyewe, kukaa na Wananchi wetu wa Tuangoma na kuwaeleza kwa kirefu suala hili, japo kulikuwa na ugumu, lakini baada ya kuwaambia ukweli kwamba Serikali imedhamiria kupanua Mji na kuboresha Jiji la Dar es Salaam kwa kuwapa watu ambao hawana viwanja ili wajenge nyumba za kisasa, ambazo zitakuwa zinapendezesha Jiji na kuwapatia makazi ya kisasa Wananchi wake, walituelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi bado walikuwa hawaamini sana kama kweli wangeweza kufidiwa, lakini kwa ujasiri wangu pamoja na wa Viongozi wangu akiwemo Mheshimiwa Komisaga, ambaye ni Mkuu wa Wilaya, tulisimama na kuwaeleza kwa undani, kwamba Serikali sasa hivi imebadilika, siyo ile ya zamani. Kwa hiyo, naamini kabisa kwamba sasa hivi ahadi inayotolewa itatekelezwa kwa muda mfupi ambao Serikali imeahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nafarijika kumpongeza tena Mheshimiwa Waziri na timu yake, kwamba walitekeleza ahadi mara moja baada ya viwanja vya Tuangoma kupimwa, haikuchukua hata wiki tatu Wananchi wangu waliweza kulipwa. Ninaipongeza Serikali, kama itakuwa inatekeleza ahadi namna hiyo, Wananchi watakuwa hawana tatizo na Serikali yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wangu wamenituma nitoe shukrani za dharti kabisa kwa Serikali kwa jinsi ambavyo imetekeleza ahadi yake mapema. Ukiondoa matatizo madogo madogo ambayo ni ya kawaida, Wananchi wameshukuru na wameniambia kama utaratibu utakuwa ni huo, basi wako tayari kupimiwa hata maeneo mengine kama watalipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo matatizo madogo madogo ambayo Wananchi waliyalalamikia, lakini kama nilivyosema, yanarekebisha. Serikali ilikuwa inaendelea kuyafuatilia ili kurekebisha na hasa kwa wale watu ambao walikuwa wanakusudia kutoa maeneo ya kununua kwa gharama nafuu, wale waliokuwa kwenye maeneo yale. Wananchi hao wengi wao walikuwa wamepatiwa viwanja, lakini walikuwa wanalalamika kwamba, walitaka wakae pale pale ambapo wameacha makazi yao, lakini Serikali ilisema si lazima ukae pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali ilikuwa ni kugawa viwanja na kuwaweka watu katika maeneo tofauti tofauti ili kusiwe na mkusanyiko wa kabila moja. Ni lazima kuwe na mkusanyiko wa watu wa makabila tofauti na ndio hasa tutaweza kupata maendeleo kwa haraka kuliko kuwa watu wa kabila moja. Wananchi wangu wameelewa suala hilo na ninashukuru kwamba kazi ya Serikali imekuwa nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna matatizo madogo madogo ambayo ni lazima niyaongelee katika Wizara hii ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Kuna baadhi ya Maafisa ambao wana kasumba ya zamani wakidhani kwamba, Serikali ya zamani ndio ya sasa! Maofisa hao wana kasumba ya kudai rushwa! Nasema hivyo kwa sababu kuna maeneo mengi ambayo Wananchi wanataka wapate hati na wamelipia kama Mheshimiwa mmoja aliyetangulia alivyosema, lakini mpaka sasa hivi ni miaka mingi hawajapata hati hizo. Sana sana wanapigwa danadana wakidai kwamba Makao Makuu ndio wanaokwamisha kutoa hati hizo, maelezo ambayo kwa kweli hayana msingi.

Mheshimiwa Spika, baadaye nitampa Mheshimiwa Waziri, baadhi ya majina ya Maafisa hao ambao wapo kwenye Manispaa ya Temeke na naomba awaondoe pale, wanatuharibia jina zuri la Serikali na Manispaa yetu. Viongozi hao ambao wanaharibu sifa ya Wizara naamini kabisa nikipeleka majina yao watahughulikiwa na kwenye Manispaa yangu siwahitaji tena, naomba mtafute pa kuwapeleka. Serikali inafanya kazi nzuri halafu mtu anahari kwa sababu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Serikali kuamua kwa makusudi kutoa viwanja kwa Wananchi wake ili waweze kujenga nyumba zao, naomba Serikali ikubaliane nami pamoja na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge wengine kwamba, malipo kwenye viwanja hivyo angalau yawe kwa awamu tatu, kwa sababu ni ukweli usiofichika kwamba, Wananchi wengi hawana fedha za kuweza kulipa kwa mkupuo mmoja. Mtu huwezi kupata Sh.1,000,000/= au Sh.2,000,000/= kwa mara moja ukalipa, haiwezekani! Ninaamini kabisa haiwezekani kutokana na hali ilivyo na kutokana na kipato cha Watanzania kilivyo. Ninaamini Serikali ikiweka utaratibu mzuri wa kulipa kwa awamu tatu tofauti, Wananchi wataweza kumudu kupata viwanja na hatimaye watajenga vyumba zao, vinginevyo wengi watahindwa kuchukua viwanja hivyo kwa sababu hawana uwezo huo. Naomba Serikali iangalie suala hilo, ikiwezekana iwasaidie kwa dhati kutokana na hayo tunayowaombea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kutoa viwanja kuendane na huduma ambazo zitawasaidia Wananchi hao ambao wananunua viwanja. Nikiwa na maana kwamba, huduma hizo ziwe ni za jamii, mfano, kuwepo na shule, hospitali, barabara ambazo sasa hivi zinatengenezwa na maji. Pia, ninamwomba Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa kushirikiana na Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, waanze kupeleka huduma ya maji kwenye maeneo yale, kwa sababu Wananchi wanahitaji kujenga na ujenzi wowote hauwezi kufanyika bila kutumia maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua watasema fedha za maendeleo zilizotoka ni kidogo, lakini naamini Serikali kwa njia nyingine inaweza ikatafuta fedha za maendeleo ili Wananchi wapate huduma hiyo na watu waendeleo kujenga nyumba zao. Wengi walioonyeshwa viwanja vyao wamekwishaanza kufyeka misitu na kutengeneza viwanja tayari kwa ujenzi. Sasa, kama huduma hizo hazitapatikana watu watahindwa kufanya kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua barabara inajengwa na sasa hivi inatengenezwa vizuri tu na ukienda kule utafikiri labda tuko Marekani japo hakujawekwa lami, lakini naamini baada ya mwaka mmoja unaokuja huduma itakuwa nzuri zaidi. Naomba Mheshimiwa Waziri, akazanie suala la huduma ya maji, barabara na hospitali kama nilivyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nilisimama hapa kwa ajili ya kuipongeza Serikali, Waziri na vijana wake, lakini kilio changu kikubwa kabisa katika Wizara hiyo ni kufanya kazi kwa ushirikiano. Ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwamba, ameonyesha ushirikiano wa dhati kabisa hasa kwangu kwa sababu kila alipofanya ziara ya kutembelea kwenye maeneo yangu alikuwa ananikaribisha kwenye safari hiyo. Huo ndio tunaita Uongozi Bora na Uongozi Bora ndio jambo la msingi kwa sababu tunaposhirikiana kufanya kazi, tunaona kabisa kwamba Serikali inafanya nini na inakwama wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakutakuwa na sababu ya kuilaumu Serikali wakati tunajua kabisa kwamba kosa liko sehemu gani na ni kwa nini tatizo liko pale. Kwa hiyo, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri na timu yake, kwa kunishirikisha kwa kila ziara waliyofanya kwenye Jimbo langu. Kila eneo walilokuwa wanapima, Waziri alikuwa mstari wa mbele kuwepo kila wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji Mawaziri kama hao, tukipata kama 10 hivi, nina imani nchi hii itabadilika sana. Nimeona baadhi, lakini Waziri huyu amekuwa mstari wa mbele sana, nasema ukweli. Kila hatua inayofikiwa yeye yupo na anauliza kuna matatizo gani. Ananiambia, Mheshimiwa niitie Wananchi wako, anaongea nao na anawaelevesha, Wananchi wanatoka pale wamefurahi bila tatizo, hata kama mtu alikuwa na jazba anatoka pale amefurahi na ameelewa kwamba kweli tuko pamoja na Viongozi wetu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Viongozi wengine tuige mfano wa Waziri, kwamba kila tunapofanya kazi, basi tufanye kwa pamoja. Kufanya kazi kwa pamoja itatujengea heshima kubwa. Hata



sisi Wapinzani tunafarijika kwamba tunapotoa maoni yetu, Serikali inayafanyia kazi, lakini tunapobaguliwa nadhani inakuwa siyo vizuri. Kwa hiyo, nawashauri sana Viongozi wengine waigwe mfano huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia napenda kumshukuru Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Mheshimiwa Baraka Komisaga, amekuwa karibu sana nami katika kufanya kazi za maendeleo kwenye Wilaya yake ya Temeke na hususan kwenye maeneo ya Jimbo langu la Kigamboni. Hata wakati wote anapokuwa anatembelea kwenye Jimbo la Mheshimiwa Hadija Kusaga au kuna jambo la muhimu anaituita tukafanye kazi pamoja kwa kuwaelewesha Wananchi na Wananchi wanatuelewa vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa kwenye uongozi utaona kwamba hakuna tofauti kati ya mtu wa Upinzani na wa Serikali, wote tunakuwa timu moja kwa sababu tunahitaji maslahi ya Wananchi wa Watanzania na maendeleo ya nchi kwa ujumla. Kwa hiyo, naomba mfano huo uigwe na nitakuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba tunafanya kazi kwa pamoja na tushirikiane kwa kila linalowezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijamalizia, napenda kusisitiza katika suala la utoaji hati. Kuna maeneo yangu ya Kwamanganya, Charambe, Mbagala Kuu, Mtoni Kijichi na maeneo kadhaa ya Jimbo la Kigamboni, wamepimiwa maeneo yao muda mrefu na wengine wamejenga, lakini wamepewa *offer letters* tu, hawana hati kamili. Sasa hivi wana zaidi ya miaka 30, sijui kinachoendelea, labda nimwulize Mheshimiwa Waziri, tatizo ni nini kwa kutowapa watu hawa hati wakati wamekwishalipia kwa muda mrefu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nimesema kwamba, kuna baadhi ya Viongozi wetu pale Manispaa ambao wana matatizo ya kukwamisha mambo kwa makusudi. Wana madai yao ambayo yanakuwa ni ya msingi, hata mteja akitimiza yale masharti bado mteja huyo anazungushwa! Sasa, kuna watu mpaka wamekuja kuniambia kwamba, bwana tumechoka, tukwambie ukweli, nikasema hebu niambieni. Wakasema, fulani tulimpa Shilingi kadhaa sasa hivi ni mwaka wa pili, hajatushughulikia suala letu, tukimwuliza anasema suala liko Mahakama Kuu! Nimesema wazi kwamba, hawa watu majina yao ninayo, nitampa Waziri na ninaomba hao watu kwangu waondolewe watafute sehemu nyingine ya kuwapeleka, siyo kule. Hatuwezi kufanya kazi na watu ambao wanatuharibia sifa na huduma ya Manispaa yetu ya Temeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naomba kuunga mkono hoja na ninakushukuru sana. *(Makofi)*

#### MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. JUMA S. KIDUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza Wizara kupitia kwa Waziri wake mahiri, Mheshimiwa Gideon Cheyo, pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, wakishirikiana vizuri na Katibu Mkuu na timu ya Wataalam. Kwa pamoja, timu hii imeleta mabadiliko makubwa na kwa muda mfupi katika upimaji na usimamizi wa uendelezaji wa ardhi kwa ujumla nchini.

Hivyo, ninalazimika kuiunga mkono hoja hii moja kwa moja. Naomba hata hivyo nitoe mchango mdogo wa kuboresha hotuba hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakipongeza Chuo cha Ardhi cha Morogoro kupitia kwa Waziri, kwa kukubali ombi la kuja Wilaya mpya ya Kilindi na kufanya mazoezi yao ya vitendo kwa kupima Mji mdogo wa Songe, ambao ni Makao Makuu ya Wilaya ya Kilindi. Kitendo hiki kimetupunguzia sana gharama za upimaji. Aidha, Wataalam wa Chuo hiki wanapima pia Mji Mdogo wa Kwediboma Wilayani Kilindi. Tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Wizara kwa kutatua mgogoro wa mpaka kati ya Wilaya ya Handeni (Kilindi) na Kiteto kati ya Mlima Nkhama na Mlima Gitu (Loskitok) kwa kutumia GN ya mwaka 1961. Hata hivyo, ili kukamilisha kazi ya kuondoa utata kati ya Mkoa wa Tanga na Manyara (Arusha ya zamani), naomba GN hii iendelezwe kati ya Mlima Gitu (Loskitok) hadi Buiko kama

ilivyoonyeshwa katika GN hii. Marekebisho haya yatasahihisha makosa ya GN iliyotumika kuiunda Wilaya ya Simanjiro mwaka 1993, ambayo imemega sehemu kubwa ya Mkoa wa Tanga. Naomba marekebisho haya yafanyike mapema ili kuepuka migongano isiyo ya lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kuunga mkono hoja hii.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nizungumzie nyumba za Serikali za NHC, ambazo Serikali ilitoa kibali ziuze/zinunuliwe na wale waliokuwa wanaishi kwenye nyumba hizo kwa wakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako wananchi ambao walipatwa na matatizo. Kwa mfano, nina watu ninaowafahamu ambao walikuwa watumishi wamefariki kabla taratibu za kununua hazijakamilika. Kilichofanyika ni kuwanyima warithi kununua hizi nyumba. Hili mimi naliona kama ni kutowatendea haki familia za marehemu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako pia wanawake ambao wameuzwa wakiwa kwenye nyumba za NHC na familia zikahangaika. Kwa kuwa nchi yetu ina uongozi unaosimamia haki za binadamu, nashauri watu hawa wasio na uwezo wasaidiwe ili wasikose makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imekiri kwamba Miji inapanuka haraka, upimaji wa viwanja na kuweka miundombinu upewe kipaumbele katika Wizara na Idara za Ardhi na Mipango Miji kote nchini. Utaratibu ukiwa mzuri, kule Wilayani tutakuwa na kazi ndogo ya kuelezea na kukubaliana kutenga fedha za kupima haraka maeneo yanayokua haraka na kuonyesha kwamba yanaelekea kuvutia makazi ya watu wengi. Aidha, mtazamo wa mbali, ningeshauri vijiji vikawa vinapangilia mipango ya matumizi ya ardhi badala ya kujivunia vibali vya kumiliki ardhi na kuitoa kwa yeyote tu. Vijiji vingine sasa havina tena ardhi ya akiba kwa shughuli zinazoweza kujitokeza mfano, mahitaji mapya ya shule, zahanati na soko au magulio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. HALIMENSHI K.R. MAYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malalamiko ni juu ya viwanja vipya huko Dar es Salaam, hizo bei ni kubwa sana. Serikali sehemu zingine hugharamia viwango. Kulipia shilingi 2,500,000/= kabla ya kujenga ni gharama kubwa. Kiwanja changu kipo Mbweni, naomba asipewe mtu mwingine mpaka nitakapolipia kidogo kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabwana Ardhi walioko katika Halmashauri au Wilaya hawana vitendea kazi wala pesa. Je, hilo lipo katika Halmashauri zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba wapewe ruzuku yao moja kwa moja ambayo Waheshimiwa Wabunge watajulishwa moja kwa moja ili ufuatiliaji wao uwe wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hatimiliki zinazotolewa kwa sehemu kama Dar es Salaam na Mwanza na baadhi ya watu wamekata tamaa. Hivyo hatimiliki ziwepo kwa kila Mkoa.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na nawatakia utekelezaji mwema wa Bajeti mliojipangia kwa mwaka wa fedha 2003/2004. Mola awabariki kwa kazi ngumu na nzuri ya kuwaandalia Watanzania makazi bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa ushauri ufuatao:-

Fedha za upimaji wa viwanja maeneo ya Mijini yapimwe mapema ili kupambana na makazi holela (*squatters*) katika maeneo ya Miji yetu Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa waliouziwa nyumba zilizokuwa za *NHC* hasa kwa watumishi waruhusiwa kuwa wanakatwa kwenye mishahara yao baada ya kutoa malipo ya awali. Katika Jimbo langu wapo watumishi ambao wameuziwa nyumba lakini inawawia vigumu sana kulipa kwa *cash*. Naomba sana Wizara ifikirie namna ya kuwasaidia wananchi hawa kukidhi mahitaji yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii na naomba ushauri wangu uzingatiwe.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze kwa kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Gideon Cheyo, Naibu Waziri, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Katibu Mkuu na Wataalam wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya. Hongereni sana. Pia napenda kutamka kwamba, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ushauri kwa mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kupatiwa viwanja kwenye mashamba katika maeneo mapya yanayopimwa. Naomba kuelimishwa kuhusu kero sugu iliyopo kwenye Vijiji na Miji yetu kwa wenye mashamba kupatiwa viwanja wakati maeneo yao yanapochukuliwa na Serikali ili kupimwa viwanja vipya. Yapo malalamiko kwa wananchi kuhusiana na suala hili. Naomba kupatiwa ufafanuzi wa wananchi hawa ambao kwa zaidi ya miaka 20, 30 au 50 wanaishi kwenye maeneo hayo, lakini wakati wa kugawa viwanja vipya wananchi hao wananyimwa. Mimi naishauri Serikali iwajali wananchi hawa hata kwa kuwapatia viwanja viwili au vitatu kwa utaratibu wa kisheria. Yapo manung'uniko makubwa sana kwa wananchi hasa katika Miji mipya inayojengwa kama Korogwe na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hati za kumiliki viwanja ziongezewe muda hasa hizi za miaka 33. Nashauri sheria ya kumiliki ardhi kwa miaka 33 ifikiriwe kubadilishwa ili ifikie angalau miaka sitini, umri wa mfanyakazi kustaafu. Miaka 33 imepitwa na wakati, toka wakati unapata kiwanja na kuanza kujenga miaka 33 itakuwa imekwisha. Siyo hivyo tu pamoja na ruhusa ya kuomba tena kujenga, siyo rahisi mwananchi kukumbuka kuomba. Kuna wageni wengi wanapewa miaka 99 sioni sababu kwa nini wenyeji nao wasipewe miaka 99.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sheria ya Ardhi Vijijini, nashauri iendelee kuelimishwa kwa wananchi. Sheria hii ni ngumu kueleweka. Juhudi ziendelee za kuwafanyia semina wanavijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa nyumba usiofuata taratibu za mipango Miji, zipo nyumba na majengo mengi nchini yaliyojengwa kinyume na *Master Plan*. *Open space* kujengwa, maeneo ya viwanja vya michezo kujengwa majengo. Hali hii imefanya Miji mingi kukosa viwanja vya michezo. Hii inafanywa na wafanyakazi ambao sio waadilifu. Nashauri hatua kali zichukuliwe kukomesha tabia hii. Wafanyakazi waliosababisha vitendo hivyo wachukuliwe hatua kali za kinidhamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *Land Use*, wasioendeleza mashamba makubwa ya kilimo kama vile mashamba ya mkonge yasiyoendelezwa wanyimwe Hati. Haiwezekani watu wamekabidhiwa ardhi waiendelee lakini wanashindwa kuiendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ijitahidi kutafuta mkakati wa kusaidia wananchi kujenga nyumba bora na za kisasa kwa bei nafuu kwa kutumia teknolojia rahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ya mpangaji na mwenye nyumba irekebishwe. Hali ilivyo sasa mwenye nyumba hana usemi ila mpangaji ndiyo mwenye haki zaidi. Hali hii haipo *NHC* tu bali hata kwa wenye nyumba binafsi, pamoja na Mikataba ya kulipa lakini wapangaji ni wagumu kulipa pango. Wizara itunge sheria mpya ya kuwabana wapangaji.

**MHE. LUCAS L. SELELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Pamoja na hayo nilikuwa na wasiwasi juu ya ardhi itakayogawiwa kwa wawekezaji wa nje kama vile mashamba. Tunawatayarisha vipi wananchi (wakulima) wetu kuiuza ardhi kwa thamani ya kutosha? Kuna ardhi gani iliyotengwa maalum kwa ajili ya wawekezaji hao wenye pesa na zana kuliko wakulima wetu. Ardhi

(mchanga) unaopelekwa nje ya nchi (Japan) pamoja na madini inathamanishwa vipi na eneo hilo linapata fidia gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate ufafanuzi juu ya haya kwani ni kero. Nawatakia kazi njema.

**MHE. ESHA H. STIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Gideon Cheyo, Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, kwa hotuba nzuri aliyoiwasilisha Bungeni na hali kadhalika nampongeza Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa maandalizi ya hotuba hiyo kwa umakini na mwelekeo madhubuti wa hotuba hiyo, naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupatiwa ufafanuzi wa masuala yafuatayo ambayo yamekwamisha wananchi wengi katika kupata mikopo na hati za nyumba walizouziwa na Shirika la Bima na *NHC* hapa Dodoma na Shinyanga.

Moja, utoaji wa hati ya kumiliki eneo alilonunua mtu kwa nyumba zenye *compound* moja kwa familia kuanzia mbili hadi nne, Ofisi ya Msajili hapa Dodoma inawazungusha sana watu kwa kutupiana mpira nenda *CDA* na *CDA* wanasema nenda kwa Msajili ndiyo wenye mamlaka ya kutoa hati na kadhalika. Ni usumbufu kwa wananchi nikiwemo mimi (Mheshimiwa Esha Stima), kama Mbunge, bado sijapewa hati kwa mizengwe hiyo. Naomba kupata ufafanuzi au utekelezaji wa masuala ya hati ukoje au tatizo ni kitu gani?

Pili, naishukuru sana Wizara hii kwa jinsi wanavyowasaidia akinamama wajane na wengine wenye uwezo mdogo kwa kuwapa mikopo ya nyumba. Lakini kuna tatizo moja linalowakwaza waombaji wa mikopo hiyo kwa kuhitajika kuwasilisha hati ya nyumba anayoombea mkopo. Hati ya Nyumba ya Serikali/Taasisi (za Bima na *NHC*), zinatunzwa na Serikali, je, huyo mwombaji ataipataje na ukizingatia ni nyumba zenye kukaa familia zaidi ya mbili. Naomba kikwazo hiki kitolewe kwa sababu wanaokopeshwa ni watumishi wa Serikali na nyumba ni za Serikali. Sidhani kama kunaweza kutokea hujuma zozote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Gideon Cheyo, Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Naibu wake Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Katibu Mkuu, Bibi Salome Sijaona, Wakuu wa Idara na Taasisi pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara/Taasisi zake kwa hotuba nzuri sana na yenye takwimu nyingi kuhusu mipango, utekelezaji na hatua mbalimbali za kuhusu matumizi bora ya ardhi, udhibiti wake, pamoja na mapinduzi katika maendeleo ya makazi. Pamoja na hayo, ningependa kuchangia kama ifuatavyo.-

Kuhusu gharama ya ardhi, pamoja na hatua ya kutambua umuhimu wa ardhi na kuipa thamani kwa ajili ya uwekezaji kwa maeneo fulani, ada ya ardhi ni kubwa mno. Kwa mfano, hata pamoja na kupunguza kodi ya ardhi kutoka shilingi 6,000/= hadi shilingi 2,000/= kwa hekta kwa mwaka, kodi hii bado iko juu kwa wawekezaji katika mashamba ya mkonge. Uwekezaji katika mashamba ya mkonge unahitaji ardhi kubwa sana. Aidha, ulimaji wa mkonge unalazimu sehemu kubwa ya ardhi kuachwa wazi kwa muda mrefu (*Fallow*). Hivyo, kodi inayotozwa sasa bado ni mzigo mkubwa ambao unawakatisha tamaa wawekezaji katika sekta hii. Nashauri Wizara ilitazame upya suala hili ili kuwapunguzia kero wawekezaji katika Sekta ya Mkonge na kuiwezesha sekta hiyo kufufuliwa na kuendelea kwa kasi kubwa zaidi.

Kuhusu ufinyu wa ardhi Kata ya Maramba na Mhindwa, nimefarijika kuona kwamba, baadhi ya vijiji katika Jimbo la Mkinga Wilaya ya Muheza ni miongoni mwa Vijiji vyenye *plan* za upimaji. Hata hivyo, Vijiji vingi katika Kata za Maramba na Mhindwa vina upungufu mkubwa sana kwa ajili ya kilimo cha wanavijiji na maendeleo ya makazi kutokana na Kata hizo kuzingirwa na hifadhi ya misitu, mashamba ya mkonge, mashamba ya Jeshi la Kujenga Taifa na Shamba la Mbegu la Mwele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba shughuli hizo nyingine nazo pia ni muhimu katika kuchangia maendeleo ya Taifa kwa jumla, wananchi wa Vijiji vinavyopakana na maeneo hayo wanakabiliwa na tatizo kubwa la ardhi kwa ajili ya kilimo chao cha kuwawezesha kujikimu na kuchangia katika Pato la Taifa na hivyo kutokuwa na fursa ya kushiriki katika mapambano ya kupiga vita umaskini. Aidha, inakuwa shida kwao kujenga makazi mapya na bora na pia majengo mengine kwa shughuli za maendeleo ya jamii kama vile shule, zahanati na kadhalika.

Hivyo, nashauri Wizara itazame upya *plan* za upimaji katika Kata hizi ili kuweza kupata ufumbuzi ufaao kwa manufaa ya wananchi na wadau wengine wote husika katika suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi nyingi sana kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Makamishna, na Watendaji mbalimbali wa Wizara hii, hongereni sana kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upimaji wa Vijiji, inaonyesha juhudi za Serikali kupima Vijiji, ramani si nguo ni kipimo cha mipaka kina sheria na watu wakivuka ni kosa. Orodha ya Vijiji vinavyotajwa katika jedwali la tano kuna Vijiji 2527 uk. 96. Wilayani Morogoro uk. 75 - 77 katika Vijiji 60 vya Morogoro Na. 1370 - Na. 1429. Vijiji hivi 60 ni Kijiji kimoja tu Na. 1422 (Tandai) Kata ya Kinole, Tarafa ya Mkuyuni. Lakini 38 Jimbo moja na 21 Jimbo lingine. Hii inasikitisha, kwa nini niunge mkono hoja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ubinafsishaji wa Ardhi, ubinafsishaji wa mashamba makubwa kama ya Mkonge, ngano, shairi, mbuga za hifadhi ya wanyama, mashamba ya chai. Kama wanaacha mapori, wananyanyasa wenye ardhi (Watanzania). Mashamba hayo yataifishwe na walio dhinisha au kutoa vibali maeneo hayo, wafungwe na mashamba yarudishwe Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kupanuka kwa Miji, imezuka tabia ya Miji kupanua mipaka ili kupata viwanja. Kwa nini wakazi wa Miji, wasiombewe viwanja katika Vijiji vilivyopo jirani na Miji hiyo badala ya tabia mbovu, mbaya na inayozoeleka hivi sasa ya Miji kujitana na kumeza Vijiji na hata mashamba kufa. Badala yake Vijiji hupungua na Miji kukua bila ya sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kodi za Ardhi ya Mijini, kuna kodi nyingi sana Mijini za ardhi ambazo ni kero, majengo, kiwanja, *Property* na kadhalika. Naomba sana kwa sababu zinakera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kodi kero za ardhi ziondolewe. Halmashauri zinazopanga kodi hizo zipitie Wizara yako ili ziratibiwe na kama ni kero zishauriwe ziachwe kupunguza kero za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuhamia Dodoma, Bajeti ya mwaka huu naomba sana sana Wizara hii ihamie Dodoma. Naomba Wizara itamke itahamia lini Dodoma au hamtaki? Naomba sana hamieni Dodoma muwe wenyeji wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni halali kwa viwanja, nyumba, mashamba kuuzwa kwa kutumia Madalali? Naomba jibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba orodha ya viongozi wa Wizara hii kuanzia Waziri hadi Kamishna. Je, utanipatia ili niwaandikie barua au kadi za pongezi? Viwanja vya Michezo vina hati nchini? Afisa Ardhi Mkoa badala yake kuna ngazi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza kupima Kijiji kimoja bila ya kushirikisha Vijiji vinavyozunguka. Mfano ukipima Kijiji cha Igalula mipaka na Vijiji jirani vinashirikishwaje kama jirani yao au wanashtukia mawe tu au Vijiji jirani navyo vinapendekeza mipaka yao na Igalula?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mtu amenunua nyumba au kiwanja chenye hati, utaratibu gani unatumika kubadilisha Hatimiliki ya eneo?

**MHE. DR. BATILDA SALHA BURIAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, pamoja na Wataalam, wakiongozwa na Katibu Mkuu, Mama Salome Sijaona, kwa kazi nzuri sana Wizara inayofanya. Kusema ukweli Wizara hii imepiga hatua kubwa sana katika kutekeleza mipango ya kazi na hususan katika kuboresha utendaji kwa kuimarisha Teknolojia ya Habari (*IT*) katika kuleta tija na ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningependa kuchangia katika maeneo makubwa manne.

Umuhimu wa kuboresha shughuli za utayarishaji ramani. Nashukuru kuona kwamba Wizara ina mikakati ya kuboresha jengo hilo la Ramani, kwani upatikanaji wa Ramani za msingi (*Base Maps*) ni muhimu sana katika kuandaa mipango ya maendeleo ya kimkakati (*Strategic Development Plans*). Vile vile gharama za kupiga picha kwa angani (*Aero Photographs*) ni ghali sana, picha moja inagharimu si chini ya dola za Kimarekani 1,000.

Hivyo, ili kuimarisha Idara hii ya Ramani na kuhakikisha kwamba shughuli za *GIS* zinaimarika kwa faida na kwa maendeleo ya nchi hii, Wizara haina budi kutoa kipaumbele kwa kuongeza fedha na mafunzo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Wizara kwa jitihada za kupima na kugawa viwanja kwa ajili ya makazi. Hata hivyo, jitihada hizi za kupima viwanja 20,000 kwa ajili ya makazi, itabidi iwe ni *Demonstration Project* na hivyo kupitia *experience* hii tuweze kuangalia uwezekano wa kujifunza na hivyo kuimarisha huduma zaidi ikiwa ni pamoja na kupunguza gharama nzima za upimaji.

Nchi kama Sri-Lanka iliweza kuwa na mkakati wa nyumba milioni moja mwaka 1989 na kufanikiwa, je, inakuwaje sisi Tanzania tushindwe kupima viwanja laki tano au hata milioni moja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuanzisha mfumo wa kukopa fedha kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa nyumba, jambo hili limekuwa likizungumzwa tangu mwaka 2000. Nafurahi kuona kwamba jitihada zimekwishaanza kufanyika, ikiwa ni pamoja na kupata ushauri wa kitaalam kutoka *UN-HABITAT*. Hivyo napenda jitihada hizi ziharakishwe ili basi wananchi waweze kupata mikopo kwa ajili ya ujenzi wa makazi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mafunzo kwa wataalam. Katika kiambatisho (13 a) inaonyesha jumla ya watumishi waliohudhuria mafunzo mbalimbali katika kipindi kilichopita, kusema ukweli, idadi hii ni ndogo sana. Hivyo basi, naomba Wizara hii na Serikali kwa ujumla, ione umuhimu wa kuongeza idadi ya watumishi watakaofaidika na kozi mbalimbali. Umuhimu au kipaumbele kitolewe kwa mafunzo ya *GIS* na *Software Engineering*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache naomba kuungana na Wabunge wenzangu, kuunga mkono hoja hii na pia nazidi kuipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri inazozifanya. Ahsante.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, kwa kazi nzuri na ngumu wanayofanya. Pamoja na hayo, ninaomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

(a) Kwa kuwa Wizara imeunda Kamati za kugawa ardhi katika Wilaya 102, Karatu ikiwa moja wapo, ninapenda kupata ufafanuzi Kamati hii inahusika na ugawaji wa ardhi ipi hasa, ikizingatiwa kuwa kwa Sheria Na. 4 na 5 mamlaka sasa yanakwenda kwa wamiliki husika yaani vijiji na Mamlaka ya Miji na Manispaa. Tatizo limejitokeza hasa Karatu, ambayo ina mashamba yanayoitwa ya mkataba na miaka yote, maeneo hayo yamekuwa hayako chini ya mamlaka yoyote, ni kama wako hewani. Je, Kanuni za kuendesha Kamati hizo zimekwishatungwa au wanatumia Kanuni zipi?

(b) Kwa vile kazi ya upimaji viwanja na hasa vijijini inakwenda polepole sana na kwa kuwa umiliki ni muhimu katika kuendeleza ardhi, ikiwa ni pamoja na kuitumia kama *mortgage*, je, Serikali wakati inaendelea kuandaa Wataalam wake wapime, inaweza ikatumia au kuruhusu wapimaji binafsi kufanya kazi hiyo angalau kwa mkataba? Hii itaondoa uwezekano wa wapimaji hao kufanya kazi hiyo kwa mlango wa nyuma.

(c) Majengo yetu mengi yaliyojengwa na au yanayoendelea kujengwa, hayazingatii mahitaji maalum ya walemavu. Kwa vile, *access* ni haki muhimu kwa wote, hasa majengo ya umma ambayo mengi ni ya ghorofa, je Wizara ya Ardhi, ambayo ndiyo yenye majukumu ya kutoa *building permit*, inaweza kutoa mwongozo au kanuni inayotaka nyumba zote zitakazojengwa ziwe *Disabled Friendly* na zote au michoro yote ambayo haiendani na sharti hili muhimu wanyimwe *Building Permit*! Ninaamini kabisa mwongozo wa aina hii utakuwa wa msaada mkubwa kwa jamii yetu hasa ndugu zetu wenye ulemavu wa viungo na wa aina nyingine yenye kuhitaji msaada maalum katika matumizi ya majengo ambayo ni *Disabled Friendly*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kwa kuwapongeza kwa kazi nzuri hasa kuniondolea tatizo la siku nyingi Wilayani Karatu ya kutokuwa na Bwana Ardhi wa Wilaya. Natumaini mambo mengi yaliyosimama, ikiwa ni pamoja na ubatilishaji wa mashamba ya mikataba ambayo haitumiki vizuri, kubadilisha matumizi ya mashamba ya mkataba bila kufuata utaratibu sasa yataisha. Nashukuru sana.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Serikali imeweka utaratibu wa kupima viwanja mijini, hasa Dar es Salaam, ambapo *green belt* yote imemezwa. Nashauri Serikali iweke eneo la *green belt* mijini, hii itasaidia wakulima wadogo kujijiri kwa vijana wengi walio mijini, lakini vile vile *green belt* itasaidia kupunguza gharama ya mboga mijini. Aidha, katika karne hii ya 21, Serikali ingekuwa inapanga kujenga *satellite towns*, badala ya kupima viwanja vidogo vidogo vya *high medium* au *low density*? Ni lazima twende na wakati. Tukiachia hivi, Jiji la Dar es Salaam litafika Kibaha, Bagamoyo na hata Mkuranga. Narudia, twende na wakati.

Pili, Serikali itoe utaratibu wa watu walionyanyanywa viwanja bila utaratibu. Sio haki mtu kupitia kiwanja halafu unakuta kiwanja kimejengwa. Mlalamikaji anapeleka malalamiko kwa Kamishna na hakuna jibu. Hiyo sio dhuluma? Kwa nini wahusika wasiwajibike pale wanapogawa viwanja bila kumpa taarifa aliyekuwa analipia? Hii ni dhuluma na Serikali ya CCM haiwezi kuendeleza au kuachia dhuluma hizi.

Tatu, ardhi ni mali na raslimali kuu ya Mtanzania. Ni vema Serikali ikadhibiti mafanikio ya wageni ambao wanataka kujipatia ardhi. Wanavijiji wengi hawaelewi ulaghai wa wageni, hivyo wanagawa tu ardhi bila kuzingatia utaratibu. Ni vema wawekezaji wote wapitie Mkoani ili vibali vya vijiji vitathminiwe ili maeneo yasigawiwe ovyo. Mfano dhahiri ni fukwe za Bahari ya Hindi, eneo lililo karibu na Hifadhi ya Saadani ni mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa hotuba nzuri na kurekebisha hali mbaya iliyokuwepo ndani ya Wizara hii miaka iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi pia kwa Mheshimiwa Naibu Waziri na Viongozi wote na Watendaji ambao wanamsaidia Mheshimiwa Waziri kukabili migogoro iliyokuwepo ndani ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utaelekea katika maeneo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya upimaji viwanja inahitaji vifaa na vifaa bora vya kisasa. Bado Wizara hii haina vifaa vya kutosha kiasi kwamba, Afisa Ardhi wa Wilaya ya Handeni au Muheza, analazimika kufuata vifaa hasa darubini kutoka Dar es Salaam kwa kuazima ili akapime kiwanja Segera na kurudisha vifaa Dar es Salaam. Utaratibu huu ni ghali sana na ni watu wachache tu wenye uwezo wamemudu kuchangia gharama hizo na kupimiwa viwanja. Wasio na uwezo hawapimiwi.

Pili, asilimia 20 ya kodi ya ardhi Kiambatanisho (1) alichobambanisha Mheshimiwa Waziri, kinaonyesha kwamba Halmashauri za Kodi ya Ardhi. Inawezekana ni Waheshimiwa Wabunge, wachache ambao Halmashauri zao zinaweka mambo wazi, wanajua kwamba Wizara inatoa fedha hizo kwa Halmashauri. Ili kuweka mambo bayana, nashauri taarifa za mgao wa fedha hizo zitolewe kila baada ya nusu mwaka kwa Waheshimiwa Wabunge, ili waweze kusimamia matumizi bora ya fedha hizo katika kuendeleza upimaji wa viwanja na maendeleo ya makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri nyingi fedha hizo hazijulikani zinafanya kazi gani. Sana sana hutumika katika shughuli zisizo za maendeleo.

Tatu, utaratibu wa kutoa barua za Toleo (*Letter of Offer*). Naipongeze sana Wizara kwa kuanzisha utaratibu wa kutoa Barua za Toleo zenye namba maalum na kutoa Hatimiliki kwa kutumia kompyuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu unaelekea kwenda vizuri katika Mkoa wa Dar es Salaam. Nafahamu kwamba, Tanzania ni kubwa sana, lakini je, Mheshimiwa Waziri, ana mpango gani wa kuendeleza mpango huo Wilayani ambapo Barua za Toleo (*Letter of Offer*) kwa viwanja zinazotolewa. Tunategemea Mheshimiwa Waziri, atatoa dokezo la mpango wake huu wa uboreshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. AISHA O. KIGODA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo, pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Tatu M. Ntimizi, kwa hotuba yao nzuri. Nawapongeze sana watumishi wa Wizara hii chini ya Uongozi wa Katibu Mkuu, Bibi Salome Sijaona.

Pili, Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Baada ya hapo nachangia maeneo yafuatayo:-

Kwanza, upimaji wa viwanja 20,000 Jijini Dar es Salaam. Naipongeze Wizara kwa kubuni mpango wa upimaji wa viwanja jijini ili kuwe na utaratibu mzuri wa kupunguza kero kwa wananchi, vile vile kuupanga mji katika sura inayokubalika. Vile vile ili Wizara iweze kupata fedha za kuweza kuboresha huduma muhimu kuwezesha wananchi waweze kuwa na uhakika wa umilikaji wa viwanja vyao hasa kwa vile utoaji wa hati haucheleweshwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi, bei ya viwanja hivi ni kubwa sana kama kweli tunataka wananchi wote waweze kununua viwanja hivi, kwani bei zote kuanzia viwanja vya sifa za *Low Medium High Density* kwa hakika ni kubwa. Hivyo, tunaomba ziangaliwe upya. Kwa vile pia sababu za kupanga bei hizi ili kupata fedha zitakazosaidia upimaji na ujenzi wa huduma muhimu za wana makazi wa sehemu ile, basi nashauri waruhusiwe kulipa kwa *installment* maalum, mathalan atoe asilimia 25 ya bei mara apatiwapo kiwanja na 75% ailipe katika utaratibu wa awamu kama itakavyokuwa imepangwa lakini isizidi miezi 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna urasimu mwingi na usumbufu usio wa kawaida kwa watoaji wa hati za Viwanja hasa mawilayani usio wa kawaida. Tunashauri Wizara iwaagize watumishi wa Ardhi wahakikishe wanaharakisha zoezi hili badala ya kutoa sababu kuna Wizara inatukwamisha! Au ni kweli kwa wakati huu hati za Wilayani Tanzania nzima lazima zipitie Wizarani kwa uthibitisho? Kama ni kweli Waziri una utaratibu gani wa kuboresha tatizo hili kwani kama wote tunavyofahamu, kuwa na hati, iwe ya kiwanja au umiliki wa ardhi, ni dhamana inayoweza kukupatia mikopo kwa shughuli za maendeleo.

Nalipongeze Shirika la Nyumba, kwa juhudi zao za kujenga nyumba ili waweze kuwapatia makazi mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nia hii nzuri, bado bei za nyumba hizi ni kubwa na wananchi wenye kipato kidogo wanashindwa kununua, hivyo wengi wanaochukua ni aidha wageni au wenye fedha nyingi, nashauri kuwa wananchi waweze kuruhusiwa kulipia kwa awamu au kujenga pia nyumba za *Low Cost*.



Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine ni kuwa Shirika la Nyumba liangalie wapangaji wa nyumba zao. Haiwezekani mtu apange nyumba, hasa akiwa mfanyakazi, kupanga nyumba hiyo hiyo kwa zaidi ya miaka 20, ukizingatia kuwa mara nyingi mtumishi huwa anahamishwa katika uhai wa utumishi wake. Uko udanganyifu na Wizara inafahamu hili, wa wapangaji kuzihodhi zile nyumba na kuzifanya zao na kuzipangisha. Ukienda *N.H.C.* kuomba nyumba unaambiwa nenda kazunguke ukiona nyumba iko wazi njoo unipe taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu haya yanakera na kukatisha tamaa, kwani inatoa picha kwamba, aidha *N.H.C.* menejimenti haijui nani *tenants* wao au wanataka wanaotaka kupanga wazunguke mlango wa nyuma. Mheshimiwa Waziri na Naibu wako, kwa vile utendaji wenu mzuri tunaufahamu wote, nadhani suala hili mtatusaidia lirekebishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. REMIDIUS E. KISSASSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema naunga mkono hoja hii na nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake yote, kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo napenda kuchangia machache kama ifuatavyo:-

Kwanza, nashauri masuala ya *master plan* miji na vijiji yafanywe kwa kutumia wataalam wetu kutoka Vyuo vya Ardhi na hata watu binafsi ili kustawisha miji yetu. Chuo Kikuu Kishiriki cha Ardhi kitumiwe kikamilifu ili miji ianze kupendeza.

Pili, utaratibu maalum uwepo wa kutenga maeneo maalum ya wafanya biashara wadogo wadogo na kwa utaratibu maalum ili wasichafue mazingira, lakini vile vile wawe sehemu ya ukuaji wa miji na sio kipingamizi.

Tatu, suala la kuwa na Benki Maalum ya Nyumba ni muhimu sana kwani hivi gharama za ujenzi ni kubwa mno. Ni wajibu wa benki hii kufuatilia na kuhamasisha wananchi wanaotaka mikopo ya ujenzi ili kuboresha huduma hiyo.

Nne, suala la *site and services* ni la msingi sana kwa kila eneo litakalopimwa. Hivyo, Wizara hii iratibu suala hili na Mawizara mengine ili kila moja ichangie wajibu wake tangu biashara, maji, umeme na kadhalika. Hii iwe ni kwa nchi nzima.

Baada ya kusema hayo, narudia kuiunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kueleza kwamba naunga mkono hoja.

Napenda kueleza machache kuhusu Wizara hii. Wizara hii ni muhimu sana ndiyo maana kuna migogoro ya hapa na pale katika kila kona ya nchi yetu. Migogoro ya ardhi iko ndani ya jamii, Kijiji, Wilaya hata ndugu na ndugu hugombania ardhi. Kwenye maeneo mengi migogoro ya mipaka imeenelea mwaka hadi mwaka.

Upimaji ni jambo muhimu sana kutatua migogoro hasa katika vijiji na kijiji na mashamba na maeneo ya mashamba ya wafugaji. Nashukuru Wizara kutoa elimu kwa wananchi hasa baada ya kupitisha Sheria ya Ardhi ya Vijiji na ardhi ya jumla, hilo limeeleweka kilichobaki ni upimaji.

Napenda kuikumbusha Wizara kupima maeneo ambayo hayakupimwa kwani migogoro inazidi katika maeneo ya wafugaji baada ya wakulima kuvamia maeneo mengi kwa kuwa ardhi imepata thamani baada ya kupitishwa Sheria ya Ardhi, inafaa sasa ardhi yote ipimwe ili kila mwananchi aliyeko katika ardhi ya nchi hii afaidike na sehemu aliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo ambalo halijaeleweka sana kwa wananchi ambalo ni ardhi inayomilikiwa kimila. Utaratibu huu unahitajika sana kwani maeneo mengi yametengwa kwa ajili ya umiliki kimila lakini hawajui namna ya kupata hati ya kumiliki eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Jimboni kwangu hawakufaidika na ardhi yao kwa sababu hawakupimiwa maeneo. Naomba hilo lianze kufanyika huko kwenye Jimbo la Longido. Nyumba ambazo Serikali inatoa kwa wananchi kwa bei nafuu au kwa kuuziwa hilo linasikika kama jambo geni kwao. Naomba utaratibu wa kujenga nyumba na kuuza nao wapate mradi huo.

Pia naomba kukumbusha vijiji vilivyopimwa na *NGO* ya *CORDS* kwenye Jimbo la Longido na kuleta maombi Wizara iwapatie vyeti vyao ili waweze kutumia kwenye maeneo yao.

Jambo lingine ni upimaji wa viwanja. Wananchi wengi wanahitaji kupimiwa viwanja ili wapate kunufaika na mikopo kwenye taasisi za mikopo, upimaji wa viwanja ni ghali sana. Naomba gharama hii ipunguzwe, kupima shamba eka moja ni Sh.80,000/=, hii ni ngumu sana kwa wananchi.

Naomba Wizara yako waelekeze macho tena kwenye Jimbo la Longido kwani wamebaki wakisikia huduma za Serikali bila kufaidika, wanahitaji upimaji wa vijiji, mashamba, viwanja na nyumba bora. Jimbo langu liko mpakani na Kenya upande wa Kenya maeneo yote yamepimwa kwao, wananchi wao wanawacheka Watanzania kwa kuwa hawafaidiki na ardhi yao. Hii imekuwa ni aibu kwa Serikali yetu kwamba wamewaacha wananchi wao bila kupata hati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba yako, lakini naomba majibu.

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumshukuru kwa dhati Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Gideon A. Cheyo, kwa hotuba yake nzuri kuhusu Bajeti ya mwaka 2003/2004. Kwa uzito huo huo, natoa pongezi nyingi kwa Naibu Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Katibu Mkuu, Makamishna wote na watumishi wote kwa ujumla, kwani wote wameshiriki kwenye maandalizi ya hotuba hiyo.

Mchango wangu kwenye hotuba hii ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, kutokana na matatizo makubwa ya Mipango Miji, matatizo ya upungufu wa wataalam, uwezo mdogo wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza, makazi ya Wana-Mwanza Mjini ni yale yasiyo rasmi. Naiomba Wizara ichukue nafasi ya pekee kuisaidia Mwanza ki-makazi. Mapungufu ya mipango miji yafufuliwe ili wananchi wapewe viwanja rasmi. Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, ndiyo yenye dhamana ya ardhi nchini na inapaswa iwe kiongozi kwenye kuweka utaratibu mzuri wa jinsi wananchi kote nchini watakavyokaa kwa mpangilio mzuri. Naiomba Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, kwa utaratibu huo huo wa Jiji la Dar es Salaam, wananchi wa Mwanza na Jiji hilo kwa ujumla, Wizara iwapatie nao mradi wa kupimiwa viwanja vya makazi na shughuli nyingine.

Pili, tatizo kubwa la wakazi wa maeneo mengi ni kuhamishwa kutoka maeneo yao kwa maelezo kwamba eneo hilo sasa limepimwa. Je, tatizo hili hasa hasa linaletwa na Maafisa wa Ardhi? Maafisa wana kiburi na hawana majibu mazuri kwa wananchi! Kwa mfano, nasema haya ili kuiomba Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi itatue tatizo la eneo la Nyashana Jiji la Mwanza kati ya raia na Jeshi. Wananchi wananyanyaswa sana na wanajeshi na watu wa Ardhi kwa kutofikiria kwamba kuna haja kubwa ya kuweka maelewano kati ya makundi haya mawili. Wizara ichukue jukumu la kuwasimamia Taasisi na Asasi mbalimbali kuhakikisha kwamba, kama kuna maeneo yao ambayo wamegawiana wayatumie na kuyalinda ili wananchi wasiyavamie. Kuna eneo la Kiyoto Jijini Mwanza, ambalo liligawiwa kwa Jeshi la Polisi, ambao bado hawajalitumia kikamilifu. Kutokana na muda kuwa mrefu, wananchi wameanza kulivamia. Sasa kuna ugomvi ambao umeanza kujitokeza. Kwenye hali kama hizi, Wizara itasaidianaje na vyombo hivi kuvuia matatizo ya aina hii kutokea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, anipe maelezo ambayo yanaweza kuisaidia jamii ili kuepuka matatizo ya aina hii ambayo yanajirudia rudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri hususan katika kazi kubwa na ngumu inayoendelea ya kupima na kugawa viwanja 20,000 katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri hiyo bado nia nzuri ya wananchi wengi kupata makazi mazuri na salama haitafanikiwa kikamilifu kama bei ya viwanja hivyo haitapunguzwa. Wananchi wengi wanashindwa kulipia viwanja hivyo kutokana na ukweli kuwa ni ghali mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitashukuru kama Waziri atatueleza atachukua hatua gani kwa wale wananchi ambao walikuwa na maeneo hayo wakiwa na mazao yao, lakini baada ya kuthaminiwa na kulipwa, bado wameshindwa kulipia viwanja hivyo. Ili kuondoa fikira ya kujiona wamenyang'anywa kinyemela ni kheri kila mwenye eneo lake apewe japo kiwanja kimoja, ili asijione amefukuzwa kwa kutumia mkono wa Sheria.

Ipo haja kubwa kuliangalia suala hili kwa makini zaidi, hasa ukizingatia maendeleo yaliyofanywa katika maeneo hayo kama vile kuwepo na mazao ya kudumu kama miembe, minazi, mikorosho, michungwa na kadhalika. Ahsante.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli tunaiona kazi nzuri inayofanywa na Wizara katika kuendesha Wizara hii, ila naomba tu yafuatayo yaangaliwe haraka:-

Mosi, tatizo la mpaka kati ya Iramba Mashariki, Karatu, Mbulu na Hanang bado lipo hasa wakati huu ambapo wenzetu wa Mbulu wameanza kuingilia mpaka unaotenganisha Mikoa ya Singida na Arusha pia Wilaya za Iramba na Mbulu hivyo kusogeza becons kuingia ndani ya Iramba. Ilikuwa tufanye ziara na Mheshimiwa Ntimizi, Naibu Waziri, kwa kuwashirikisha viongozi wote wa Wilaya husika lakini ilishindikana kwa kuwa uliingiliana na Sherehe za Kitaifa zinazohusu wanawake. Nakuomba Mheshimiwa Waziri, safari hiyo ifanyike mapema iwezekanavyo kurudisha mahusiano mazuri kati ya Wilaya na Wilaya.

Jambo lingine ni viwanja vipya vinavyopimwa Dar es Salaam, tunaomba utaratibu mnaotumia kugawa viwanja hivyo uendelee lakini wale ambao hawana uwezo wapewe muda wa kulipa hata kwa mikupuo mitatu au minne. Kauli ya baadhi ya watendaji wako kusema kama huna fedha za kulipia kwa mkupuo mmoja uwapishe wenye fedha siyo mzuri na itazua matabaka ya makazi. Tunaomba mpango huo usitishwe na waombaji hasa watumishi wa umma, Wabunge, wapewe muda wa kutosha wa kulipia viwanja hivyo. Jambo hili si dogo na si la kulidharau, nakushauri ulizingatie sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii kwa njia ya maandishi, kuwapongeza Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Gideon Cheyo, Naibu Waziri, dada yangu Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Katibu Mkuu na Watendaji wote walioshiriki katika kuandaa Bajeti hii, yenye kuainisha utekelezaji wa sekta zote ndani ya Wizara. Kweli Bajeti ina mwelekeo wa kuboresha utendaji na kutoa huduma bora kwa wananchi.

Naipongeza Serikali kupitia Bajeti hii kwani imetambua kuwa kulikuwa na tatizo kubwa la vifaa katika zoezi la upimaji wa viwanja. Kukosekana kwa vifaa huwafanya wateja waliokuwa wanapimiwa viwanja kubeba mzigo mkubwa wa gharama ikiwa ni pamoja na gharama ya vifaa vitakavyotumika.

Kwa kuwa tatizo hili Serikali imetenga fungu, basi mgao uende sambamba na mahitaji kwa kila eneo husika yaani Kijiji, Mji Mdogo, Mji, Manispaa na Jiji, ili kufanya zoezi la upimaji liwe jepesi na kutokuwaongezea gharama wananchi (wateja).

Vile vile niungane na maoni ya Kamati ya Bunge iliyojadili Bajeti hii kuwa suala la rushwa lipo, hasa wananchi wanapohitaji kupata kiwanja hasa kwenye maeneo yanayogombewa. Maafisa Ardhi huomba rushwa na anayetoa ndiye anayepewa kipaumbele, tabia inayowafanya wananchi wa kawaida kutotendewa haki. Naiomba Serikali ikemee na kuwachukulia hatua Maafisa wanaobainika na tabia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie haki ya kumiliki ardhi, kwa kuwa kuna wananchi au Watanzania wajanja au waliowahi kupata Hatimiliki ya ardhi kwa maeneo makubwa na kutoyatumia vilivyo. Basi Serikali iwapunguzie na kugawa kwa wengine kwani wapo wananchi wanaohitaji kuliko wananchi wachache kumiliki maeneo makubwa bila hata kuyazalishia kwa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna nchi nyingi ambazo hujenga nyumba nyingi na kupangisha raia wake na kisha kuwauzia. Kwa kuwa utaratibu huo ni mzuri sana na hata Serikali yetu imebaini utaratibu huo mzuri. Niombe Serikali ijitahidi kupata maeneo makubwa ya kujenga nyumba kwa kila Miji, Manispaa na Jiji ili Miji yetu kuwa na nyumba zenye ramani za kufanana.

Ni imani yangu kuwa miji yetu itapendeza na kufanya utoaji wa huduma zingine kama maji, simu na umeme kuwa rahisi. Naipongeza Serikali kwa kuwauzia wananchi nyumba ambazo walikuwa wanapanga. Kwa kuwa wapo raia ambao wameshindwa kununua basi, nyumba hizo zitakapoanza kuuzwa zitangazwe ili waweze kupata wananchi wengi kuliko wachache kujinufaisha.

Sasa nizungumzie nyumba zinazojengwa karibu na barabara. Naiomba Serikali ikemee suala la wananchi kupimiwa karibu na barabara wakati maafisa wa Ardhi wanafahamu upana wa barabara za Kitaifa za Kimkoa, Kiwilaya na kadhalika. Kwani Serikali hupata gharama ya kulipa fidia inapoamuliwa baadhi ya nyumba kubomolewa. Vile vile wananchi hupata hasa ya kuhamahama na kujenga nyumba upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya miji mingi katika nchi yetu, zipo nyumba katikati ya miji ambazo zimechakaa sana na kuharibu shoo za miji. Naiomba Serikali iwashauri wananchi hao kuuza nyumba hizo kwa wananchi wenye uwezo na wao kupewa fedha za kujenga nyumba zingine nje ya miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu wakazi hao wakielimishwa vizuri wataondoka na kuwapa wenye uwezo wajenge ili miji yetu ipendeze. Baada ya mchango huu, sasa niungane na wenzangu kuunga mkono Beti hii kwa asilimia mia. Nawatakia utekelezaji wenye maslahi kwa wananchi na Taifa kwa ujumla.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuunga mkono hoja. Nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Naibu wake pamoja na wataalam wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa kwanza ni kuhusu nyumba za *National Housing*. Wapo wapangaji wa miaka mingi katika nyumba hii. Pamoja na kuwepo mpango wa kuziua nyumba hizo kwa kuuziwa wao, lakini kutokana na unyonge wa kutomudu kuzinunua, nashauri Wizara iwasiliane na mwajiri wa mpangaji kwa walio watumishi kuona vipi anaweza kumsaidia mtumishi wake badala ya kumtimua na kupoteza sifa ya kutoimiliki nyumba ambayo amekuwa akipanga kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili ni kuhusu viwanja vipya 20,000 ambavyo vimepimwa kwa ajili ya makazi mapya. Viwanja ni vidogo kutokana na mazingira yalivyo hasa vile vya kiwango cha kati, kwani ingepaswa viwanja viwe vikubwa kiasi ambacho unaweza kufanya mambo mengine ya kujitegemea kiuchumi huku unaishi. Mpango huu katika maandalizi mengine upanuzi wa viwanja uwe mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine ni kuhusu viwanja vilivyowazi na vinavyotumiwa na vijana kwa ajili ya michezo. Upo mtindo wa matajiri wenye uwezo kifedha kuvinunua viwanja hivyo kinyemela kwa maslahi yao. Ili kulizuia hilo bora Serikali ingetoa tamko rasmi la kinga kwa maslahi ya vijana wetu kwa ajili ya burudani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine ni kuhusu maeneo ya kuzikia yaani maeneo maalum ya kuzikiana kwani pamoja na mjini Dar es Salaam kujaa bado binafsi nina wasiwasi wa kutengwa kwa maeneo mengine maalum kwa ajili hiyo ambayo ni muhimu kwetu sisi binadamu katika hatua ya mwisho ya mapumziko ya milele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Wizara hii inapaswa kuongeza nafasi kwa ajili ya huduma za vyoo katika sehemu tofauti za miji yetu kwani hivi sasa imekuwa shida sana kupata huduma hii muhimu, lakini ipo mbali na mawazo yetu kwani linaonekana ni dogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo yoyote katika nchi yanaendana na mipango mizuri ya ujenzi, mimi napendekeza pia yatengwe maeneo maalum ya ujenzi wa nyumba za ghorofa ikiwa katika mpango maalum wa ghorofa mbili mbili au tatu kwa wenye uwezo hii itasaidia sana kuboresha uzuri wa miji yetu, lakini pia kutoa nafasi maalum kwa wenye uwezo kuboresha miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja kwa kuwatakia ufanisi mzuri wafanyakazi wote kwa Wizara hii katika kutuboreshea mazingira tofauti na majukumu yanayowakabili. Ahsante.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na wataalam wote wa Wizara kwa hotuba nzuri iliyojaa mipango ya kutatua matatizo ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hatua aliyochukua juu ya kuimarisha mipaka ya Kimataifa kati ya nchi yetu na nchi jirani Kenya, Uganda na Malawi. Lakini ingefaa kuimarisha alama za mipaka yetu yote ya Kimataifa na nchi tunazopakana nazo kama Rwanda, Burundi, Zambia na Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naomba sana kufahamu kama Serikali imeanza mazungumzo na Serikali ya Malawi juu ya utata wa mpaka wa Ziwa Nyasa. Ni kweli Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, alitushauri kuwa suala hili tusilipigie kelele sana kwa kuwa ni suala nyeti hivyo liendeshwe kwa makini na uangalifu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si kama sithamini ushauri wa Mheshimiwa Waziri, hapana, lakini kwa sababu kubwa suala hili linawagusa sana wananchi wangu wa Jimbo la Mbinga Magharibi hivyo inanilazimu kufuatilia chini chini ili jambo hili lipate ufumbuzi mapema kwa manufaa ya Taifa letu nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hotuba ina mipango mizuri itakayoleta faida kwa wananchi kwa jumla, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii ili nichangie hoja ya Waziri wa Ardhi na maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Gideon Cheyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza natumia nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara na wafanyakazi wote wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa Bajeti nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nauelekeza kwenye Jimbo langu la Nanyumbu ambako kuna maeneo kadhaa ambayo yanakaliwa na wananchi wengi sana lakini hadi sasa hakuna mipango ya maeneo hayo kupimwa hivyo kuruhusu ujenzi holela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mangaka ni sehemu ya kwanza ambayo ina wakazi wengi na kwa hivi sasa inakadiriwa kuwa na wakazi 15,000 lakini hakuna mpango wowote wa upimaji mji. Mji huu mdogo ambao ni Makao Makuu ya Jimbo la Nanyumbu na kuwa na taasisi mbalimbali ndani yake bado hulina mpangilio mzuri wa ujenzi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mji wa Mangaka una taasisi za shule ya sekondari, kituo cha Polisi, Mahakama ya Mwanzo, Kituo cha Kuendeleza Zao la Korosho, *Parish*, Kituo cha Afya, Makanisa, Misikiti, Kituo cha Mafuta, maduka, shule za msingi, mashine za kusaga nafaka, Ofisi ya Mbunge, Ofisi za Kata, Jimbo, Vijiji, soko, mahoteli, vilabu, viwanja vya mchezo, Zahanati na *garage*. Kutokana na shughuli hizo zote ni wazi kuwa Mangaka inahitaji kupimwa kimji. Naomba Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kusaidia katika kufanikisha lengo hilo ili kupunguza migogoro inayoweza kutokea hapo baadaye. Mji wa Mangaka kwa kuwa ni katikati ya Jimbo la Nanyumbu una nafasi nzuri ya kukua kwa haraka sana hivyo inawezekana idadi ya wakazi wake ikaongezeka kwa kipindi kifupi kijacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mji mwingine ambao unakua haraka sana ni Michiga ndani ya Jimbo la Nanyumbu ambapo sasa mji huo unakadiriwa kuwa na wakazi zaidi ya 10,000. Ujenzi katika mji huo bado ni holela hivyo kuhitajika msaada wa upimaji kutoka Serikalini. Michiga nayo ina taasisi nyingi kama Mahakama ya Mwanzo, Kituo cha Afya, Shule ya Sekondari, Shule ya Msingi, Misikiti, Makanisa, maduka, mahoteli, nyumba za wageni, ofisi za kijiji na makazi ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kuwa Michaga inastahili kuwa na mipango miji yake. Hivyo naomba Serikali isaidie ili tuwe na miji mizuri inabidi kuanza mapema kuweka miji yetu iwe mizuri na iendelee kukua ikiwa bado ni miji mizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makao Makuu ya Kata zote nayo yanahitaji kupimwa kwa bahati nzuri vijiji vingi vilianzishwa wakati wa Sera ya Vijiji vya Ujamaa ambapo sasa watu wanaishi kimji kuanzia ujenzi na shughuli nyingine. Hivyo ni vizuri vijiji hivyo navyo vikapatiwa mipango miji ili wananchi ambao sasa wameitikia wito wa kujijengea nyumba bora wafanye hivyo wakijua kuwa maeneo hayo yatakuwa ya kudumu. Naomba Serikali kusaidia upangaji wa maeneo yote ambayo hivi sasa yanaonekana kuwa ni kivutio kwa wananchi wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na kushukuru tena kwa kupata nafasi hii, ahsante sana.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niwapongeze Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wakuu wa Wizara kwa hotuba na mipango mizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nipongeze Wizara kwa umakini mkubwa wa utekelezaji wa mpango wake wa mwaka wa fedha wa 2002/2003 hususani upimaji wa viwanja 20,000 Jijini Dar es Salaam. Hongera sana Mheshimiwa Waziri na hongereni sana viongozi wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tulipopitisha mpango wa upimaji viwanja 20,000 Dar es Salaam tuliona huu ni mwanzo mzuri. Kila mwaka tuendelee na kasi hii ya kupima viwanja na mwaka huu ingepima viwanja vingine 20,000 mpaka 30,000. Tulitegemea, mwaka huu mpango ungekwenda Morogoro, Arusha, Mwanza, Moshi, Dodoma, Singida, Tabora, Kigoma, Mbeya, Mtwara, Lindi, Songea, Iringa, Tanga, Babati, Shinyanga, Bukoba, Musoma na kadhalika.

Halafu mwaka ujao upimaji uende Mwanga, Gairo, Matombo, Mto wa Mbu na kadhalika. Wizara inasema nini juu ya hili? Kuna njaa sana ya viwanja nchini. Hili kama nilivyosema huko nyuma, lina uwezo wa kuondoa wananchi kwenye umaskini kufumba na kufumbua kwa kuwa mwananchi anayemiliki ardhi anaweza kukopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jedwali la hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Jedwali Na. 5 ukurasa wa 51 imeorodheshwa vijiji vyote vilivyopimwa au vyenye *plan*. Katika jedwali hili, Wilaya ya Mwanga haipo kabisa kama vile hakuna hata eneo moja lililopimwa. Lakini ni kweli kuwa zaidi ya 90% ya vijiji havina *plan*? Naomba mwaka huu Wizara itupimie hata vijiji 30 tu. Katika ombi hili Wizara pia iwasaidie wananchi wa kijiji cha Mgagao ambacho kina barua ya *offer*, basi kipate Hati Miliki.

Mwaka jana Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi aliniahidi kuwa angetuma wataalam kuwapa utaalum wa kutengeneza matofali ya urahisi na kisasa

wananchi wa Kisijicha Mamba, wanaojenga Zahanati ya Kikweni Kata ya Msangeni, Tarafa ya Ugweno, kijiji cha Mkuu, wanaojenga Zahanati ya Mkuu, Kata ya Shighatini, kijiji cha Njia Panda, wanaojenga Zahanati ya Njia Panda eneo la Nyumba ya Mungu, Kata ya Kirya na kijiji cha Vuchama-Ndambwe, wanaojenga shule ya sekondari ya Kamwala, Kata ya Shighatini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri anipe matumaini ya haya kutendwa. Mimi naunga mkono hoja hii bila wasiwasi, ahsante sana.

**MHE. ABU T. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili vijiji vifaidike na gawio la faida ya uwindaji pale *Professional Hunters* kutoka nje wanapokuja kuwinda kwenye *Designated Hunting Blocks* Wilaya husika hupewa 25% na hatimaye vijiji au kijiji ambacho kinahodhi *Hunting Block* hiyo hupata pia gawio la asilimia saba na nusu lakini baada ya kijiji hicho kuwa kimeandikishwa kwa mujibu wa *Wildlife Management Area Act*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano wakati mnyama husika aliyewindwa ni nyati Pato kwa Taifa ni shilingi 600,000/= . Kwa sababu hii kijiji huwa na haki ya kupewa shilingi 45,000/= lakini inabidi kijiji hicho kiwe kimeandikishwa kwa mujibu wa *WMAA*. Je, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii, zina mikakati gani ya kutekeleza azma hii ya uandikishaji wa vijiji ili kuviwezesha vijiji kupata kipato na kupunguza kero za jamii kama vile ujenzi wa shule, Zahanati, visima vya Maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna mipango je, Jimbo la Kilombero, vijiji vya Utengule, Mofu, Mugetu (Mchoube), Tanganyika Masagati, Ngalimila, *Msolwa Station* Kidatu na vinginevyo vimepangiwa mpango gani wa upimaji kwa kazi yao muhimu ya kuhifadhi na kulinda raslimali hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na kumpongeza kwa dhati na kazi nzuri ya Mheshimiwa Waziri na safu yake yote ya uongozi.

**MHE. MWADINI ABASS JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kushukuru kupata fursa ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Aidha, nimpungeze Mheshimiwa Gideon Cheyo pamoja na Naibu Waziri wake na watendaji wao wote kwa ujumla kwa maandalizi mazuri ya hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nitoe mchango wangu na zaidi nitazungumzia upimaji na ugawaji wa viwanja kwa ajili ya makazi ya wananchi. Zoezi la upimaji wa viwanja kwa ajili ya makazi ni jambo la msingi na la muhimu sana kwani linapunguza matatizo ya ujenzi holela hasa katika miji mikubwa na hali kadhalika linaepusha wananchi kujenga katika sehemu za mabonde. Lakini ili matatizo hayo yaweze kuepukika kikamilifu hapana budi upimaji wa viwanja ni lazima uendane na kasi ya mahitaji ya viwanja hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo lingine ambalo kama halikuangaliwa vizuri ile azma ya kuwapatia wananchi wanyonge viwanja huenda likaingia dosari. Bei ambazo zinatozwa na Serikali ili kummilikisha mwananchi kiwanja imekuwa kubwa kwa mwananchi wa kawaida kuimudu. Hali hii inaweza kusababisha wananchi kushindwa kuvilipia viwanja hivyo na hatimaye kunyang'anywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshauri Mheshimiwa Waziri ajaribu kutafuta utaratibu ambao utawawezesha wananchi wa kawaida kumudu kulipia viwanja ili nao waweze kujijengea nyumba za kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine lililojitokeza ni kuongezeka kwa gharama za kulipia vibali vya kujengea na ada kubwa za uchoraji ramani za nyumba. Gharama hizi pia zinakuwa ni kikwazo kwa wananchi wa kawaida ambacho hupelekea wenye viwanja kushindwa au kuchelewa kuviendelea viwanja ambavyo wanavimiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshauri Mheshimiwa Waziri kuandaa utaratibu utakaoweza Wizara yake kutoa huduma za uchoraji wa ramani za nyumba kwa bei nafuu atakayoweza kuimudu mwananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuchangia katika Wizara hii ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi na naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa kumi na tatu katika hotuba ya Waziri, imeeleza juu ya kuendelea na programu yake ya kutoa elimu kwa umma juu ya Sheria za Ardhi ya mwaka 1999 na kanuni zake kwa njia ya redio, *television* na makala katika magazeti mbalimbali pamoja na semina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli suala la ardhi ni suala nyeti na muhimu kwa umma wote wa Watanzania. Kwa hiyo, mbali ya kuwa Wizara hii hutoa elimu hiyo kwa umma vile vile ni lazima Wizara ihakikishe kuwa elimu hii inafika vizuri sana kwa umma wote wa Tanzania. Pia katika elimu hii ni lazima itoe ufafanuzi mzuri ili kuzijua pia haki zao za ardhi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa kumi na sita, Wizara ilieleza juu ya suala la upimaji wa viwanja 20,000 katika Jiji la Dar es Salaam. Ninapongeza sana hatua hii ya Wizara. Lakini pia ninaishauri kuwa wawe waangalifu sana viwanja hivi visije vikaangukia kwa matajiri tu na kuwaacha wanyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa kumi na nane, unaeleza juu ya Mipaka ya Kimataifa. Kwanza nachukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Malawi kumteua mtaalam mwelekezi (*Consultant*) wa kufanya upembuzi yakinifu juu ya kudhibiti Mto Songwe. Naomba Serikali kulikamilisha haraka sana ndani ya muda huu wa uongozi wa Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiu ya viongozi mbalimbali nchini pamoja na wananchi wote wa Tanzania wanayo hamu ya kutaka kuona suala hili linamalizika vizuri na kwa haraka iwezekanavyo ili kuepusha migogoro ambayo inaweza ikatokea huko mbele ya safari kati ya nchi zetu hizi mbili yaani Tanzania na Malawi. Ni matumaini yangu kuwa Serikali itatoa taarifa kwa umma mara tu hatua hizi zitakapokamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 25, unaeleza mipango ya matumizi bora ya ardhi. Tunaipongeza na pia kuitaka Wizara hii pamoja na mipango hii mizuri sana lakini ninashauri kuwa kati ya mipango hiyo lakini suala zima ni kwa Wizara, Halmashauri kuepusha migogoro ndani ya umma ikiwa ni pamoja na mipango ya utoaji wa maeneo mbalimbali yawe sahihi. Jaribio ambalo linaweza kuepusha mivutano kati ya Serikali, taasisi za umma, makampuni na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu kupewa eneo la kujenga nyumba yake au jengo lake lolote lile na baadaye pakatokea amri ya kuvunja au kuhamisha nyumba yake au jengo lake hilo kwa visingizo kama ujenzi wa barabara na kadhalika ni usumbufu mkubwa kwa wananchi jambo ambalo linaweza kupoteza imani ya wananchi mbalimbali kwa Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la rushwa, naiomba Serikali kuwa makini sana kupambana nalo ili wananchi wasipoteze mali zao kwa kitu ambacho ni haki yake kukipata kuhusiana na suala la upatikanaji wa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Ukimwi, Wizara iendeele kuwaelimisha wafanyakazi wake kujinusu na ugonjwa huu hatari wa Ukimwi ili Wizara iwe na wafanyakazi walio bora na safi kiutendaji na kiafya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante.



**MHE. HAMISI J. NGULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kuunga mkono hoja hii kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja hii katika *point* chache ili kuboresha utekelezaji wa kazi ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kuwa Wizara imejishughulisha na upimaji wa vijiji. Tatizo langu hapa ni jinsi mipaka inavyofahamika na wanavijiji wote isivyofuatwa punde upande moja wa kijiji usiposhirikishwa. Sasa hivi ardhi imeanza kuwa mali kwa wananchi wote, hivyo migogoro ya mipaka imezuka karibu katika sehemu nyingi kijijini katika vijiji vya Singida vijijini na Singida mjini kila moja akitaka kujiongeza ardhi.

Ushauri wangu ni kuwa mahali penye migogoro Serikali, itafute ufumbuzi haraka kwani inawezekana kusababisha uvunjaji wa amani. Pia wakati wa upimaji uongozi wa vijiji vyote ushirikishwe ili pasiwepo na malalamiko baadaye. Mara nyingi mipaka hii inafahamika tangu siku nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado upimaji wa viwanja unakwenda pole pole ukilinganisha na wananchi wanavyojenga. Matokeo yake ni miji kujengwa ovyo kiasi cha kuathiri taratibu za kuweka miundombinu kama vile umeme, barabara, maji na mifereji ya maji ya mvua visingizio hapa ni wataalam wachache na upungufu wa fedha. Je, kwa visingizio hivyo miji yetu iendelee kuwa ovyo?

Singida Mjini ni Mji mmojawapo ambao una tatizo hilo kiasi kwamba wananchi wanachangishwa fedha ili wapimiwe viwanja lakini hata hivyo mpaka leo hawajapimiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri anieleze kama ni halali kuichangia Wizara kwa ajili ya upimaji na ni lini basi waliochanga watapimiwa viwanja vyao. Wananchi hawa wanangojea majibu na walishalalamika kwangu na imeshakuwa tatizo la muda mrefu tangu mwaka 1998.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, nitashukuru kama nitapata maelekezo ya hayo na narudia kuunga mkono hoja hii.

**MHE. SALIM OMAR ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila ya jazba ya kisiasa natamka kuwa fedha uliyoiomba itapitishwa na sisi Wabunge wenzako, ila fedha hii unayoiomba ni ndogo ukilinganisha na ukubwa wa Wizara yenyewe na mahitaji muhimu ya Wizara pamoja na mipango ambayo imeshajipangia kuitekeleza katika mwaka huu 2003/2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rushwa katika Wizara ipo na inaathiri mno Wizara na ni kero kwa wananchi kwa ujumla. Ushauri wangu kwa hili, napendekeza pawe na mfanyakazi maalum ili afuatilie mwenendo wa wafanyakazi wenzake ambao wanapokea rushwa ili awataje na mfanyakazi huyo atoe mwenendo mzima anaouona bila ya woga wowote.

Upimaji wa ardhi vijijini/mashamba, inaonekana utaratibu wake si mzuri. Inatakiwa utaratibu uimarishwe ili ipunguze adha iliyopo sasa hivi ili kila mwananchi apate ardhi ya kujenga nyumba ya kuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uuzaji wa viwanja, viwanja ni muhimu na ni sehemu ya maisha ya binadamu na mifugo yao. Kwa ukweli huo basi Wizara izingatie bei ya viwanja kwa sababu inaonekana viwanja vimegawanywa kulingana na nani aishi wapi kwa maana mtu wa kipato cha chini hana haki ya kuishi mjini kutokana na bei kubwa ya viwanja hivyo hapo mjini. Pia naomba unifahamishe ni kwa nini fedha za maendeleo kwa mwaka 2003/2004 zimepungua ukilinganisha na mwaka 2002/2003 ni kwa sababu gani na ukubwa wa eneo ni lile lile?

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kwa kusema naunga mkono hotuba hii, nawatakieni kila la kheri. *Amin.*

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Waziri na kumpongeza Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara kwa jitihada wanazozifanya kuwatumikia wananchi. Pamoja na kero zinazojitokeza kwa upande wa watumishi kuishi kwa kulaghai wateja na kuendelea kuweka rushwa kama msingi wa kazi zao, vita hivi lazima viendeleo kwa nguvu zote. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kukubali kuongeza muda wa kulipia nyumba kwa wapangaji. Naelewa kuwa wapangaji wengi walikuwa wanahaha kuhusu hatima hiyo ya mwisho wa mwezi wa Juni (*June 30<sup>th</sup>*).

Pamoja na hilo, nashauri sasa baada ya maamuzi hayo, ingefaa mikataba iandaliwe ya kisheria ili atakayeshindwa kutekeleza hayo basi iwe rahisi kuwachukulia hatua. Maelekezo ya Waziri ni budi yaambatane na mikataba ya kisheria ili wapangaji wasije wakapata kisingizio kingine. Naomba kumshauri Waziri katika kuwavutia wawekezaji wakubwa kwenye mashamba ya mazao ya biashara wapewe kodi nafuu kama wanavyopewa wengine *Tax Holiday* kwa kipindi cha miaka mitano. Ni vizuri pia maeneo yanayofaa yatengwe nje na mbali kidogo ya makazi ya vijiji, ili kuondokana na matatizo ya migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wanaongezeka kwa kasi kubwa. Lakini pia miji fulani kama Sumbawanga unapanuka kwa kasi kubwa sana sawa na Dar es Salaam. Ningemwomba Mheshimiwa Waziri asaidie kutupatia wapimaji ili mji wetu usiwe na *squatters*. Huu ni mji ambao umejengwa vizuri na mfano mzuri wa kuigwa. Ni vizuri tukasaidiwa. Pia mji huu upatiwe msaada wa ujenzi wa nyumba (*model*) za bei nafuu kwa kuwa wakazi wengi wa mji wa Sumbawanga wanajenga majengo makubwa kutokana na urahisi wa kupata tofali za kujenga, lakini vifaa vya uezekaji huwa ni tatizo kubwa sana. Hapa tunahitaji michoro inayoweza kuwa ya bei nafuu kwa watu wetu.

*Master Plan* zetu za miji mingi ni budi ziangaliwe upya. Sehemu zinazovamiwa, huwa ni tatizo kubwa na michoro kugushiwa kila mara na baadhi ya watumishi wabovu. Ni vizuri mapendekezo ya Mipango Miji yetu (*Master Plan*) zinazotoletwa Wizarani zisikubaliwe mpaka Maafisa husika watakapokwenda kutembelea maeneo yanayopendekezwa, wajionee wenyewe badala ya sasa kutoa vibali bila wataalamu kuona maeneo yenyewe. Mpango wa kugawa ardhi kwa wananchi katika vijiji ufanywe kwa uangalifu zaidi hasa kwa kuangalia hali ya ongezeko la watu na mahitaji ya ardhi kwa ajili ya kilimo, mifugo, viwanda, shule, zahanati, michezo na kadhalika. Hivyo ni vizuri Maafisa wa Ardhi wasaidie *Master Plans* za vijiji vyetu. Nyumba nyingi za Upanga za *NHC* zinaonekana kukaa bila wapangaji kwa muda mrefu. Nashauri uchunguzi ufanyike ili tuone ukweli na uhalali wa nyumba hizo kubaki wazi. Maana mimi mwenyewe ningependa kupata nyumba ya kupanga hapo Upanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana watumishi wote wa *NHC Upanga Branch* kwa jinsi wanavyosimamia nyumba zote za *NHC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii asilimia 100.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ili niweze kuchangia katika hoja ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

Vile vile Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusaidia kujibu hoja mbalimbali ambazo zimezungumzwa leo kwa maandishi na zile ambazo zilizungumzwa wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anatoa Bajeti yake. Pia, Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na hata wakati wa bajeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haitakuwa rahisi kujibu hoja zote, lakini ambaye hatutamjibu hapa leo atuvumilie, hata yule tutakayemjibu tutahakikisha kwamba tumeweka kwa maandishi ili muwe na kumbukumbu za kutosha katika masuala ambayo mmeyaongelea kuhusu Wizara yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza na hili suala la ndugu yangu Mheshimiwa Omar Kwaangw', ambaye amenitaja kwamba nilifika kule kwake. Ni kweli, lakini wakati ule nilifika kukemea mambo ya ukeketaji nikiwa Naibu Waziri wa Afya, kwa sababu kule hiyo ndiyo kazi. Lakini wakati huo huo, niliona matatizo ya jinsi wawekezaji na Wananchi wanavyogombana kwa ajili ya mashamba ambayo yamemilikishwa na mengine yametelekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoweza kumwambia ndugu yangu huyo ni kwamba, asiwe na wasiwasi katika Jimbo lake la uchaguzi, matatizo haya bahati nzuri yanafahamika katika Halmashauri, Wizara pamoja na yeye mwenyewe. Kulikuwa na utata wa jinsi ya kuthamini, kwa sababu tusingeweza kugawa mashamba hayo baada ya kutelekezwa na Serikali kuyachukua bila kuyathamini tena halafu tuone tunaendaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uthamini wa binafsi wengine wanafika mpaka Sh.15,000,000/=, uthamini wa Serikali ulifika gharama karibu za Sh.6,000,000/=. Utata huo ulijitokeza, lakini upo katika Ofisi ya Kamishna wetu wa Ardhi, nina hakika utatatuliwa hivi karibuni. Lakini kwa kuwa Wakurugenzi na Watendaji wetu bado wako hapa kwa siku mbili/tatu, kama Mheshimiwa Kwaangw' hataona vibaya tukutane ili tumpe maelezo ya kina na wakati gani muafaka hawa watu watarudi tena kufanya kazi ambayo ametulilia hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, napenda kumjibu ndugu yangu Mheshimiwa Prof. Sheikh Mikidadi, Mufti, alipouliza: "Kwa nini *National Housing* haifanyi mpango wa kwenda kwenye Shirika la *Shelter Afrique* kukopa?"

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mikidadi mara nyingi anakuja sana katika ofisi yangu, masuala haya ningemjibu kule kule ofisini. Mradi wa Boko usingeweza kukamilika au kufikia hali iliyopo bila ya mkopo ule. Kwa hiyo, sisi pia ni Wanachama, tumekopa katika Shirika hilo. Asiwe na hofu, tuna hakika Shirika hili tunalitumia kwa ukamilifu na michango tunatoa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru ndugu yangu mwingine, Mheshimiwa Major Jesse Makundi; yeye kaandika, lakini tulishindwa kupeleka kwa wataalam. Amesema kwamba, anamuomba Waziri atembe katika mipaka na Wakuu wa Mikoa na Wilaya kwanza kudumisha ujirani mwema na pili, waweke azma ya kufyeka mipaka yao mithili ya gridi ya Taifa ya umeme ili Wananchi wajue hapa ndiyo mwisho wa Tanzania, Uganda, Kenya, Rwanda na kadhalika na anaomba ifikapo tarehe 1 Agosti, 2003 tuwe tumekwishampa jibu kwamba Waziri na wataalam wetu wamefanya kazi hii. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Inshallah* tuombeane salama, kazi itafanyika kwa sababu ni kwa manufaa yetu ili kutambua Wananchi wetu wanaishia mpaka wapi. Tutafanya hayo na tutamarifu Mheshimiwa Mbunge, hata kama siyo tarerhi 1 Agosti, 2003, lakini tutajitahidi kwa sababu kawaida yetu ni kujibu Wananchi mahitaji yao yote wanayozungumzia katika mikutano hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mipaka ya nchi kwa nchi, limezungumzwa na Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mbunge wa Vitongoji, kuhusu *Pemba channel*. Bahati mbaya labda hakuweza kufanya mawasiliano katika Wizara husika kule Zanzibar.

Mwaka 2001 nikiwa na Mkurugenzi mmoja, kwa bahati nzuri tulihudhuria kikao cha *East Africa Community* pamoja na Katibu Mkuu wetu. Suala hili lilizungumzwa kwa kirefu jinsi gani mpaka ndani ya maji unakuwa na tukawasilisha karatasi zetu tukampa Waziri aliyehusika na shughuli hiyo.

Bado Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar walileta tena hoja hii wakasema kwamba, wanahitaji kufahamu kuhusu mpaka huu wa Pemba. Ikawa bahati mbaya nafikiri zile document walizokuwa wamepata mwaka 2001 wamezi-misplace au pengine kwa ajili ya kazi nyingi hawakujua ziko wapi na bado mwaka huu tumepeleka tena kueleza kwa kinagaubaga kabisa kwamba mpaka wetu uko hali hii.

Pia, mkataba ambao ulitayarishwa mwaka 1975 ulipelekwa moja kwa moja Umoja wa Mataifa mwaka 1996. Kwa hiyo, mpaka wa Tanzania na Kenya kupitia Pemba channel unafahamika kisheria.

Mpaka wa Malawi umeongelewa tena na hasa msisitizo ameutoa Ndugu yangu Mheshimiwa Kolimba; Mbunge wa Ludewa kwamba, mpaka wetu katika *Lake Nyasa*, uko wapi?

Kwa taarifa ni kwamba, *Joint Commission of Cooperation* imekaa Dar es Salaam na kwamba tatizo la Ziwa Nyasa siyo tatizo la Tanzania na Malawi peke yake. Pia, kwa upande mwingine tuna *Joint Commission* ya Msumbiji na Tanzania, katika upelelezi ule wa jinsi gani nchi hizi tatu zitafaidika na maeneo ya ziwa hili.

Wizara yetu ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Wizara ya Mambo ya Nje ya Malawi na Msumbiji, wao ndiyo Wenyeviti wetu na sisi kama wataalam wao tunashughulikia suala hili na tuna hakika tutapata hakika haraka iwezekanavyo ni jinsi gani kila mmoja afurahie kutumia maji ya Ziwa Nyasa. Kwa hiyo, tufanye subira Inshallah suala hili litakamilika hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Janguo ameeleza upimaji wa Mji wake wa Kisarawe na kwamba nyumba zimebomolewa ili Mji uwekwe sawa. Suala hili tumelipokea na tutawasiliana na Wizara ya Ujenzi tuone ni jinsi gani wale waliobomolewa nyumba watafidiwa na Mji wao upangwe vipi, ingawa haupangiki! Kisarawe kuna milima, watu wenyewe hawaujengi Mji huo vizuri, ingawa wanalima mihogo mingi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji utatengenezwa kwa sababu Serikali imesema tubomoe nyumba, tupange vizuri na nyie tusaidieni. Pale tulipobomoa msijenge tena vile vidungu vidogo vidogo kama watu wa Rufiji, kwa sababu mtazidi kuharibu Mji na ninawatakiwa kila la kheri Mji ule upendeze, mtu akichoka kukaa Dar es Salaam anakwenda Kisarawe kupumzika. Kwa hiyo, Mheshimiwa Janguo usiwe na wasiwasi. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Slaa alizungumzia kuhusu upimaji viwanja na hasa Vijijini kwamba zoezi hilo linakwenda pole pole sana na kuwa umiliki ni muhimu katika kuendeleza ardhi. Suala hilo tunalifahamu, lakini taratibu za kupima viwanja huanzia kwa kuandaa ramani za Mipango Miji. Upimaji wa viwanja Vijijini ikiwa na maana ya maeneo ya makazi Vijijini haufanyiki bali upimaji unaofanyika ni ule wa mipaka ya Vijiji husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la upimaji binafsi, Wataalam hao wanaruhusiwa kufanya upimaji sehemu yoyote nchini kwa kutumia Kampuni inayotambuliwa na iliyosajiliwa na Halmashauri ya Taifa ya Wapima Ardhi.

Aidha, Mpima Ardhi huyo naye awe amesajiliwa na Halmashauri hiyo. Wapima Ardhi hao wameshiriki katika upimaji wa viwanja 20,000 Dar es Salaam, kwa hiyo, Wananchi wako huru kuwatumia ili mradi tu wana leseni na wanatambulika kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Diana Chilolo amezungumzia tatizo la upungufu wa vifaa vya upimaji katika Wizara yetu. Ninashukuru kwamba anafahamu tatizo hilo.

Pia, alisema kwa kuwa Serikali imetenga fungu, basi mgao huo uende sambamba na mahitaji kwa kila eneo. Ingawa si rahisi, lakini vifaa vya upimaji hununuliwa kwa gharama kubwa sana.

Kwa muda mrefu wakati Halmashauri zetu zinajijengea uwezo wa kununua vifaa hivyo, tutaendelea kutumia vifaa vichache vilivyopo kwa utaratibu wa kushirikiana Serikali Kuu na Halmashauri hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za upimaji zinaweza kupungua kama Wananchi wengi watahamasishwa kugharamia upimaji kwa wakati mmoja katika eneo moja. Ingawa kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja amesema kwamba, wanachanga pesa za kupima Vijiji, lakini hawapimiwi! Nafikiri tu

muda muafaka bado au pengine pesa hazijatimia kuweza kugharamia upimaji wa Vijiji hivyo, lakini tumo katika harakati hizo za kupima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mbunge wa Shinyanga na kaka yangu, ametoa ushauri kwamba fedha za upimaji maeneo ya Miji inatakiwa zitolewe mapema ili kupunguza au kupambana na ongezeko la makazi holela (*squatters*). Tunashukuru kwa ushauri huu, lakini Wizara yangu itaendelea kushirikiana na vyombo vyote vinavyohusika kuhakikisha kwamba huduma zinaendelea kutolewa kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu mmoja amechangia kwa maandishi, Mheshimiwa John Magufuli, Mbunge wa Biharamulo, anatupongeza kuhusu upimaji wa viwanja Mbweni na yeye kaomba, lakini bado hajalipia. Anaomba isiwepo vurugu, lakini tuendee kufanya kazi kwa haki. Jambo hilo nalifahamu kwamba tunafanya kazi kwa haki. Kwa hiyo, tunashukuru kwa ushauri wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migogoro ya mipaka ya ndani kati ya Mkoa na Mkoa, Wilaya na Wilaya au Kijiji na Kijiji, katika uchangaji kwenye Hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu na ile ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, wamechangia watu kama watatu hivi ambao ni Mheshimiwa Hamisi Nguli, Mheshimiwa Benedict Losurutia na Mheshimiwa Mgana Msindai. Hawa wameulizia kwamba inakuwaje mpaka hakuna utatuzi katika migogoro ya mipaka ya ndani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipaka ya ndani ya nchi inawekwa na Halmashauri zilizopakana kwa kushirikiana. Wizara yangu haiweki mipaka, kumbukumbu na vipimo vilivyokubaliwa na majirani hao ndizo tulizotumia kuingiza mipaka ya kwenye ramani ya Wizara ya Ardhi. Uwekaji wa alama zote za mipaka hauna budi kufuata maelezo ya *Government Notice* husika.

Kila Mkoa na kila Wilaya kuna watalaam wenye uwezo wa kutafsiri hizo *Government Notice* na kuonyesha alama za mipaka. Kwa mfano uwekeji wa mipaka ya vijiji unahusisha wananchi kupitia Serikali za Vijiji, mabadiliko yoyote ya mipaka hushughulikiwa na Serikali za Mitaa inashirikisha wananchi, mwenye mamlaka ya mwisho kuigawa miji katika sehemu zote kufanikisha utawala bora ni Mheshimiwa Rais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Mheshimiwa Kisyeri Chambiri, ametueleza kwamba machimbo yanaathiri sana makazi ya watu. Wanatolewa katika maeneo yao lakini hawalipwi wala hawapewi viwanja. Ninafikiri kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, yupo hapa nafikiri kalisikia na nilikuwa namwona akiandika kwa haraka haraka alipokuwa anachangia Mheshimiwa Kisyeri Chambiri kwa hiyo, ikifika wakati muafaka ndugu yangu Mheshimiwa Ibrahim Msabaha atalitolea ufafanuzi kwa sababu si Wizara yake nafikiri angesimama kueleza lakini tumpe nafasi muafaka atakapokuwa anaelezea kwenye Wizara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si vema kuondolewa katika maeneo halafu wasipewe fidia. Lakini sidhani kwamba watu kweli hawakupewa fidia pengine mawasiliano hatupati ya Mbunge na Utawala wa Wilaya na Wizara hayakuwa mazuri au hayakuwepo ndiyo maana Mheshimiwa Kisyeri Chambiri, amelileta hapa. Lakini pia nakupongeza kwa kulileta hapa.

Pia Mheshimiwa Charles Kagonji, amesema nyumba za Serikali zinazuzwa zinazozunguka Hospitali ya Lushoto. Mimi nafikiri sidhani kama ni nyumba za *National Housing*. Kwa hiyo, kama ni za Serikali na bahati nzuri Mheshimiwa John Magufuli alikuwa hapa kalisikia. Lakini wamekwishaelezea kwa hiyo, nina hakika muwasiliane na Ofisi ya Ujenzi ili waweze kukupa maelezo yakinifu ili lisije likaulizwa tena katika Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Mheshimiwa Dr. James Msekela amesema mipango isiyokuwa mizuri katika kuendeleza miji yetu. Ni kweli kama alivyoelezea Mheshimiwa Mbunge, kuwa uendelezaji wa miji katika ukuaji na usambazaji bila ukomo na matatizo. Baadhi ya matatizo yakiwa ni pamoja na kuongezeka kwa gharama za ujenzi na utunzaji wa miundo mbinu kama barabara, mifumo ya usambazaji wa maji safi na maji taka, mifumo ya nguzo za waya za umeme, usambazaji umeme. Kwa maana hiyo, ina

maanisha ongezeko la gharama za fedha. Aidha kutotapakaa kwa miji kuna faida zake ambazo ni pamoja na kuwezesha matumizi mazuri, *economical use* ya ardhi, huduma na miundo mbinu zilizopo, lazima kulinda mazingira kuhakikisha muingiliano wa matumizi yanayofaa na kushabikiana. Kuwa na mfumo mzuri wa kimji, *efficient urban system* kwa kuzingatia faida na hasara zinazopatikana katika kuendeleza miji yetu Serikali imechukua hatua zifuatazo:-

- \* Imeandaa Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995.
- \* Imetunga Sheria ya Ardhi namba 4 na namba 5.
- \* Imeandaa Sera ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000. Hivi sasa inahisha Sheria ya Mipango Miji na vijisura namba 378 ya mwaka 1976 ili iendane na hali halisi ya udhibiti wa miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Mheshimiwa Jackson Makwetta alieleza Mji wa Njombe, ujenzi holela unaofanyika katika maeneo ya miji husababishwa na baadhi ya sababu zifuatazo:-

- \* Ongezeko la wakazi mijini lisilo wiana na ongezeko la viwanja vilivyopimwa, ufinyu wa Bajeti ya kulipa fidia na kupima viwanja mijini.
- \* Kuwepo na miliki za kimila za maeneo ya ardhi ya miji na uuzwaji holela wa maeneo hayo na upungufu wa katika fani mbalimbali za sekta.

Ili kuweza kutatua masuala yaliyoelezwa hapo juu, Idara ya Mipango Miji pamoja na sekta nyingine zinazohusiana na ardhi inatakiwa kuimarishwa kiuwezo yaani fedha, kiutam na kuwepo kwa vitendea kazi vilivyo muhimu ambavyo ni vya kisasa. Umarishaji huu utawezesha uandaaji wa mipango ya kusimamia ukuaji na uendelezaji miji kufanyika na hivyo kupunguza ongezeko hilo la ukuaji wa maendeleo holela katika maeneo ya mji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upimaji nimekwishatolea jibu. Mheshimiwa Leonard Derefa alivyoeleza, hata Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe kwamba upimaji zaidi wa viwanja nchini. Mara upimaji huu utakapokamilika na kufanyiwa tathmini, utaratibu wa kupeleka katika mikoa mingine utafanywa. Tunakwenda kwa awamu pia kutokana na ufinyu wa Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Mheshimiwa Lekule Laizer amezungumza kwamba taratibu za kupima vijiji katika Mkoa wa Kilimanjaro na Jimbo la Longido. Taratibu za kupima vijiji katika Mkoa wa Kilimanjaro na Jimbo la Longido limekamili. Kikosi cha upimaji kinajiandaa kwenda kupima vijiji katika maeneo hayo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Lekule Laizer wasubiri wapimaji, nina hakika utaona kazi watakayokuja kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa kuboresha shughuli za utayarishaji ramani kwa kuboresha mazingira na kuongeza elimu kwa watumishi. Suala hili bado linakuwa gumu hasa ukizingatia kwamba Bajeti inakuwa chini. Pamoja na hali hiyo Wizara inaboresha mazingira kwa kufanya ukarabati wa majengo yaliyopo, Wizara pia inahitaji kutoa nafasi kwa watumishi kuhudhuria masomo hapa nchini na nje ya nchi kwa idadi inayolingana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye maendeleo ya makazi. Miji yetu haina master plans, zilizopo zimepitwa na wakati, pia michoro mingi ya miji haijumuishi maeneo ya huduma mbalimbali kama vile maeneo ya michezo, maegesho ya magari, viwanda vidogo vidogo. Yamezungumzwa haya na Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Abdula Suleiman Lutavi, Mheshimiwa Maria Watondoha na Mheshimiwa Remidius Kissassi. Ni kweli miji mingi iliyotengenezwa *Master Plan* zamani, zoezi linaloendelea ni kuipitia mipango hiyo kwa kushirikiana na Halmashauri husika na kuandaa mipango yakiniifu. Tunahitaji *Urban Development Plans* ambayo inazingatia zana ya ushirikishwaji kwa wadau mbalimbali. Michoro inapoandaliwa inazingatiwa kutenga maeneo ya huduma mbalimbali ni vema Halmashauri husika isimamie utekelezaji ili matumizi ya ardhi yaliyopangwa yasibadilishwe bila kuzingatia taratibu zilizowekwa. (*Makofi*)

Pia Mheshimiwa Aridi Uledi, alizungumzia kwamba miji midogo inahitaji kuandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi. Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri mbalimbali inaandaa mipango ya matumizi

ya ardhi kwa ajili ya miji midogo. Kama nilivyoelezea katika hotuba suala hili lilitiwa mkazo. Tayari ya mipango ya miji kama Makambako, Karatu, Vuawa, Tunduma, Lushoto na Masasi inashughulikiwa. Utaratibu utaendelezwa kwa miji mingine midogo. *(Makofi)*

Pia amezungumzia upo umuhimu wa Serikali kuanzisha utaratibu wa kutoa mikopo kwa ajili ya ujenzi au ununuzi wa nyumba. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, tayari imeandaa taarifa ambayo itawasilishwa Serikalini ili kupata idhini hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameeleze kwamba tuboresha makazi mijini hasa yaliyojengwa bila mpango wa kutekeleza utaratibu wa *regularization*. Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga hili kalizungumzia kwa kirefu. Maelekezo ya kutekeleza miradi ya *regularization* yametolewa katika Sheria namba 4 ya mwaka 1999 na Sera ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000. Wizara yangu itasimamia utaratibu huo kwa kushirikiana na Halmashauri zinazohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi pia katika viwanja 20,000 Dar es Salaam. Haya yamezungumzwa na wengi. Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Sophia Simba, Mheshimiwa Halima Kimbau, Mheshimiwa Rhoda Kahatano, Dr. Sulemain Juma Omar. Ni kweli tangu mwaka 1984 Serikali haijaweza kupima viwanja vingi mjini kutokana na ukosefu wa fedha za kulipia fidia. Kuweka miundo mbinu na gharama za umilikishaji inayojumuisha kupima, kugawa na kutoa hati miliki, matokeo yake ni upungufu mkubwa wa viwanja katika miji na tuhuma nyingi za rushwa katika ugawaji wa viwanja, vichache vilivyopatikana. Ni katika kutekeleza mradi huu wa viwanja 20,000 Mkoa wa Dar es Salaam, wananchi na viongozi wa Jiji na Mkoa wa Dar es Salaam walishirikishwa kikamilifu. Tangu mwanzo wa mradi ulipobuniwa mpaka mwisho katika ugawaji wa viwanja.

Ushirikishaji huu ulifanyika katika maeneo yote 11 ya mradi ambao ni Twangoma, Buyuni, Mwanagati, Kisota, Bunju, Mivumoni, Mbweni, Mtoni Kijiti, Boko Dovia, Mbweni JKT na Vijibweni. Mkutano wa ufahamisho wa mradi ulifanyika katika ngazi mbalimbali. Mkutano wa kwanza ulifanyika kwa viongozi wa Mkoa katika Ukumbi wa Manispaa Kinondoni tarehe 28/8/2002. Mkutano wa pili ulikuwa wa Waheshimiwa Madiwani na Mheshimiwa Sophia Simba, alikuwa mmojawapo kama Diwani wa pale. Waheshimiwa Madiwani wa Kamati ya Mipango Mji na Mazingira katika Ukumbi wa Kalimjee tarehe 3/9/2000. Mkutano wa tatu wote wa maeneo wa mradi ilifanyika katika kumbi za kila Manispaa za Dar es Salaam. Temeke mkutano huu ulifanyika tarehe 10/9/2000, Ilala ulifanyika tarehe 11/9/2000, Kinondoni ulifanyika tarehe 12/9/2000. Katika mikutano yote hii Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi na Maendeleo na Makazi na Wakurugenzi wake walieleza viongozi wa Mkoa na Manispaa madhumni na mipango ya utekelezaji wa mradi huu na kujibu hoja zote za viongozi. *(Makofi)*

Aidha amekutana na wananchi wote kwenye maeneo yao ya mradi na mimi ni mmojawapo ambaye nilifika katika eneo la Twangoma. Kwa hiyo, si kweli kwamba wananchi hawana habari, Si kweli kwamba wananchi wamenyang'anywa viwanja. Naomba nirudie tena wananchi wamepewa nafasi ya kupewa viwanja katika maeneo ambayo wanayoishi. Akikubali anatoa fedha kidogo kwa ajili ya maendeleo yatakayofanyika, wala haizidi shilingi shilingi 50,000, wala 100,000 lakini siyo kwamba wanauziwa. Kama kweli wanauziwa mimi naomba niambiwe au tufuatane twende tukakutane tena na Viongozi wa Halmashauri akiwemo Meya, Mkurugenzi, Mkuu wa Wilaya, Madiwani, Wenyeviti wa Serikali na sisi wenyewe Wabunge. *(Makofi)*

Lakini jambo hili hakuna mtu atakayejitokeza kwamba ameuziwa kiwanja. Kilichofanyika baada ya yeye kutambua kwamba hili eneo ndilo nitakalojenga, sasa linalobakia wanagawiwa wananchi wengine kwa kawaida. Wale ndiyo wanatoa thamani ya pale palipo. Lakini na yeye pia haachwi mtupu inabidi athamini maeneo yale ambayo yeye hakuchukua. Kama kulikuwa na miembe, kama kulikuwa na nyumba nyingine licha ya ile anayoishi, kama kulikuwa na mifenesi, mapapai, viazi wanaolima Wanyamwezi wenzangu kule wamepewa kutokana na thamani ya mali. Huwezi kutegemea ukapewa milioni moja thamani ya mwembe mmoja. Ukapewa milioni kumi kwa thamani ya mnazi mmoja. Tuwe wakweli, hakuna aliyeondoka mtupu na kama kuna kitu alichotoa ni kwa sababu ya miundo mbinu iliyowekwa pale na ndiyo na yeye anachangia.

Kwa hiyo, jamani naomba tusiwapotoshe wananchi. Wamepewa fidia zinazostahili fidia yao na wamepewa viwanja. Jambo ambalo Waziri hapa alilijibu siku moja akasema kwamba hatuwezi kufanya vya ukoo kwa sababu wanataka huyu mjukuu, huyu mtoto, haiwezekani mbona vijiji vya ujamaa tuliamishwa mwaka 1974? Hatukusema mimi siondoki kwa sababu babu yangu amekufa hapa? Sasa sembuse leo iwe nongwa viwanja 20,000 wakati ule ilikuwa na sasa imekuwaje? Ni kwa manufaa ya wananchi. Kwa faida yetu sisi kwa ajili ya kutengeneza mji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba Waheshimiwa Wabunge kama kuna matatizo hebu njooni mlango wangu ofisini uko wazi, Katibu Mkuu uko wazi, Wakurugenzi wote milango iko wazi. Hakuna Mbunge aliyefika katika Wizara yetu akakataliwa kumwona kiongozi yeyote yule. Kama kuna tatizo la msingi, tulateeni ndugu zangu tulitatie kwa sababu hapa ni maneno tu. Lakini tukienda kwenye *service* nafikiri tutakuwa mahali pazuri na muafaka kwa kuweza kuwasaidia wananchi wetu. Pengine leo hasikilizi kwenye redio, sasa atajuaje kwamba kweli umemsaidia?

Lakini tukiongea ana kwa ana na yeye yuko pale nina hakika ataona kwamba Mbunge wangu, Diwani wangu amefanya kazi ambayo nataka anifanyie. Kwa hiyo, nawaomba wote wenye matatizo ya viwanja 20,000 basi njooni ofisini hata kesho Wakurugenzi wapo, wanakuwa wamejaa, njooni tuambizane. Wale wateja ambao wako kule basi tuko tayari kuwafuata lakini hili jambo nakanusha, naendelea kukanusha na nitazidi kukanusha, hakuna aliyedhulumiwa kiwanja wala hakuna ambaye hakupata fidia na kama katoa fedha hakuuziwa, amechangia miundo mbinu ambayo imewekwa. Tofauti na zamani tulikuwa tunatoa tu viwanja. Sasa utafikaje kwenye kiwanja ni juu yako. Lakini sasa hivi katika mradi huu unafika kuna barabara ambayo imetengenezwa, unapata maji ambayo yamewekwa, unapata umeme ambao umevutwa pale. Tunataka nini jamani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja katika suala hili. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuhitimisha hoja yangu. Kwanza napenda kutumia fursa hii kuwatambua Waheshimiwa Wabunge, ambao wamepata nafasi ya kuchangia hoja yangu. Waliochangia kwa kuzungumza humu Bungeni ni Waheshimiwa 16 ambao ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Kidawa Hamis Saleh kwa niaba ya Kamati ya Kilimo na Ardhi, Mheshimiwa Ali Said Salim Msemaji Mkuu wa Upinzani, Mheshimiwa Kisyeri Chambiri, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Dr. Suleiman Juma Omar, Mheshimiwa Sophia Simba, Mheshimiwa Halima Kimbau, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Mheshimiwa Monica Mbega, Mheshimiwa Rhoda Kahatano, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Profesa Juma Mikidadi, Mheshimiwa Frank Magoba na Mheshimiwa Tatu Ntimizi Naibu Waziri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge 34 nao naomba niwatambue ambao ni Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Stephen Kazi, Mheshimiwa Sophia Simba, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Hamisi Nguli, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Juma Kidunda, Mheshimiwa Mwandini Abass Jecha, Mheshimiwa Salim Omar Ali, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Abu Towagale Kiwanga, Mheshimiwa Profesa Juma Maghembe na Mheshimiwa Aridi Uledi,

Wabunge wengine ni Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, Mheshimiwa Maria Watondoha, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Lucas Seleli, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro, Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Major Jesse Makundi, Mheshimiwa John Magufuli, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali. Kama kuna ambaye nimemsahau basi tuarifiane. Lakini nimejitahidi kuwataja wote ambao wamepata nafasi ya kuchangia.



Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha wapo Waheshimiwa Wabunge ambao walipata nafasi ya kuchangia katika hoja zilizopita za Waziri wa Fedha, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Waziri Mkuu na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Sasa nao ningependa niwatambue waliochangia katika hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Lucas Seleli, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Christopher Wegga, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Musa Lupatu, Mheshimiwa Talala Bana Mbise. (*Makofi*)

Waliochangia hotuba ya Waziri Mkuu na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ni Mheshimiwa Stanley Kolimba, Mheshimiwa Dr. James Msekela, Mheshimiwa Maria Watondoha, Mheshimiwa Hamisi Nguli, Mheshimiwa Sophia Simba, Mheshimiwa Benedict Losurutia, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Philip Marmo, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Talala Bana Mbise, Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, Mheshimiwa Dr. Chegeni Masunga, Mheshimiwa Christopher Wegga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wote nawashukuru sana kwa michango yao yote ambayo ilielekezwa katika Sekta ya Ardhi na Makazi. Tunashukuru kwa michango yao mizuri ya kututia moyo na ambayo itatusaidia kuboresha mbinu na mikakati ya utekelezaji wa bajeti yetu na mipango yetu kwa mwaka wa fedha 2003/2004. Tumekwisha tayarisha majibu ya maandishi kwa Waheshimiwa Wabunge waliochangia katika hoja zilizopita na tumekwisha wagawia. Waliochangia katika hoja zilizopita na hawa waliochangia katika hoja hii kwa kuzungumza na kwa maandishi tuna tayarisha majibu ya maandishi na wote watapata siku chache zijazo.

Nkumshukuru Mheshimiwa Tatu Ntimizi Naibu Waziri kwa kunisaidia kujibu hoja nyingi za Waheshimiwa Wabunge. Mimi nitajitahidi kujibu baadhi ya hoja ambazo hazijajibiwa na kutoa ufafanuzi na msisitizo katika masuala machache tu yaliyojitokeza katika michango ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza nipitie hoja zilizotolewa na Kamati ya Kilimo na Ardhi. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh kwa uwasilishaji wake mzuri Taarifa ya Kamati. Napenda kurudia tena kuwashukuru wajumbe wote wa kamati hiyo kwa michango yao mizuri katika kupokea na kuunga mkono mapendekezo na ushauri wao napenda kusema machache tu kama ifuatavyo:-

Kwanza, hoja ya kuwa na chombo cha kutoa mikopo kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa nyumba nchini kama nilivyosema kwenye hotuba yangu kwa kweli tumefikia hatua ya kuridhisha. Napenda nimtoe hofu Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga kwamba hatua tuliyofikia nina hakika kama, nilivyosema katika mwaka wa fedha 2003/2004 bila shaka tunaweza ku-*take off*. Kwa hiyo tuwe na subira nadhani tumepiga hatua nzuri tu.

Kuhusu maendeleo katika miji yetu sheria zipo na taratibu zipo tunachomba kwa kweli napenda kusisitiza watendaji katika Halmashauri zetu zote, wazingatie sheria na miongozo ambayo ipo kwa ajili ya kuendeleza miji yetu. Wawaelimishe wananchi na wataalam wenyewe waizingatie na waisimamia katika uendelezaji wa miji yetu ili miji yetu ijengwe kwa mujibu wa sheria na Kanuni na miongozo ambayo ipo. Tusiwe kama ni watu ambao ni wakimbizi hatujafika kwenye nchi yetu. Hii ni nchi yetu tuna sheria, tuna mipango, tuna miongozo basi tujenge, tukae kama watu ambao wana nchi yao na miji yao wanaipenda ambayo imepangwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, yote ambayo yamependekezwa katika Taarifa ya Kamati ya Kilimo na Ardhi kwa ufupi Wizara yangu inayapokea na inayakubali na tutayafanyia kazi. Mengi kwa kweli ndiyo hayo ambayo tunayashughulikia sasa hapa ni msisitizo tu kwamba hayo yote ambayo yamependekezwa ndiyo yako katika mipango yetu na tutaendelea kuyatekeleza na *Inshallah* mwakani kama tutakuwepo basi katika taarifa ya utekelezaji Kamati itaona jinsi tunavyoendelea kutelekeza yale

ambayo wameyapendekeza ya kutusaidia kutushauri kwa ajili ya utekelezaji wa Bajeti ya mwaka ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme hivyo kwa kuwa tunayapokea hakuna haja ya kuyarudia moja moja. Tungekuwa tunapingana basi tungeweza kufafanua. Lakini kwa kuwa tunayapokea basi nashukuru tunayapokea na tutayafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mchango wa Mheshimiwa Ali Said Salim Msemaji Mkuu wa Upinzani. Kwanza namshukuru kwa mchango wake mzuri kwa kipindi kifupi amejitahidi kupitia nyaraka mbalimbali ambazo nimempatia ili kumsaidia kuelewa sera, sheria na mipango mbalimbali ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo na Makazi. Hata hivyo ni dhahiri kwamba ipo haja ya kuendelea kuelimishana kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu Sekta ya Ardhi na Makazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumechambua mchango wake na tumeainisha hoja kama 26 na zote tumezitolea maelezo. Sasa kwa kuwa ni nyingi aniruhusu tu kwamba nisipitie moja moja lakini tutamkabidhi ili aweze kupitia hoja moja moja na tutaendelea kushirikiana na kushauriana kadri tunavyoendelea. Lakini tunamshukuru kwa mchango wake nadhani ni mwanzo mzuri, basi tutakiane kila la kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nilidhani nipitie kwa ufupi masuala machache tu ya jumla na maalum. Kwanza suala la migogoro ya mipaka ndani ya nchi. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge, kwamba Serikali hailifanyii mzaa suala hili, bali inalipa uzito unaostahili. Mamlaka zipo zinazowajibika na suala hili kuanzia ngazi ya kijiji hadi taifa. Tatizo ni kutozingatia na kutii makubaliano na maelekezo yaliyoko kwenye *Government Notice* halali za kisheria zinazotangazwa. Wataalam wa Ardhi hawaamui mipaka iwe vipi au mpaka uwe wapi. Bali wanatafsiri kitaalam makubaliano ya pande mbili zinazohusika katika mgogoro kuweka alama za mpaka kwenye ardhi. Naomba viongozi na wananchi katika ngazi ya vijiji na Wilaya wawe tayari kukaa pamoja kuzungumza na kukubaliana mipaka ya maeneo yao na kisha watii na kuheshimu makubaliano yao. *(Makofi)*

Mipaka inayowekwa ni alama tu ya kiutawala na haikusudii kuwagawa na kuleta uhasama miongoni mwa wananchi wa Tanzania. Wizara yangu itaendelea kuwasiliana na wenzetu wa TAMISEMI, ambao ndiyo wasimamizi wakuu wa masuala haya ili tushauriane jinsi ya kuimarisha usimamizi na kuepuka migogoro hii ya mipaka ndani ya nchi ambayo ni aibu kwetu wote. *(Makofi)*

Kwa hiyo, rai yangu kwa wananchi na viongozi mahali popote nchini, iwe kwenye Vijiji na Wilaya tuwe na tabia ya kukaa kuzungumza na kukubaliana na tukisha kukubaliana tutii yale ambayo tumekubaliana na yaliyowekwa kisheria ili tuweze kuishi kwa amani na mshikamano katika Taifa letu. *(Makofi)*

Suala la pili, mradi wa viwanja 20,000 Dar es Salaam. Napenda kuwashukuru wote waliochangia kuhusu suala hili. Wote wameunga mkono mradi huu, lakini baadhi wametaja mapungufu hapa na pale. Tunatiwa moyo kwa kuungwa mkono na tumesikia ushauri wa kuboresha utekelezaji, tunaupokea na tutaufanyia kazi kwa kushirikiana na wenzetu wa Mkoa wa Dar es salaam, Jiji na Manispaa zote tatu. Naomba Waheshimiwa Wabunge wote wa Mkoa wa Dar es Salaam wa Majimbo na Viti Maalum, tushirikiane na tushauriane mara kwa mara kwenye vikao vyetu ili kufanikisha utekelezaji wa mradi huu. *(Makofi)*

Kwa upande wa Serikali tutaendelea kushauriana na wenzetu wa Wizara ya Fedha, kuhusu uwezeshwaji wa Wizara yetu kutekeleza miradi ya maendeleo kama huu wa viwanja 20,000 vya Dar es Salaam. Natumaini tutafikia muafaka mzuri. Wengi mmetoa rai kwamba fedha ya maendeleo haitoshi na sisi tunakubali. Natumaini tutaendelea na mazungumzo hali ikiruhusu tuweze kupata fungu kubwa zaidi ili tuendeleo na kazi hii muhimu ya kuweza kuboresha miji yetu upatikanaji wa viwanja vingi kwa wingi na haraka ili kuendana na kasi ya wananchi wanaohamia mijini na ambao hawana mahali pa kuweza kupata viwanja. Kwa hiyo, hili tutaendelea kushirikiana tunashukuru kwa michango yenu mmetutia moyo na nguvu na tutaendelea kushirikiana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu vita dhidi ya rushwa. Tunashukuru kwa pongezi ambazo Waheshimiwa Wabunge, wamezitoa kwetu. Tunatiwa moyo katika jitihada zetu hizi za vita dhidi ya rushwa ndani ya Wizara. Vita hii ni ya kudumu. Sisi tutaendelea kupigana katika maeneo tuliyo na madaraka nayo. Mimi nina madaraka katika Wizara.

Hayo madaraka ninayo na tutaendelea kuyatumia, Mwenyezi Mungu atusaidie. Lakini natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge ingawa wengine hawapendi niseme hivyo kwamba vita dhidi ya rushwa katika Sekta ya Ardhi na Makazi kwenye Halmashauri zetu ni jukumu letu sisi Wabunge na viongozi wenzetu kwenye maeneo hayo. Naomba tuendelee kushirikiana kadri tuwezavyo ili kusafisha uchafu wowote wa rushwa katika ngazi zote, tutende zaidi kuliko kulalamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na utaratibu wa kuwa na Mkutano wa Wizara kila mwaka na mwaka huu baada ya Mkutano wa Bunge hili tutakuwa na Mkutano wa mwaka wa Wizara yetu na tunawashirikisha Watendaji wa Sekta ya Ardhi na Makazi nchi nzima kutoka kwenye Halmashauri zote. Tutakuwa na Mkutano hapa Dodoma. Sasa Wizara inachoweza kufanya ni kukumbushana na kuelekezana kwamba tutende kazi zetu kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu. Lakini usimamizi wa siku kwa siku Wizara hatuna, uko kwenu huko! Sasa sisi tutaendelea kukumbushana na kuhamasishana, lakini usimamizi wa siku kwa siku ni wenu na viongozi walioko kwenye Halmashauri zetu.

Katika michango ya Waheshimiwa Wabunge kuna wengine walisema tutakupa majina, tutakupa mifano na nini, mimi napokea. Nipeni. Kwa kuwa wakuja, nipeni kama kuna mifano kuhusu Sekta ya Ardhi na Makazi katika Halmashauri yenu. Kwenye wasiwasi, kwenye matatizo nipeni, maana wakuja, tutazungumza. Kuna baadhi wameshanipa, tutazungumza. Tunaambiana ukweli, wee bwana unatutia aibu. Heshima ya Wizara yetu nzuri, hatutaki ichafuke toka Makao Makuu mpaka kwenye Halmashauri. Sasa tusaidiane, tushirikiane. Hiyo ndio rai yangu kwamba tushirikiane, kazi hii ni ngumu kwa hiyo lazima tuifanye wote kwa kushirikiana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Waheshimiwa Wabunge mbalimbali wametoa michango yao mingine hatukuweza kujibu, inahitaji mazungumzo na pengine mashauriano zaidi. Kwa hiyo ningewaomba Waheshimiwa wafuatao kwa nafasi zao kuanzia Jumatatu, tunaweza kukutana ili tuzungumze na tupate maelezo zaidi na ufafanuzi zaidi kwa hoja mbalimbali ambazo wamezitoa.

Mheshimiwa Chambiri, Mheshimiwa Makongoro, Mheshimiwa Kwaangw', Mheshimiwa Janguo na wengine ambao watakuwa tayari. Sisi tuko tayari. Wataalam wangu wako hapa mpaka wiki ijayo, kwa siku mbili tatu watakuwepo. Kama kuna eneo linahitaji kuzungumzwa na kushauriana ana kwa ana, tafadhali naomba tuonane ili tuweze kuyazungumza hayo tuyamalize hapa hapa Dodoma kabla hawajarudi Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia napenda kutumia nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuru wananchi wa Ileje kwa mshikamano wao katika jitihada za kujiletea maendeleo yetu na kwa imani na ushirikiano wao kwangu. Tuendelee kutimiza wajibu wetu na Mungu atusaidie. *(Makofi)*

Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano wenu mwema kwangu na Wizara yangu kwa ujumla. Tunaomba radhi kwa upungufu wowote ambao umejitokeza, tuendelee kushirikiana kwa manufaa ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 48 - Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi**

Kif. 1001 - <i>Administration and General...</i>	Shs. 1,561,998,300/=
Kif. 1002 - <i>Finance and Accounts</i>	Shs. 636,174,600/=
Kif. 1003 - <i>Policy and Planning</i>	Shs. 187,304,500/=
Kif. 1004 - <i>Management Information System...</i>	Shs. 96,952,400/=
Kif. 2001 - <i>Land Development</i>	Shs. 815,894,000/=
Kif. 2002 - <i>Surveys and Mapping...</i>	Shs. 793,941,000/=
Kif. 2003 - <i>Customary Land Tribunal...</i>	Shs. 203,173,800/=
Kif. 3001 - <i>Human Settlements Development...</i>	Shs. 830,154,200/=
Kif. 3003 - <i>Housing Appeal Tribunal</i>	Shs. 288,336,100/=

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo Juu Vilipitishwa na Kamati bila Mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 48 - Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi**

Kif. 1004 - <i>Management Information</i>	Shs. 214,200,000/=
Kif. 2001 - <i>Land Development</i>	Shs. 155,000,000/=
Kif. 2002 - <i>Survey and Mapping</i>	Shs. 230,800,000/=

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo Juu Vilipitishwa na Kamati bila Mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2003/2004 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Kwa hiyo naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka 2003/2004 yalipitishwa na Bunge)*

*(Saa 12.38 Jioni Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumatatu Tarehe 21 Julai, 2003 Saa Tatu Asubuhi)*

